# NAFASI NA ATHARI YA KIONGOZI WA KIKE KATIKA TAMTHILIA TEULE ZA KISWAHILI

**SYEKEI MARTHA NYANGWESO**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA KATIKA KITIVO CHA SANAA NA SAYANSI ZA KIJAMII ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI.**

**CHUO KIKUU CHA MAASAI MARA**

**2017**

## HATILINZI

Martha Nyangweso Syekei © 2017

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kuiga, kupigisha chapa, kutafsiri na kuitoa kazi hii kwa njia yoyote ile bila idhini kwa maandishi kutoka kwa mwandishi wa tasnifu hii au Chuo Kikuu cha Maasai Mara.

## TABARUKU

Kazi hii ninaitabarukia watoto wangu Vivian Kemunto na Margaret Bwari. Mmekuwa msukumo wangu wa kweli.

## SHUKURANI

Tasnifu hii haingekamilika kama si bidii na roho ya usambe kutoka kwa wahusika mbalimbali na mawaidha yao yaliyonifaa ili nifike hapa.

Kwanza ningependa kumshukuru Maulana kwa mapenzi yake kwangu hasa kunipa uhai na afya njema. Uinuliwe na upewe sifa daima na milele. Shukrani zangu za dhati kwa wasimamizi wangu Dkt. Nancy Ayodi na Prof. Sangai Mohochi. Ushauri wao, uelekezi na kujitolea kwao kumeniwezesha kuikamilisha tasnifu yangu vizuri sana.

Aidha ninawashukuru wahadhiri wote wa Idara ya Lugha, Isimu, Mawasiliano na Uandishi wa Habari kwa hekima mliyoniongezea. Wahadhiri hasa walionifunza ni pamoja na Dkt. Ontieri Omari, Dkt. Kisurulia Simiyu, Prof. Sangai Mohochi, Dkt. Ayodi Nancy na Dkt. Obuchi Moseti.

Ninawashukuru pia wasomi wenzangu tulioshirikiana na kushauriana nao kuhusu masuala mbalimbali ya lugha ya Kiswahili. Wao ni Frida Oiko, Teresa Nyanumba, Ayiera Elijah, Onduso Zachary, Gladys Morwabe, Kisia Issa Ahinga na Ombaba Wilbert. Asanteni.

Kwa mume wangu Elijah Syekei, ufadhili wako na kunipa matumaini kuendelea na utafiti, baraka zake Mola ziwe nawe daima na milele. Kwa watoto wangu Vivian Kemunto na Margaret Bwari ninawashukuru kwa kunipa motisha kuwa nitamaliza kisomo changu vyema. Bila shaka ndoto yenu imetimia. Ari yenu ya kuniona nimefuzu Mola na awajalie mema mnapokua.

Marafiki zangu wote walionihimiza niendelee nilipolemewa, hususan Naomi Nyaboke na Mary Nyamori. Mungu na awabariki siku zote. Kwa Florence Ongaki wosia wako ulinifaa sana. Ulipo kuzimu tuombee nasi. Shukrani kwa Frida Oiko kwa kuisoma kazi hii mwishoni. Mola na akubariki sana.

Kwa wote walionifaa kwa njia moja au nyingine na sikuwataja ninawashukuru sana na Maulana awabariki sana.

## IKISIRI

Fasihi ni kioo cha jamii. Fasihi imekuwepo tangu jadi. Fasihi hunuia kufunza mada kuu katika jamii kama vile; mila, itikadi, dini, miiko, imani, matambiko, tamaduni za kale, utawala na kadhalika. Mambo haya yana nguvu mahsusi katika jamii. Fasihi kama katiba yoyote ile, huelimisha, huhifadhi tamaduni na pia kuburudisha. Utafiti huu ulilenga kuchunguza na kutathmini nafasi na athari ya kiongozi wa kike katika tamthilia teule za Kiswahili. Tamthilia ikiwa utanzu mmojawapo wa fasihi andishi ziliteuliwa ili kutufaa. Malengo ya utafiti huu yalikuwa ni kuchanganua dhana ya uhusika katika tamthilia husika. Tulipambanua na kuchanganua nafasi ya viongozi wa kike na tukatoa tathmini ya athari yao kwa kuwasilisha sifa zao na mwelekeo wao katika jamii husishi. Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Ufeminsti wa Kiafrika. Hali lengwa halisi ni ya jamii nyingi za bara za Afrika kihadhi na kitamaduni. Katika kuendeleza utafiti huu tulitumia mbinu kusudio ili kuteua tamthilia za *Kilio cha Haki, Posa za Bikisiwa*, *Sudana* na *Pango*. Njia ya ukusanyaji data ilikuwa ya kuhakiki matini. Data iliyopatikana ilichanganuliwa kwa kuzingatia malengo, maswali na nadharia ya utafiti na matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kwa njia ya kimaelezo. Utafiti huu utasaidia kuelewa nafasi na athari ya kiongozi wa kike kwa mujibu wa waandishi watukuka katika Kiswahili. Masuala ya kimsingi ya utafiti yalilengwa sawasawa. Utafiti huu pia uliangazia dhana ya uhusika, uteuzi wa wahusika kutoka tamthilia teule na muhtasari wa tamthilia zilizofaa utafiti huu. Uchunguziwa kina wa nafasi chanya na hasi ya kiongozi wa kike ulifanywa. Uchanganuzi wa athari na changamoto zinazomkabili kiongozi wa kike ulishughulikwa.Hatimaye muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti wetu ulifikiwa.Utafiti wetu vilevile ulinufaika kutoka kwa marejeleo mbalimbali vitabuni na wavuti tuliyoyapitia ili kukusanya data iliyolenga mada ya utafiti. Dhamira kuu ya utafiti huu ililenga ushirikiano, uana na suala zima la mapinduzi ya kijamii, kisiasa, kiutamaduni na kiuchumi. Utafiti huu ulizamia mada ya utafiti kwa kina ili kufikia upeo wa juu katika utafiti, daraja ya uzamili. Matokeo yatakuwa na mchango mkubwa katika fasihi ya lugha ya Kiswahili kwa ujumla.

# ABSTRACT

Literature is any work of creative imagination deemed to have artistic or intellectual value that deploys language in a way that differs from ordinary usage. It includes spoken and sung texts. The very basic forms of literature include: poetry, drama, fiction and non fiction. Literature feeds the soul and for great literal scholars it is the only asset that gives a clear picture of a given society. Great literal works resonate readers across centuries by telling the human condition today as it was when printed word was first produced. Literal works are a central part of many lives by providing a gateway to a deeper level of thought by unlocking culture of a time period, giving wisdom to modern society, broadening the mind as well as helping one write well. Little attention has been given on the role and challenges faced by the women leaders in Africa. On this basis, our research has deemed it fit to critically examine and analyse content to highlight on their role and influence in the larger society. This research fully examined and explained the role and challenges faces by women leaders. Our main concern was to know if women leaders had realized their cross gender relations and attitudes as leaders inorder to fully understand their society. Our research was focused on analysing content from four Kiswahili written plays commonly known as drama. The plays to analyse were*; Kilio cha Haki, Pango, Sudana* and *Posa za Bikisiwa*. Drama genre potrays serious presentations or stories that show realistic characters in conflict either with themselves, others or forces of nature. This genre showed human beings at their best, worst and everything in-between. Our main area of study was the theme of leadership. This theme has played a large role in developing the plot of the selected plays. It helped develop character, role and influence the women leaders had on the diverse societies the plays were staged. According to the feminist literary theory, which was used as a guide in the analysis of the data in this study, women leaders threaten the men domain. Leadership was a men domain for centuries in many African societies. Due to world awakening and change of guard, affirmative action has taken centre stage. Despite the many challenges faced, women leaders now are having a positive influence in many African societies. Purposive sampling was used due to its reliability for our study. By employing it we were able to get representative information about the study topic. The results of this study have shed light on societal attitudes towards women leaders. This research would be of great importance to Kiswahili readers and reseachers of literature. This study has also identified and recommended topics of future research in literal works related to this area.

**YALIYOMO**

**MADA**.................................................................................................................i
**UNGAMO NA IDHINI**..........................................................................................ii
**HATILINZI**........................................................................................................iii
**TABARUKU**........................................................................................................iii
**SHUKURANI** ......................................................................................................iv
**IKISIRI** ..................................................................................................................v
**ABSTRACT**..........................................................................................................vi
**YALIYOMO**.........................................................................................................vii

**SURA YA KWANZA** ..............................................................................................1
**MISINGI YA UTAFITI** ..........................................................................................1
1.1 Utangulizi..............................................................................................................1
1.2Usuli wa Mada ........................................................................................................1
1.3 Suala la Utafiti .......................................................................................................2
1.4 Malengo ya Utafiti .................................................................................................2
1.5 Maswali ya Utafiti..................................................................................................2
1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti.....................................................................................3
1.7 Sababu za Kuchagua Mada .....................................................................................3
1.8 Umuhimu wa Utafiti ...............................................................................................4
1.9 Msingi wa Kinadharia.............................................................................................4
1:10 Mapitio ya Maandishi ..........................................................................................9
1.11 Mbinu za Utafiti ..................................................................................................15
1.11.0 Utangulizi..........................................................................................................15
1.11.1 Muundo wa utafiti.............................................................................................15
1.11.2 Eneo la utafiti ...................................................................................................15
1.11.3 Idadi Lengwa ....................................................................................................15
1.11.4 Uteuzi wa Sampuli ............................................................................................15
1.11.5 Ukusanyaji data.................................................................................................15
1.11.6 Uchanganuzi na uwasilishaji data ......................................................................16

**SURA YA PILI**.........................................................................................................17
**MUHTASARI WA TAMTHILIA TEULE** ..............................................................17
2.1 Utangulizi...............................................................................................................17

2.2 Dhana ya Tamthilia........17
2.3 Historia Fupi ya Tamthilia Teule........17
2.3.1 Tamthilia ya *Kilio cha Haki*........17
2.3.2 Tamthilia ya *Pango*........18
2.3.3 Tamthilia ya *Sudana*........19
2.3.4 Tamthilia ya *Posa za Bikisiwa*........19
2.4 Dhana ya Wahusika........19
2.5 Uteuzi wa Wahusika........21
2.5.1 Uteuzi wa Lanina kama Kiongozi wa Kike.........21
2.5.2 Uteuzi wa Katango kama Kiongozi wa Kike........22
2.5.3 Uteuzi wa Sudana Kama Kiongozi wa Kike........22
2.5.4 Uteuzi wa Bikisiwa kama Kiongozi wa Kike........23
2.6 Hitimisho........23

**SURA YA TATU........24**
**NAFASI YA KIONGOZI WA KIKE KATIKA TEULE ZA KISWAHILI........24**
3.1Utangulizi........24
3.2Nafasi Dhalilishi na Duni ya Kiongozi Mwanamke........24
3.2.1 Mwanamke Kuteswa Kwa Sababu ya Maumbile........26
3.2.2 Mwanamke kama Chombo cha Kumfurahisha Mwanamume........30
3.2.3 Kanuni za Utamaduni Kutomtambua Kiongozi wa Kike.........34
3.2.4 Utamaduni na Ugavi wa Kazi Unaomkandamiza Mwanamke Kiongozi.........35
3.2.5 Mwanamke kama Kizingiti cha Ukombozi wa Mwanamke Mwenzake........38
3.2.6 Mwanamke kama Kiumbe Asiyeweza Kuongoza........40
3.3 Nafasi Chanya Anayopewa Kiongozi Mwanamke........45
3.3.1 Mwanamke kama Kiongozi Jasiri........45
3.3.2 Mwanamke kama Mlezi Mwema.........51
3.3.3 Mwanamke kama Mtu Mwerevu na Mwenye Akili Tambuzi........52
3.3.4 Mwanamke Msanii wa Lugha........56
3.4 Hitimisho........57

**SURA YA NNE** .......... **58**
**ATHARI INAYOMKABILI KIONGOZI WA KIKE KATIKA TAMTHILIA TEULE ZA KISWAHILI** .......... **58**
4.1 Utangulizi .......... 58
4.2 Asasi za Kitamaduni .......... 58
4.2.1 Asasi ya Ndoa .......... 58
4.2.2 Mila na Itikadi .......... 62
4.3 Masuala ya Kiuchumi Yanayofafanua Harakati za Ukombozi .......... 65
4.3 Hitimisho .......... 68

**SURA YA TANO** .......... **69**
**MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO** .......... **69**
5.1 Utangulizi .......... 69
5.2 Muhtasari wa Utafiti .......... 69
5.3 Matokeo ya Utafiti .......... 69
5.3 Mahitimisho .......... 75
5.4 Mapendekezo .......... 75
**MAREJELEO** .......... **77**
**KIAMBATISHO A: MASWALI YA KULENGA ILI KUPATA DATA YA UTAFITI HUU** .......... **81**
**KIAMBATISHO B: KIBALI CHA UTAFITI** .......... **84**
**KIAMBATISHO C: BARUA YA KUIDHINISHWA KUTAFITI NYANJANI** .......... **81**

# SURA YA KWANZA

# MISINGI YA UTAFITI

## 1.1 Utangulizi

Katika sura hii ya kwanza tunajadili masuala ya kiutangulizi ya utafiti huu. Masuala tunayozingatia ni suala la utafiti, malengo ya utafiti, nadharia tete, upeo na mipaka ya utafiti, sababu za kuchagua mada hii na umuhimu wa utafiti huu. Vilevile, tunachambua msingi wa kinadharia, mapitio ya maandishi na mbinu za utafiti. Masuala haya ni muhimu sana kwa sababu yatatupa mwongozo imara katika utafiti wetu. Utafiti wetu utachunguza iwapo waandishi wanaume wamefaulu katika kumsawiri kiongozi wa kike kwa kutambulisha nafasi yake bayana katika jamii.

## 1.2Usuli wa Mada

Utafiti huu umechunguza nafasi ya viongozi wa kike katika tamthilia za *Kilio cha Haki* (1981), *Sudana* (2006), *Posa za Bikisiwa* (2008)na *Pango* (2003). Wasanii mbalimbali wameshiriki vita hivi katika harakati za kumkomboa mwanamke. Kulingana na Mukobwa (1987), wasanii hudhihirisha vipawa vyao kwa namna tofauti tofauti. Waandishi hawa wana imani kwamba matatizo yanayowakabili wanajamii yanaweza kutatuliwa. Kazi zao zinatoa suluhu ya kufikia hali iliyo shwari. Waandishi hawa huwa wa kimapinduzi. Huwa na ndoto ya kuwa na jamii mpya inayowahimiza watu katika harakati za kujiendeleza na kujikomboa. Kwa maoni yetu, vita vya ukombozi wa mwanamke ni vita vya kijamii na hivyo basi wanaume kwa wanawake wanapaswa kushiriki kwa njia moja au nyingine. Na kama anavyosema Mugambi (1982), fasihi ni silaha mojawapo katika ghala la silaha nyingi zinazotumiwa na tabaka (kundi) moja kutetea maslahi yake katika mapambano.

Harakati za kupigania haki na usawa miongoni mwa wanaume na wanawake zimeendelea kwa muda mrefu. Haya ni tangu kuasisiwa kwa vuguvugu la Ufeministi linalohoji taswira dhaifu na dunishi ya mwanamke katika jamii. Ingawa mapambano ya vuguvugu lenyewe kwa kiwango fulani yamezalisha matunda, bado pana haja ya kuimarishwa zaidi.

Mapambano haya ni ya jinsia moja yaani ya mhusika wa kike kwa sababu ndiye aliyeathirika moja kwa moja. Hata hivyo, waandishi wa kiume wametilia chuma moto kwa kuangazia suala hili la ukombozi.

Kwa hivyo, vita vya kumkomboa mwanamke vimewashirikisha waandishi ambao wanajaribu kujenga taswira chanya ya mwanamke na wakati uo huo kuangazia vizingiti vinavyokwaza ufanisi huu wa ukombozi wake.

Katika utafiti huu, tunanuia kuchunguza ni vipi waandishi wanaume wanavyomsawiri mhusika wa kike aliye kiongozi katika tamthilia teule za kiswahili. Waandishi pia wameijenga kazi yao kwa njia teule na kuzua mambo mageni kama hadhi ya juu wanayompa mhusika wa kike.

Utafiti wetu unanuia kuchunguza namna waandishi wanaume wanavyotumia silaha hii ya fasihi katika mapambano. Pia tutazingatia mchango wa waandishi wanaume katika kuwaunga mkono wanajamii wenzao wa kike katika vita hivi. Tumechukulia kuwa hivi ni vita vya kijamii hasa nyakati hizi ambapo pana harakati za ujenzi wa jamii mpya.

**1.3 Suala la Utafiti**

Tafiti chache zimefanywa kuhusu viongozi wa kike katika fasihi ya Kiswahili. Ni katika msingi huu ambapo utafiti huu unaazimia kuchunguza na kuchanganua uongozi wa jinsia ya kike unavyoendelezwa, hasa katika kazi teule za tamthilia. Hilo ndilo pengo ambalo tunanuia kuliziba.

**1.4 Malengo ya Utafiti**

Madhumuni ya utafiti huu ni kusawiri viongozi wa kike katika tamthilia za Kiswahili. Tunadhamiria kutekeleza yafuatayo:

(a) Kuchanganua dhana ya uhusika katika tamthilia za *Kilio cha Haki, Posa za Bikisiwa, Sudana* na *Pango.*

(b) Kupambanua nafasi ya viongozi wa kike kwa wahusika wengine katika jamii zilizosawiriwa katika tamthilia za *Kilio cha Haki, Sudana, Posa za Bikisiwa* na *Pango.*

(c) Kutathmini athari ya viongozi wa kike katika tamthilia za *Kilio cha Haki, Sudana, Posa za Bikisiwa* na *Pango.*

**1.5 Maswali ya Utafiti**

Maswali ya Utafiti huu yalikuwa:

(a) Waandishi wameshughulikia vipi dhana ya uhusika wa kiongozi wa kike kwa mujibu wa tamthilia za *Kilio cha Haki, Sudana, Posa za Bikisiwa* na *Pango*?

(b) Nafasi ya kiongozi wa kike imepambanuliwa vipi kulingana na tamthilia za *Kilio cha Haki, Sudana, Posa za Bikisiwa* na *Pango*?

(c) Ni athari zipi zinazozuka kutokana na viongozi wa kike katika tamthilia za *Kilio cha Haki, Sudana, Posa za Bikisiwa* na *Pango*?

**1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti**

Tumejikita katika tamthilia teule nne za lugha ya Kiswahili. Tamthilia hizo ni; *Kilio cha Haki* (Mazrui; 1981), *Sudana* (Mazrui na Njogu; 2006), *Posa za Bikisiwa* (Mohamed na King'ei; 2008), na *Pango* (Wamitila; 2003).

Katika uhakiki wetu tumechunguza na kuthathmini nafasi na athari ya wahusika wanawake viongozi na mchango wao kufanikisha dhamira na maudhui ya uongozi katika tamthilia teule. Tumejadili wanawake viongozi, sifa zao, mwingiliano na mahusiano yao na jamii husika. Tulijikita pakubwa katika tamthilia za *Kilio cha Haki, Sudana, Posa za Bikisiwa naPango*. Hata hivyo hatuna budi kurejelea kazi zingine zenye nadharia tuliyoitumia na maandishi ambayo yameshughulikia mada yetu.

**1.7 Sababu za Kuchagua Mada**

Waandishi wa tamthilia teule: *Kilio cha Haki* (Mazrui; 1981), *Sudana* (Mazrui na Njogu; 2006), *Posa za Bikisiwa* (Mohamed na King'ei; 2008), na *Pango* (Wamitila; 2003), ni miongoni mwa wasanii wa jinsia ya kiume ambao wameandika kazi inayowasawiri wahusika wa kike kama viongozi. Wamekuwa katika mstari wa mbele kuihamasisha jamii kuhusu utangamano bora wa kijinsia. Wahakiki wengi wameshughulikia mada pana ya uhusika tu.

Sababu nyingine ya kuchagua mada hii imetokana na maono yetu ya mapambano na harakati za ukombozi. Wanawake ndio hujipigania na hujaribu kujikomboa kidesturi. Hata hivyo, waandishi hawa wa kiume *Mazrui, Njogu, Mohamed King'ei na Wamitila* wamekiuka mipaka na kuandika kazi nzuri zenye kupigania haki na usawa kwa jinsia ya kike. Kazi zao ni za hadhi ya juu za kumtambua mhusika wa kike aliye kiongozi mwenye maono na matarajio mema kwa jamii yake. Wanaume wametambua hali halisi ya utangamano na ufanisi unaotokana na mke kuwa kiongozi.

Sababu nyingine ni kwamba ni vyema suala hili liangaziwe hasa wakati huu ambapo jamii inapitia mabadiliko ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Mchango wa wanawake katika shughuli za uongozi ni bayana jinsi unavyoendelezwa katika fasihi ya Kiswahili. Uongozi wa jinsia ya kike unalenga jamii yenye kupigania usawa wa kijinsia katika karne ya ishirini na moja.

### 1.8 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utawasaidia waandishi kuelewa mambo muhimu ya kijinsia katika tamthilia za Kiswahili. Kwa wasomi utawapa mwelekeo wa uelewa jinsi ya kuchanganua maswala ya kijinsia kitaaluma. Pia utafiti huu utakuwa wa umuhimu kwa wanawake ili kuwatia hamasa kubadili hali zinazowapata. Utafiti huu pia unamulika matatizo wanayoyapitia wanawake na jinsi ya kuyatatua. Utafiti huu utawaelimisha wanawake wote jinsi ya kuongoza vyema. Mchango huu wetu utaongeza uhamasishaji wa waandishi wengine wengi wanaume wawe kiunzi muhimu katika kuleta ufanisi katika harakati za kumkomboa kiongozi wa kike na kumpa hadhi ya juu katika jamii za ubabedume.

Utafiti huu utaelimisha wanafunzi kuhusu juhudi ambazo wanawake walitumia ili kuongoza. Katika karne ya ishirini na moja, serikali nyingi zimetenga nafasi za uongozi zinazoshikiliwa na wanawake. Utafiti huu ni kichokozi na kichocheo cha fikra kwa wahakiki na wanafunzi vyuoni na katika shule za sekondari. Kama marejeleo mwafaka, utafiti huu ni muhimu kwa wasomi na watafiti katika harakati zao za kuongezea maarifa karne hii ya ishirini na moja. Ithibati iliyoandikwa inahifadhiwa kwa vizazi vijavyo na kuwa kazi rejea.

### 1.9 Msingi wa Kinadharia

Mwasisi wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ni Filomena Steady (1981) anayefafanua matarajio ya nadharia yenyewe. Nadharia hii inachunguza hali za kijamii na kitamaduni. Nadharia yenyewe inadhihirisha nia na malengo mahsusi yanayotokana na hali halisi ya jamii za Kiafrika. Inatambua historia ya jamii za Kiafrika ambazo zilikuwa na watawala na mashujaa wanawake. Inachunguza hali ya mwanamke katika jamii ambazo zimekuwa na harakati za ukombozi na ujenzi wa jamii mpya. Hivyo basi, nadharia hii ya Ufeministi wa Kiafrika ni nadharia itakayotufaa zaidi. Itatufaa katika utafiti wetu wa kumsawiri kiongozi wa kike. Kwa maoni yetu, ni nadharia mwafaka inayotetea haki na usawa wa kijinsia katika jamii.

Utafiti huu wetu utaegemea Ufeministi wa eneo la Afrika. Huu ni ufeministi unaozingatia suala la utamaduni. Ufeministi wa Kiafrika hasa ule unaohusisha fasihi inajishughulisha na hali halisi katika jamii ya Kiafrika. Nadharia yenyewe hudhamiria kuonyesha kwamba uana na uhusiano kati ya mwanamume na mwanamke ni mambo ya kati kabisa katika fasihi. Azma kuu ya nadharia hii ni 'kusoma upya' kazi ya fasihi ili kusisitiza umuhimu wa vipengele vilivyotumika. Ufeministi ni siasa ya ukombozi. Uhusiano wa jinsia ya kike na kiume umejaa mivutano, hughubika miundo yote ya maisha pakiwemo familia, elimu, kazi na siasa, utamaduni, starehe na anasa. Uhusiano huu huongoza jinsi wanajamii, wanavyoishi, wanachotenda, wanayemtendea na jinsi watakavyokuwa siku za usoni.

Utafiti wetu uliongozwa na nadharia ya Ufeministi. Hii ni kwa sababu tumechunguza ni vipi waandishi wa kiume wamefaulu kumsawiri kiongozi wa kike katika tamthilia za *Kilio cha Haki, Sudana, Posa za Bikisiwa* na *Pango.* Nadharia hii iliasisiwa kwa lengo la kuangalia na kujaribu kutatua matatizo yanayowakabili wanawake katika jamii inayotawaliwa na wanaume. Matatizo yenyewe yanasababishwa na tofauti za kijinsia. Kwa maoni ya waasisi wa nadharia hii, matatizo yanayomkabili mwanamke yamejengeka kwenye misingi ya jinsia yao. Hii ina maana kuwa mwanamke amewekwa katika hadhi au daraja fulani katika jamii.

Kulingana na Wamitila (2003), Ufeminsti ni nadharia inayopinga asasi zote za kijamii zinazochangia katika kudhulumiwa kwa mwanamke. Wafuasi wa nadharia hii wanashikilia kwamba, pana haja ya kuwa na usawa wa kijinsia licha ya kuwepo kwa tofauti za kimaumbile. Kwa hivyo, wote wanaelekea kukubaliana kuwa, wanawake wanafaa wajitokeze kupigania haki zao ili angaa pawe na usawa wa kijinsia.

Kulingana na Wafula na Njogu (2007), kuna njia mbili za kubainisha matapo tofauti ya nadharia ya ufeministi. Kuna uainishaji unaoangazia masuala ya wanawake kimaeneo na uanishaji unaozingatia mirengo ya kiitikadi.

Katika uainishaji wa kimaeneo kwa mujibu wa hawa wasomi wawili, ulifanywa kwa kuzingatia changamoto zinazowakabili wanawake katika maeneo mbalimbali. Uainishaji huu ulitokana na ufahamu kwamba, wanawake wanakabiliwa na matatizo na changamoto tofauti tofauti kutegemea maeneo wanakotoka. Waligawa sehemu zenyewe katika makundi manne: Ufaransa, Marekani, Uingereza na Afrika.

Kulingana na wahakiki hawa wa kifeministi wa kiafrika, wao walitilia mkazo matumizi ya lugha. Kwamba lugha ilitumiwa kwa kumpendelea mwanamume. Wanawake wengi duniani wakajua kuwa lugha na maandishi yaliyomtofautisha mwanamke na mwanaume. Wao walizingatia maandishi, namna mwanamke alivyojieleza na kukariri dhamira fulani katika maandishi yao.

Wanawake wa Uingereza nao walitilia mkazo suala la siasa na historia. Kwa maoni ya wanawake hawa wa Uingereza, wenzao wa Marekani walisisitiza zaidi masuala ya kihisia na sanaa na kusahau historia na siasa. Wanawake wa Afrika nao wakawa na mtazamo tofauti na wenzao wa Ulaya na wale wa Marekani. Kwao, suala la utamaduni ndilo liliwakabili. Suala hili lilikuwa linawanyima nafasi ya kujieleza kwa namna mbalimbali; kuwakosesha nafasi ya kujieleza, uwezo wa kuchagua kuwa mke au mzazi mwanajamii, tohara na ukeketaji pamoja na desturi zilizomdharau mwanamke asiyezaa. Kwetu tutazingatia mwelekeo wa Kiafrika kwani tunaangazia masuala yanayohusu wanawake wa bara la Afrika na hasa eneo la Afrika Mashariki.

Uainishaji wa pili kama wanavyoangazia Wafula na NJogu, ulifanywa na Adamson, Briskin na McPhail (1998). Wahakiki hawa walizingatia mirengo ya kiitikadi. Walibainisha mitazamo mitatu ya kifeministi. Nayo ni Ufeministi huru, ufeministi wa kiharakati na ufeministi wa kijamaa. Ufeministi huru hutetea usawa kati ya wanawake na wanaume katika ngazi zote za maisha. Mkondo huu hushikilia kwamba maadamu wanadamu wameumbwa kuwa viumbe sawa na wako huru kutekeleza majukumu na malengo yao.

Ufeministi wa kiharakati humchukulia mwanamume kama adui mkubwa zaidi wa mwanamke. Waitifaki wake wanaamini kuwa uwezo wa mwanamke wa kuzaa ndio ambao hutumiwa na mwanamume kumdhalilisha. Kwa maoni yao, suluhu ni kuwahimiza wanawake wasiolewe na wanaume. Badala yake wanawake wanahimiza kushirikiana wao kwa wao hata kimapenzi.

Ufeministi wa kijamaa hulenga kukosoa ujamaa wa kimapokeo ambao licha ya kudai kwamba msingi wa unyonyaji ni jamii ya kitabaka inayompa uwezo mwenye kumiliki njia kuu za kuzalisha mali, kutumia mali hiyo kadiri ya uwezo wake, huendeleza utabaka na unyonyaji katika misingi ya kijinsia. Mrengo huu unawahimiza wanaume kushiriki katika malezi ya watoto na kadhia nyingine ambazo kimapokeo zimechukuliwa kuwa kazi za mwanamke.

Nadharia ya ufeministi inajaribu kufichua matatizo yanayopata wanawake kama ya kitabaka la kiuchumi na pia kama wanawake. Nadharia hii imewekewa msingi na msukumo mkubwa pamoja na nia ya kupigania ukombozi wa mwanamke kutokana na pingu za kiutamaduni, kidini, kijamii, kisiasa na kiuchumi – pingu ambazo zimejengeka kwenye misimamo na itikadi ya kiume.

Asasi tatu zinazomdhalilisha na kumdunisha mwanamke ni dini, ndoa na utamaduni. Utamaduni humsawiri mwanamke kama tamathali hasi na duni. Wanawake Waafrika wamedhalilishwa kwa vitengo vya utamaduni kama dini, utamaduni na ndoa na hivyo kukosa uwezo wa kuchagua kuwa mwanajamii na kimya cha kulazimishwa na desturi na mila.

Katika nadharia ya kifeministi tutatumia mihimili ifuatayo:

i) Usanii wa kuzingatia vipengele vya fasihi

Nadharia hii hutumia fasihi kama jukwaa la kuelezea kwa uyakinifu hali aliyomo mwanamke ili kumsaidia mtu yeyote kuielewa hali hiyo. Vyombo mbalimbali vya kisanii kama lugha yenye kujaa upekee hutumiwa. Maigizo huigizwa jukwaani na hivyo kufanikisha kazi teule ya fasihi. Mandhari na maudhui lengwa huwasilishwa jukwaani wakati wa maigizo. Dhamira ya mwandishi huweza kusomwa kimaandishi na kimaigizo. Mhimili huu utatufaa katika uchambuzi wa mbinu mbalimbali za usanii zilizotumika katika tamthilia tutakazozitumia katika utafiti wetu huu.

ii) Usawa

Nadharia hii pia inanuia kusawazisha wanadamu kwa upande wa utamaduni na uana. Sehemu hizi mbili huleta mkanganyiko katika jamii yoyote ile ulimwenguni. Ili kuonyesha ukaribu na umoja wa pande hizi, wahusika wanaopigania usawa hutumiwa. Mienendo na maigizo yanayoleta usawa huigizwa jukwaani. Harakati za usawa nazo hudhihirika kutoka kwa maigizo. Mhimili huu utatuwezesha kuangazia mada ya usawa na harakati za kuleta usawa unavyoigizwa katika tamthilia teule.

iii) Uhusika

Mtazamo huu huhamasisha utungaji wa kazi za sawa zenye wahusika wa kike wanaoweza kuigwa. Wanawake ambao hawawategemei wanaume ili wajitambulishe. Matumizi ya wahusika wa kike ili kuleta dhana ya ufeministi hujenga mchezo vile tutakavyoona katika utafiti wetu wa baadaye. Mwandishi huweza kufaulu kwa kuongeza wahusika wa kiume wanaopingana na wahusika wa kike katika mchezo

wake. Mhimili huu utatufaa sana kuona jinsi wahusika wa kike wanavyohusishwa na uongozi wa jamii zao.

iv) Umoja wa Wanawake na ukombozi

Ni nadharia inayokuza na kuendeleza hisia za umoja wa wanawake kama kundi linalodhulumiwa. Wahusika hawa wa kike hushiriki pamoja ili kujikomboa. Harakati zao za ukombozi hukumbwa na changamoto nyingi sana. Mwishowe pana ushindi kwa wanawake. Nadharia hunuia kuzindua mwamko kwa upande wa mwanamke jinsi wanavyojiona na uhusiano wao na watu wengine. Mhimili huu umetudhihirishia wazi harakati zitakazotumika na wanawake na kilio chao cha ukombozi kifafanuliwe kamili.

Wollstonecraft (1792) ndiye anayetambuliwa kwa kuanzisha harakati za kumkomboa mwanamke kutokana na 'pingu' za kijamii zinazotokana na misingi ya ubabedume na mpangilio wa kiume katika jamii. Katika kazi zenyewe, *A Vindication of the Rights of Wollstonecraft(1792)*, mfeministi huyu aliupinga mfumo wa ubabedume. Kwake mfumo wenyewe uliwapotosha vijana kiasi cha kuwafanya watambue 'uwezo' wa kiume katika jamii na kujitambulisha kwao au kulazimishiwa kuitikia desturi wa jamii yenyewe.

Kama hatua ya kupiga vita mpangilio kama huo, Wollstonecraft alipendekeza elimu ya kibinafsi kwa nia ya kumtenganisha mtoto na ubabe dume au wanafunzi wachanganywe madarasani na kupewa fursa ya kufurahia ujana wao na wakati huo huo wapewe shughuli za kutekeleza kwa ushirikiano. Anapinga vikali mazoea yaliyopelekea kutwezwa kwa mwanamke. Anafichua hali ambapo mwanamke hutazamwa kama mwanamke ndipo baadaye aonekane kama binadamu. Anasema mtazamo huu ndio unaomdunisha na kumpa mwanamke hadhi ya chini baada ya mwanamume.

Mapendekezo ya Mary Wollstonecraft ni kuundwa kwa jamii mpya yenye usawa kati ya mwanamke na mwanamume. Mawazo haya yanaungwa mkono na Simone de Beauvoir katika kazi yake ya *The Second Sex* (1949). Beauvoir anazishambulia asasi za kitamaduni zilizojengwa kwa imani ya uwezo mkubwa alio nao mwanamume kiasi sha kumchukulia mwanamke kama kiumbe duni. Alikuwa na mawazo sawa na ya Wollstonecraft kwamba, jamii inaendeleza taswira fulani chukulizi kumhusu mwanamke. Inamwangalia mwanamke kama kitu hasi ilhali mwanamume ni binadamu kielelezo.

Kwa mujibu wa Wamitila (2002), Beauvoir anasisitiza kuwa utamaduni anamokulia mwanamke huchangia katika kumdidimiza katika hali ya unyonge. Utamaduni huo hivyo basi, unamfanya na hata kumlazimisha mwanamke kukubali kuwa yeye ni kiumbe duni.Miller (1969) naye katika kazi yake ya *Sexual Politics,* anashiriki vilivyo katika kutetea haki za mwanamke kwa kupinga namna ambayo waandishi wanaume wanavyowasawiri wahusika hao wa kike. Anarejelea kazi za waandishi Henry Miller, Norman Mailer na Jean Genet.

Kulingana na Millet (1969), malezi ndiyo chanzo cha hali dhalilishi na duni ya mwanamke katika jamii. Kwa kuwa mtoto wa kiume analelewa kwa namna ya kumdhihirishia sifa za uume: kujikidhia 'haja' za kiume. Malezi hayo yanamwandaa na kumtanbulishia kuwa uume unahusisha matumizi ya nguvu, utundu na umilikaji wa kila kitu. Anaendelea kusema kwamba, mwanamume anamtawala mwanamke (1969). Torril Moi (1985) katika *Sexual Textual Politics* anaelezea uwili unaojitokeza katika jamii. Anasema kuwa kila jinsia hunasibishwa na sifa fulani. Mwanamume hunasibishwa na jua kisitiari, na mwanamke hunasibishwa na mwezi.

Malengo ya ufeministi yameleta ukinzani wa maisha halisi ya mwanamke wa kiafrika. Hali hii imeleta mabadiliko katika maisha ya wanawake wa kiafrika kutaka haki ya elimu, kumiliki mali, kurithi mali, kutaka nafasi za uongozi na kuwa na maamuzi ya kifamilia .

Kazi hizi zitakuwa dira katika kazi yetu ya kiutafiti. Mawazo yao yatatuelekeza kutathmini namna ambavyo waandishi wamemsawiri kiongozi wa kike na vilevile changamoto zinazomkabili katika jamii inayotawaliwa na mfumo wa kiume.

### 1:10 Mapitio ya Maandishi

Udurusu wetu wa yaliyoandikwa umetutia moyo na wakati uo huo kutagusa kwani kuna kazi nyingi zilizotafitiwa kuhusu wanawake. Si riwaya, si tamthilia, si ushairi, zote zimetafitiwa. Hata hivyo, tutaangazia machache yatakayokuwa na umuhimu zaidi kwetu.

Msomi Ndungo (1985), ametafitia maendeleo ya mwanamke na mabadiliko ya kihistoria katika fasihi ya Kiswahili. Ameangazia aina mbalimbali za ukandamizwaji zilizomkabili mwanamke katika mifumo tofauti ya kiuchumi, kijamii na hata kisiasa. Anasema kuwa mwanamke amefanywa kuwa chombo cha mwanamume cha kujifurahisha. Na kwamba mwanamke anaishi kulingana na matakwa ya

mwanamume. Anaeleza namna ambavyo dini inatumiwa kumkandamiza na kumdhalilisha mwanamke, akiangazia *Utenzi wa Mwanakupona* na riwaya ya *Kaburi Bila Msalaba.* Amesawiri nafasi muhimu na mchango aliotoa mwanamke katika harakati za kupigania ukombozi wa jamii licha ya changamoto nyingi zilizomkabili. Tofauti na kazi za Ndungo, aliyeshughulikia tanzu mbili (ushairi na riwaya), tutafanya utafiti kwa kuzamia nafasi na athari ya kiongozi wa kike katika tamthilia nne teule *Kilio cha Haki, Sudana, Pango na Posa za Bikisiwa* za lugha ya Kiswahili.

Lugano (1989), katika utafiti wake ameshughulikia usawiri wa mwanamke kisiasa, kiuchumi na kijamii katika riwaya tatu za Euphrase Kezilahabi. Alionyesha jinsi mwanamke alivyosawiriwa kama mtegemezi wa mwanamume, chombo chake na chanzo cha maovu yote. Mtafiti huyu alitumia nadharia ya ufeministi wa kiitikadi. Utafiti wake umesaidia uelewa wa usawiri wa mhusika wa kike kwa jumla. Hata hivyo utafiti huu utakuwa tofauti na wetu maana tutaangazia kitengo cha siasa katika tamthilia teule na bali si riwaya.

Kazi nyingine imetufaa ni tasnifu ya Nyamberi (1997) aliyeangazia ‘‘Mwamko wa Mwanamke katika Tamthilia za Penina Muhando’’. Mhakiki huyu anaangazia namna mwanamke ameanza kutambua haja ya kupigania usawa wa kijinsia katika jamii yenye mfumo wa ubabe dume. Sawa na jinsi anavyoshughulikia kazi yake, kazi yetu itashughulikia kiongozi wa kike na pia mchango wa waandishi katika kufichua changamoto katika ukombozi wenyewe. Tofauti ni kuwa Penina ni mwandishi wa kike ilhali tunahakiki kazi za waandishi wa jinsia ya kiume *Mazrui, Njogu, Wamitila, Mohamed na King’ei*. Pia, Nyamberi alitumia nadharia ya Ufeministi Asilia lakini tutatumia Ufeministi wa Kiafrika. Lengo ni kutathmini changamoto zinazowakabili viongozi wa kike katika jamii za Kiafrika.

Mtafiti Kruger (1998), ametafiti kuhusu mhusika wa kike na jinsi anavyosawiriwa na waandishi wa Kiafrika walioandika riwaya na hadithi fupi. Anasema kuwa waandishi hawa hawatumii wahusika wanawake kama wahusika wakuu. Mara nyingi waandishi wamewachora wanawake kama wahusika wajenzi na hivyo wanawabagua. Mtafiti huyu ameshughulikia riwaya na hadithi fupi.

Nadharia iliyomwongoza ni ya mwingilianomatini. Utafiti huu utasaidia kutupa mwanga kuhusu mhusika wa kike. Tofauti na utafiti wetu ni kuwa tutashughulikia tanzu ya tamthilia ambayo imemsawiri mwanamke kama mhusika mkuu.

Mwihaki (1998), ameshughulikia usawiri wa umbo la mwanamke katika fasihi simulizi ya kiafrika, methali za Gikuyu na Swahili. Alishughulikia umbo kwa kuchanganua fasihi simulizi hasa methali. Amelinganisha na kuchanganua jinsi kipera cha methali kinavyomchora mhusika wa kike katika jamii hizo mbili. Mwanamke amechorwa kuwa na umbo teule linalodhihirika wazi katika methali ya jamii ya Gikuyu. Nadharia zilizomwongoza ni za kimaumbo na uchanganuzi linganishi. Utafiti huu utasaidia kuelewa fasihi simulizi ilivyomsawiri mhusika wa kike katika jamii husika za kiafrika. Tofauti na utafiti wetu ni kuwa nadharia tutakayoitumia ni ya Ufeministi wa Kiafrika na tanzu ya fasihi andishi ya tamthilia. Msomi huyu ametafiti kitengo cha fasihi simulizi.

Thiong'o na wenzake (2001), katika utafiti wao, wametambua sehemu za baadhi ya maandishi ya fasihi zilizo na mtazamo chanya kuhusu uana na hususan zinazungumzia mambo ya wanawake. Sura ya ujumla wanayompa msomaji ni kuwa, fasihi iliyoandikwa na wanaume ina mtazamo hasi na isiyowakomboa wanawake Waafrika. Utafiti huu umetupa mwanga zaidi na taswira chanya watafiti hawa wanayompa mwanamke. Tofauti na utafiti wetu ni kuwa tutalenga siasa za mhusika wa kike na hasa mtazamo chanya na hasi wanaompa mwanamke waandishi wa kiume katika fasihi ya Lugha ya Kiswahili.

Naye Burhani (2003), katika utafiti wake ameshughulikia usawiri wa wahusika wanawake na lengo lake kuu ni kupiga vita mfumo wa kuumeni. Utafiti wake ulitumia nadharia ya Kimarxi. Utafiti huu utatusaidia kupata data kuhusu usawiri wa mhusika wa kike kwa ujumla tu. Tofauti ni kuwa ameshughulikia mhusika nasi tumelenga mhusika wa kike aliye kiongozi na aliyebobea kisiasa. Nadharia yetu pia ni ya Ufeministi wa kiafrika bali zi ya Kimaksi.

Kwa utafiti mwingine Maingi (2005), naye katika utafiti wake wa kuchunguza na kutathmini ''Upembezwaji wa Mwanamke katika Udokezi wa Nafasi ya Mwanamke katika *Utenzi wa Fatumah''*. Anaonyesha namna ambavyo mwanamke anapembezwa kwa kutoshirikishwa katika maamuzi muhimu ya kijamii ilhali anasifiwa kwa mchango wake wa kuwalea watoto nyumbani. Kazi hii imekuwa na umuhimu kwetu kwani inamulika asasi zinazomtweza mwanamke. Hata hivyo, tofauti ni kuwa mhakiki huyu alichunguza tanzu ya ushairi ilhali sisi tumeangazia tanzu ya tamthilia.

Katola (2006), katika utafiti wake ameshughulikia udhalimu dhidi ya wahusika wa kike katika tamthilia za Kiswahili. Alitathmini tamthilia za *Hatia*, *Buriani*, *Mama Ee,* na *Kitumbua Kimeingia Mchanga.* Madhumuni ya utafiti huo yalikuwa takilenga suala la udhalimu kama linavyojitokeza katika kazi za waandishi wa jinsia zote. Tamthilia nne za Kiswahili zilichanganuliwa ili kuafiki lengo la utafiti. Nadharia ya Ufeministi iliongoza utafiti huu. Matokeo yalielezwa kwa kina, nayo dhamira kuu kuwa ni kupata ukombozi kwa mhusika wa kike. Mhakiki huyu anaangazia udhalimu dhidi ya mwanamke katika jamii ilhali utafiti wetu utachunguza usawiri wa kiongozi wa kike kwa kurejelea kazi za waandishi wanaume *Mazrui, Njogu, Mohamed, King'ei na Wamitila.* Tuliegemea mwanamke aliye na mwamko mpya wa kuiongoza jamii yake. Sawa na utafiti wetu, mhakiki huyu ametumia nadharia ya Ufeministi ya Kiafrika.

Utafiti wa Mwanakombo (2008), katika utafiti wake naye alizungumzia mhusika wa kike. Nadharia aliyoshughulikia ni ufeministi wa kiafrika katika fasihi ya Kiswahili. Eneo lake lilikuwa fasihi ya Kiswahili ambapo aliupa utafiti wake mtazamo wa wanawake waislamu. Alionyesha jinsi wamesawiriwa kama wahusika wanaokiuka mihimili ya kiafrika na hivyo kuenda kinyume na nadharia ya ufeministi. Utafiti huu utakuwa tofauti kwa sababu haujikiti katika jamii moja bali jamii nzima. Utafiti huu utatupa mwanga kutoka kwa jamii ya kiislamu. Utafiti huu wake ni tofauti maana ni wa nyanjani nasi huu wetu ni wa maktabani.

Katika utafiti wa Mulila (2009), anatathmini usawiri wa mwanamke katika tamthilia za *Zilizala* na *Chamchela.* Alieleza namna ambavyo waandishi wa tamthilia hizi (Njogu Kimani na Tomothy Arege) wamechangia katika ukombozi wa mwanamke kwa kumjenga mwanamke kihadhi. Kazi hii itatufaa sana kwani tutachunguza mchango wa waandishi wanaume katika kumsawiri kiongozi wa kike. Tofauti ni kuwa tutaangazia waandishi wa kiume watano *Mazrui, Njogu, Mohamed, King'ei na Wamitila* ilhali alichunguza wawili, Arege na Njogu.

Msomi Swaleh (2011), katika utafiti wake, amehakiki mtazamo wa usawiri wa jinsia katika riwaya nne za Kiswahili ambazo ni; *Rosa Mistika* (Kezilahabi; 1971), *Mwisho wa Kosa* (Burhani; 1987), *Nguvu ya Sala* (Wamitila; 1999) ya Wamitila na Tumaini (Momanyi; 2006). Riwaya ya Tumaini ilitathmini jinsi kijana Tumaini alipuuza utamaduni na kujikomboa kutoka utamaduni wa kupashwa tohara na kujiunga na

masomo. Kazi hii iliwafaa katika utafiti wao kwa vile maudhui ya kumsawiri mhusika mkuu yalijengwa kupitia mbinu za lugha ambazo ndiyo mada yao. Tofauti na utafiti wetu ni kuwa tutatumia tamthilia.

Kulingana na Mavisi (2011), katika utafiti wake ameshughulikia usawiri wa wahusika wa kike katika kazi za Zainabu Burhani. Mtafiti huyu amehakiki riwaya tatu zake mwandishi huyu. Kazi zilizochanganuliwa ni *Mali ya Maskini* (1981), *Mwisho wa Kosa* (1987) na *Kipimo chaMizani* (2004). Nadharia ya mtazamo-kike iliongoza utafiti huu. Itikadi kama pingamizi ya kumkandamiza mwanamke inapingwa katika matini teule na harakati za ukombozi zimejadiliwa. Tofauti na utafiti wetu ni kuwa tutatumia tamthilia. Utafiti utatusaidia kuchanganua jinsi mhusika wa kike alivyosawiriwa riwayani.

Mirikau (2011), katika utafiti wake ameangazia taswira ya mwanamke katika tamthilia za Kiswahili. Utafiti ulichanganua sura ya mhusika wa kike katika tamthilia za K. Wamitila ambazo ni *Wingu la Kupita* (1999), *Pango* (2003) na *Seserumbe* (2009). Nadharia ya Ufeministi wa kiafrika ilitumika. Muhtasari wa kila tamthilia ulielezwa kisura. Tofauti na utafiti wetu ni kuwa tutamsawiri mwanamke kiongozi na athari yake katika jamii anamoishi. Utafiti huu utasaidia kwa kuwa tutapata sura hasi na chanya aliyopewa mhusika wa kike na kuangazia changamoto zinazowakabili wanawake katika harakati zao za kujikomboa.

Katwina (2012), katika utafiti wake amehakiki swala la mwanamke kama linavyojitokeza katika tamthilia za Kiswahili zilizoandikwa na waandishi wa kike. Uchunguzi ulishughulikia taswira katika kila mojawapo ya kazi teule. Suala kuu ni ukombozi wa mhusika wa kike. Uchunguzi wake wa kina ulikuwa ni kujaribu kuangalia iwapo waandishi ni watetezi halisi wa maslahi ya wanawake. Kazi za fasihi za waandishi mashuhuri wa kike zilichambuliwa nazo ni za *Sheila Ryanga, Ari Kartini Mwachofi, Penina Muhando na Angeline Chogo*. Tofauti na utafiti wetu ni kuwa waandishi wa tamthilia teule ni wanaume wanaomsawiri mwanamke kisiasa.

Muindi (2012), katika utafiti wake ameshughulikia suala la ukahaba katika riwaya nne za Said Ahmed Mohammed ambazo ni Mwis*ho wa Kosa, Utengano, Arusi ya Buldoza na Dunia Mti Mkavu.* Nadharia za ukahaba zilitumika. Tofauti na utafiti wetu ni kuwa tutatumia nadharia ya ufeministi wa kijamaa. Utafiti huu utatupa ufahamu jinsi mhusika wa kike alivyosawiriwa riwayani.

Mwenderani (2012), katika utafiti wake ameshughulikia taswira ya mwanamke katika tamthilia mbili za Kiswahili. Ameangalia picha ambayo mwanamke amepewa na jamii katika tamthilia za *Kilio cha Haki* (Mazrui; 1981) na *Pango* (Wamitila; 2003). Mtafiti huyu alishughulikia sura chanya na hasi ambazo amepewa mhusika wa kike. Tofauti na utafiti wetu ni kuwa tutachunguza kuhusu kiongozi wa kike na utafiti huu utatusaidia kupata sura mbili alizopewa mhusika wa kike.

Mtafiti Onyoni (2012), anachunguza usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia za *Mama Ee*(Mwachofi; 1987)na *Natala*(Mberia; 1997).Mhakiki mwenyewe anachunguza namna ambavyo mwanamke amesawiriwa katika kazi zenyewe. Tofauti na kazi hii, tutapiga hatua zaidi kwa kuangazia changamoto zinazosababisha hali yenyewe kama inavyojitokeza katika tamthilia ambazo mhusika wa kike ni kiongozi.

Naye Kipyegon (2013), anahakiki nafasi na utambulisho wa mwanamke katika *Natala* (Mberia; 1997), na *Kifo Kisimani* (Mberia; 2001).Amechunguza nafasi dhalilishi na chanya ya mwanamke. Alitumia Nadharia ya Ufeministi wa Kijamaa. Tofauti na utafiti wetu ni kuwa tutatumia Ufeministi wa Kiafrika. Ametumia tamthilia mbili za mwandishi mmoja na sisi tutatumia tamthilia nne za waandishi tofauti. Pia tutamwangalia mwanamke kama kiongozi na sio mwanajamii wa hadhi ya chini.

Kairi (2014), amehakiki tamthilia ya *Sudana* kwa kuangalia ukoloni mamboleo na utandawazi. Ameongozwa na nadharia ya Baada ya Ukoloni na kuchanganua masuala haya ya uzito mno hasa katika karne hii ya ishirini na moja. Tofauti nasi tamthilia hii tumemchora mwanamke kama kiongozi na kutumia nadharia ya Ufeministi.

King'ora (2014), amehakiki suala la utendaji katika tamthilia ya *Sudana* na *Kimya Kimya*. Nadharia iliyomsadia kutekeleza malengo yake ni ya Utendaji. Tofauti na utafiti wetu, mhusika Sudana tutamchora kama kiongozi na nadharia itakayotuongoza ni ya Ufeministi.

Msomi Mwikali (2014), ametafiti kuhusu uchanganuzi wa uhusiano wa kijinsia katika kuvichunguza vipengele vya tamthilia za *Kilio cha Haki* na *Sudana*. Nadharia iliyomwongoza ni ya kimaumbo. Tofauti na utafiti wetu ni kuwa nadharia yetu itatuelekeza kwa sifa za mhusika huyu kama mke nayo ni Ufeministi wa kiafrika.

### 1.11 Mbinu za Utafiti

#### 1.11.0 Utangulizi

Sehemu hii inafafanua muundo wa utafiti, eneo la utafiti, idadi lengwa, usampulishaji, ukusanyaji, uchanganuzi na uwasilishaji data.

#### 1.11.1 Muundo wa utafiti

Utafiti huu umetumia muundo elezi. Kerlinger (1969), anasema kuwa muundo elezi husaidia kuainisha, kuchanganua, kulinganisha na kufasiri data, jambo ambalo utafiti huu unanuia kufanya.

#### 1.11.2 Eneo la utafiti

Eneo la utafiti ni kuhakiki matini. Maktaba mbalimbali nchini Kenya zilikuwa za umuhimu kwetu. Maktaba za vyuo vikuu vya Kenyatta, Nairobi, Maseno na Moi zilitufaa sana. Katika maktaba hizi matini mbalimbali ilisomwa, ikaduruswa, ikachanganuliwa na kutathminiwa kuhusu suala la utafiti. Njia ya kipekuzi ilijumuishwa ili kupata data tosha ya mada yetu ya utafiti.

#### 1.11.3 Idadi Lengwa

Utafiti huu ulilenga tamthilia nne za Kiswahili ambazo ni; tamthilia za *Kilio cha Haki* (Mazrui; 1981), *Sudana* (Mazrui na Njogu; 2006), *Posa za Bikisiwa* (Mohamed na King'ei; 2008) na *Pango* (Wamitila; 2003).

#### 1.11.4 Uteuzi wa Sampuli

Utafiti huu uliteua sampuli kimaksudi, mahsusi sampuli ilikuwa tamthilia nne *Kilio cha Haki, Sudana, Pango na Posa zaBikisiwa*, zilizolenga fasihi ya Kiswahili ili kusaidia kutimiza madhumuni na malengo ya utafiti wetu. Mtaalamu Mwanje (2001), katika utafiti wake anaeleza ya kuwa usampulishaji dhamirifu huangalia na kuchuja data ili kupata sampuli yenye sifa zinazohitajika. Wahusika hawa wa kike wana mchango upi katika kuongezea maarifa na kukua kwa fasihi ya karne hii ya ishirini na moja?

#### 1.11.5 Ukusanyaji data

Data ilikusanywa kutoka tamthilia teule zenye wahusika wanawake viongozi. Data ilipangwa ili ichambuliwe kwa urahisi. Uchunguzi huu wa kina ulituwezesha kuhakiki kwa makini vipengele vya kisanaa vinavyojitokeza katika kazi husika ya fasihi na jinsi vinavyosaidia kumsawiri mhusika wa kike. Uchanganuzi ulifanywa kuhakikisha kuwa data sahihi na kamili ndiyo imetumika.

### 1.11.6 Uchanganuzi na uwasilishaji data

Truex (1996), anathibithisha kuwa njia ya uchanganuzi matini ni muhimu kwa utafiti wowote ule. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa, ikafasiriwe na kuwekwa kwenye mpangilio mwafaka ili kuhusisha malengo na nadharia zetu za utafiti. Uhusiano wa mihimili ya nadharia na matini teule ulizingatiwa ili kuonyesha muoano ulioko baina ya matokeo na umuhimu wa utafiti. Hatima ya utafiti wetu ulikuwa kueleza matokeo yetu kwa matumizi ya mada ndogo ndogo na aya mbalimbali.

# SURA YA PILI

# MUHTASARI WA TAMTHILIA TEULE

## 2.1 Utangulizi

Sura hii tutajadiliana dhana ya tamthilia, kisha tueleze historia fupi ya tamthilia teule, muhtasari wa kila tamthilia teule na dhana ya uhusika na uteuzi wa wahusika wa jinsia ya kike walio viongozi. Historia ya tamthilia ni changa na pia uhakiki wake haujakomaa. Tamthilia nyingi zimeandikwa ili kuhubiri maadili ya jamii na kusuta maovu ya kiuchumi na kisiasa yanayotendwa dhidi ya wakazi wa bara la Afrika.

## 2.2 Dhana ya Tamthilia

Tamthilia ni utungo wa kisanaa ambao huweka wazo fulani katika matendo na mazungumzo. Tamthilia huwa na sehemu tatu muhimu: mwanzo, katikati na mwisho. Tamthilia nzuri inajitosheleza kimuundo. Sehemu kama wahusika, maudhui na ploti zinatazamiwa kuingiliana, kujengana na kukamilishana. Tamthilia pia huwa na lengo mahsusi. Vitendo vinapaswa kuchangia katika ufanisi wa dhamira ya mtunzi. Watunzi wa tamthilia wanawajibika kutumia mbinu za kisanii zinazowashajiisha wasomaji kuendelea kusoma na kutazamia matokeo ya matendo yanayoigwa. Wasanii bora ni wale wanaoandika tamthilia zinazozungumzia kadhia zinazoweza kutimia katika maisha ya binadamu.

## 2.3 Historia Fupi ya Tamthilia Teule

### 2.3.1 Tamthilia ya *Kilio cha Haki*

Hii ni tamthilia ya kwanza katika lugha ya Kiswahili iliyochapishwa na Profesa Alamin Mazrui mwaka wa 1981. Tamthilia hii imeainisha na kutumia kunga za fasihi zinazooana na itikadi za kijamaa. Tamthilia hiiinaigiza mapambano baina ya wafanyakazi na udhalimu wa makaburu walioivamia nchi yao. Katika mapambano hayo wanaongozwa na mwanamke jasiri, Lanina.Utafiti wetu uliongozwa na mkondo wakihistoria ambapo, mwandishi ameshughulikia nafasi ya mwanamke katika jamii iliyozongwa na mikinzano ya kiuchumi na kitamaduni. Mhusika mkuu wa kike anayeitwa Lanina, amegandamizwa maradufu: kama mfanyakazi anayeuza jasho lake na pili kama mwanamke anayedunishwa na utamaduni. Lanina anaupinga utamaduni huu kwa kusema:

Utamaduni! Utamaduni! Utamaduni ni kitu gani

Mwengo? Kwa nini sisi tuwe watumwa wa utamaduni wetu! (*Anamgeukia tena Mwengo*) Mwengo ... si sisi tulioufinyanga utamaduni? Si sisi tulioupa uhai utamaduni... uhai wa kutuongoa? Basi kwa nini tuuache utamaduni ututie pingu na fahamu zetu kututawalia, utupige pande na tabia yetu ya kuzingatia? Kwa nini Mwengo! ... Kwa nini Mwengo! ... tuendelee kuufuata utamaduni hata uwapo makosani yakini? (uk. 32)

Lanina anasema kwamba utamaduni unategemea itikadi, na iwapo itikadi itabadilika kutegemea na mabadiliko ya mahusiano ya kiuchumi, basi utamaduni unaoitegemea itikadi hiyo hauna budi kubadilika.

Itikadi ya kijamaa imetumiwa katika tamthilia hii na mwandishi kwa nia ya kuonyesha hali halisi inayopatikana katika mgomo wa wafanyakazi. Mwandishi anaibainisha mikakati inayoweza kutumiwa kuwazindua wafanyakazi na vilevile kuwachochea ili wapate ari ya kutetea haki zao.

### 2.3.2 Tamthilia ya *Pango*

Tamthilia hii imeandikwa na Profesa Wamitila, K.W. mwaka wa 2003. Ni tamthilia inayotufunulia na kujadili utata wa kisiasa, uchumi, uongozi na migongano ya wimbi la ukale na usasa. Tamthilia hii ni mchango mwingine mwafaka katika medani ya fasihi hasa uga wa drama. Tamthilia hii imetumia jazanda ili kusawiri mawazo kwa kina kirefu zaidi. Masuala ya itikadi yanalengwa ili kuonyesha tofauti kati ya ukale na usasa.

Mwandishi ametumia mhusika mkuu wa kike aitwaye Katango. Katango ameiashiria Afrika. Ni bara inayoathirika na siasa mbaya, uongozi dhalimu na unyanyasaji wa kiuchumi kutoka mataifa ya mashariki na magharibi mwa dunia. Uongozi unakuwa ndilo jambo kuu na harakati za ukombozi. Watu wanaishi katika jamii hii kwa haki na kiutamaduni. Mhusika mmoja katika tamthilia anatujulisha kuwa Afrika bado inatilia utamaduni maanani sana, tunamnukuu hapa akisema:

**Mbabekazi:** Haiwezekani! *Culture, culture* bwana, unafikiri watu watakubali mwanamke awaongoze wewe? *We are not yet there*!(uk.25)

Katango, ni mwanamke aliyesoma, na akaelewa mambo kama siasa.  Hata hivyo vijana kama Mbabwkazi wana uelewa kuwa bado asasi za kijamii zitampendelea kiongozi wa kiume Ngwese.

### 2.3.3 Tamthilia ya *Sudana*

Tamthilia hii imeandikwa nao Profesa Alamin Mazrui na Kimani Profesa Njogu mwaka wa 2006.  Katika jalada, bara ya Afrika imechorwa kama iliyosafarini kwa meli.  Wasafiri wamo ndani ya meli yao inayovuja baharini.  Baharini wanakutana na wasafiri wengine lakini sio wangwana.  Sudana akiwandiye kiongozi wa kike yu safarini na wanawe.  Matatizo ya chombo baharini yanapelekea Sudana, msafiri mkembe, pamoja na jamaa yake kujikuta dhidi ya washirika wawili – Amerigo na Muzungu, watu ambao matendo, tabia na hatua zao zinatawaliwa na imani, mielekeo na taasubi kali.

Sudana anatatizika baina ya kulinda hadhi yake, kwa upande mmoja na kuiuza hadhi hiyo, kwa upande mwingine, ili kuwanusuru wanawe wasiangamizwe katika madhila na mzigo wanaotwikwa na Amerigo na mshirika wake.  Maingiliano changamano baina ya pande hizi mbili ndiyo yanayosuka hadithi ya tamthilia hii.  Athari ya nchi za mashariki na magharibi ulimwenguni kwa Afrika imedhihirishwa wazi.  Nchi hizi zinanyofoa nchi za Afrika kiuchumi na kitamaduni.

### 2.3.4 Tamthilia ya *Posa za Bikisiwa*

Tamthilia hii imeandikwa na Profesa Said A. Mohamed na Profesa Kitula King'ei mwaka wa 2008.  Waandishi hawa ni watukuka na wamebobea katika lugha na fasihi ya Kiswahili.  Waandishi wamemtumia mwanamke kama kiongozi na kumchora kama aliyebaleghe.  Wanaume wengi wamejaribu kumposa kwa kutumia nguvu za misuli, vitisho na hata pesa.  Waandishi wametumia mhusika huyu kajazanda kudhihirisha asili, vitendo na mielekeo ya mabara yenye kujinaki "bora mimi" dhidi ya bara la Afrika, hasa katika ulimwengu wa sasa wa makuadi wa utandawazi na soko huria.

## 2.4 Dhana ya Wahusika

Wahusika ni viumbe wanaopatikana katika kazi ya kifasihi.  Viumbe hawa huwa sehemu ya kazi nzima. Katika fasihi, matendo ya viumbe hufanana na yale ya binadamu.  'Binadamu' hawa wana sifa za kimaadili, kitabia, kiitikadi na kifalsafa. Wataalamu kama Mbatiah (2001), Mutiso (2005) na Wamitila (2003) wanadai kuwa

wahusika ni watu, vitu, wanyama, ndege, wadudu, miti, mashetani na kadhalika wanaotumiwa na watunzi katika utendaji na upitishaji wa ujumbe. Kutokana na matendo na mazungumzo yao wanatudokezea kuhusu ujumbe wa kazi inayohusika.

Kulingana na maelezo ya wataalamu hawa, ni dhahiri kuwa kila mhusika akiwa ameshikilia jukumu lolote lile, ana umuhimu mkubwa sana katika kazi ya sanaa. Yeye hupenyezwa katika nafasi yake maalum ili kutimiza malengo maalum ya msanii. Nafasi yake huwa pana au finyu kwa mujibu wa mtunzi ili kuwasilisha dhana fulani.

Wahusika wengine hushirikishwa kwa kupewa nafasi ya kutenda, kusema, kujiwasilisha na kujitambulisha kwa hadhira. Mhusika husawiriwa kwa namna inayokaribiana sana na binadamu katika ulimwengu wa kihalisia. Hata hivyo, uandishi wa tungo za fasihi unaweza kuvuka mipaka ya uhalisia. Kuvuka huko kunajitokeza katika wahusika wake na usawiri wao. Hivyo basi uandishi unahusu uteuzi na uteuzi huo unajitokeza kwenye usawiri wa wahusika pia. Tulipata ya kuwa wahusika wamejengwa kwa kuzingatia utendaji.

Kama tulivyoona hapo juu, wahusika ni vivuli wanaochukua nafasi za wahusika halisi. Msanii anapowasawiri wahusika wa kifasihi huwa na dhamira na malengo ya kudhibiti. Msingi wa hisia, hali ya kimaadili, mazungumzo na matendo ya wahusika ndiyo kiini cha motisha au uhamasishaji wa wahusika.

Umuhimu wa wahusika ndicho kipimo ili kuonyesha iwapo wametekeleza majukumu yao ya kisanaa vilivyo na kujitokeza bayana. Wahusika wamesawiriwa kwa kuchorewa picha wa kitu au mtu inayoiga maisha kwa kuzingatia misingi ya maisha ya jamii inayohusika.

Utafiti wetu utaangalia kwa muhtasari mitazamo ambayo ilitupa data jinsi wahusika wa kike viongozi walivyoteuliwa. Mtazamo wa kwanza, kwa mujibu wa Forster (1972), wahusika wako katika makundi mawili makuu, wahusika bapa na wahusika duara. Wahusika bapa hutumiwa na mwandishi ili kusimamia wazo au dhana fulani. Wahusika bapa hawabadiliki tangu mwanzo hadi mwisho. Utafiti wetu ulichunguza wahusika bapa vielelezo.

Wahusika bapa vielelezo hawabadiliki na hupewa majina ambayo yanaafikiana na matendo na tabia zao. Majina ya wahusika hawa huwa kama kielekezi na kifupisho

cha wasifu wao.  Sifa hii huitwa majazi.  Mbinu ya majazi imetumiwa tangu zamani kwakuwa majina katika jamii nyingi huwa na maana.  Uchunguzi wa majina ya wahusika lazima uhisishwa na msuko, dhamira na itikadi au motifu katika kazi husika.  Utafiti wetu uligundua kuwa mhusika Lanina wa *Kilio cha Haki*, Sudana wa *Sudana*, Bikisiwa wa *Posa zaBikisiwa* na Katango wa *Pango* ni wahusika bapa vielelezo.

Mtazamo wa pili, ni ule wa kulichunguza suala la uhusika kwa kuangalia nafasi ya mhusika kuhusiana na mgogoro na mkondo wa tamthilia nzima.  Kazi ya fasihi husika huwa na mhusika anayeitwaa nafasi kuu.  Huyu ni shujaa au nguli.  Mhusika huyu huwa na kinyume chake, yule anayeupinga mtazamo wake.  Huyu huwa hasidi au muwi.  Utendaji na maelekezi yatatuongoza ili kuchanganua wahusika hawa wateule.

## 2.5 Uteuzi wa Wahusika

### 2.5.1  Uteuzi wa Lanina kama Kiongozi wa Kike.

Msokile (1993:42), anaeleza ya kuwa majazi ni tamathali ambayo huwakilisha kitu kizima au sehemu ya kitu.  Mara nyingine majazi hutumika kwa dhana inayokaribiana au dhana ambayo ni sawa na ileinayozungumziwa.  Mhusika Lanina ameteuliwa kimajazi.

Lanina ni kiongozi wa wafanyakazi. Ana moyo mkuu na ni mwenye imani kwa wafanyakazi wenzake.  Anapenda hakina kuchukia maonevu, unyonyaji na ukoloni. Ni kwa sababu hiyo, anajitolea mhanga kupigania haki za wafanyakazi na ujenzi wa jamii mpya.  Ana moyo safi kama msahafu kama inavyodhihirishwa na uaminifu wake kwa itikadi inayomwongoza kwa mumewe na wafanyakazi wenzake. Anauchukia ufisadi na ubinafsi kwa hivyo anakataa kuhongwa kwa mshahara mkubwa na cheo.  Lanina anajinyima maisha mazuri kwa manufaa ya mapambano anayoamini yatawaletea walio wengi nafuu.

Lanina amejikomboa kimawazo, anadhihirisha udhalimu wa jumuiya yake unaowapata wafanyakazi kwa upande mmoja na wanawake kwa upande mwingine. Anafaulu kuwazindua wafanyakazi wenzake wapambane na udhalimu na watetee haki zao.  Mapambano haya yanaleta mwamko wa kisiasa ambao ndio mwanzo wa matayarisho ya vita vilivyoikomboa nchi nzima kutokana na ukoloni.  Katika *Kilio cha Haki* asasi ya ndoa imejengwa kwa misingi ya taasubi ya kiume.

### 2.5.2 Uteuzi wa Katango kama Kiongozi wa Kike

Katango ni mwanamke kijana aliye na ujuzi wa ualimu. Ndiye kiongozi wa kike katika tamthilia ya *Pango* (Wamitila:2003). Amezinduka kutoka mikatale ya utamaduni na kujiopoa. Jitihada zake za kuikomboa jamii yake zinamtia matatani na wazee wa kijiji chake na hata baba mzazi. Hata hivyo hafi moyo bali anajikakamua na kuona pana ufanisi mwishowe. Asasi kuu inayoongoza jamii ya pango ni utamaduni. Kila jamii ina utamaduni unaowaelekeza na kuwaongoza wanajamii na maisha yao. Asasi za kitamaduni zinaonekana kuwa na mshiko mkubwa kwa wanajamii wake.

Kwa mujibu wa Pilcher na Imelda (2004) wanasema kuwa kuna ithibati tosha kuonyesha ugavi wa majukumu kulingana na jinsia ya mwanajamii. Wanathibithisha madai yao kwa kurejelea madai ya Hartman(1982). Hartman anaeleza hali ambayo jamii inagawia wanajamii majukumu kwa kufuata utaratibu maalum. Kazi na staha zinafanywa na wanaume. Zile zinazoonekana kuwa duni zinaachiwa wanawake. Anaona kuwa huu ni ubepari wa kijinsia: kulingana nao jamii yenye mfumo kama huu, huendeleza utabaka wa kijinsia. Hartman, kwa mujibu wake, anaeleza namna wanaume hufaulu kudumisha hadhi yao ya juu. Anaona ukuruba baina ya ubabe-dume na ubepari. Kutokana na hali hii mwanamke hugawiwa majukumu mengi ya kinyumbani.

### 2.5.3 Uteuzi wa Sudana Kama Kiongozi wa Kike

TUKI (1984:153) inaeleza kuwa sitiari inafafanuliwa kama tamathali ya usemi inayohusisha vitu au viumbe viwili vilivyotofauti kitabia au kimaumbile kwa msingi wa sifa fulani iliyopo katika vyote viwili lakini ulinganishi huo haujitokezi wazi kwa sababu ya ukosefu wa vilinganishi kama vile 'mfano wa', 'kama' 'mithili ya' na 'sawasawa na'. Matumizi ya sitairi hujenga taswira fulani, kwa hivyo msanii anapomwita mhusika fulani 'twiga' inawezekana mhusika huyo kuwa mwenye sifa zinazoshabihiana na za mnyama huyo kama vile urefu. Mhusika Sudana ameteuliwa kiistriari.

Sudana ni msafiri mkembe, anayesafiri na jamaa yake baharini. Kwa bahati mbaya anajikuta katikati ya washirika wawili wakatili – Amerigo na Muzungu. Watu hawa wawili wametawaliwa na imani, mielekeo na taasubi kali za kiume. Sudana anatatizika baina ya kulinda hadhi yake, kwa upande mmoja na kuiuza kwa upande mwingine ili kuwanusuru wanawe wasiangamizwe katika madhila na mizigo

wanaowatwika washirika Amerigo na Muzungu. Sudana ni kiongozi wa kike aliye na maono ya mbali. Zaidi ya changamoto anazozipitia baharini kweli ni kiongozi anayepigania usawa na haki ya walio wanyonge.

### 2.5.4 Uteuzi wa Bikisiwa kama Kiongozi wa Kike

Bikisiwa ndiye mhusika mkuu katika tamthilia hii ya *Posa za Bikisiwa*. Mwana dada huyu amezaliwa na kulelewa katika jamii ya utashi. Wazazi wake ni mfalme na malkia. Katika jamii yoyote ile tujuayo, milki kama hizi zina umuhimu mkuu. Mtoto yeyote alelewaye katika jamii hizi hulindwa na kuamuliwa mengi na wazazi wake. Tofauti na jamii za kale, Bikisiwa amechorwa na waandishi *Mohamed na Kitula,* kama kiongozi aliye na maono tofauti katika karne hii. Bikisiwa ni kiongozi anayetangulia, aliye mbele na hata anayewaongoza wenzake kwa njia ifaayo. Utandawazi umeleta uwanagenzi katika jamii ya Bikisiwa. Kiongozi huyu amehanikiza uhusiano wenye kupendwa na kuenziwa na wengi.

Bikisiwa anapobaleghe anachaguliwa mume wa kumuoa. Kinyume na matarajio ya wazazi wake, anapinga mfumo wa kikale wa kuchaguliwa cha kufanya au cha kujihusisha nacho. Bikisiwa anabadilika na kuwa mpya mwenye mawazo mapya ya kisasa yanayowazindua wahusika wengine katika tamthilia hii. Wanaume wengi wamejaribu kumposa Bikisiwa – binti mrembo, malkia mwenye nyota ya jaha. Kuna wanaotumia nguvu za misuli yao kumvutia, wengine vitisho, wengine pesa. Kina Sogoramaneno wametumia maneno kumsuta na kumuongoa, wengine zawadi, lakini vyote hivi kwa Bikisiwa si lolote si chochote. Anachohitaji ni mapenzi ya kweli, na kama anavyosema mwenyewe... "*Nangojea posa za hapa petu, bila ya shaka, zikiwaposa za maslahi ya pande zote*'' (uk. 32).

## 2.6 Hitimisho

Katika sura hii, tumeangazia na kuchunguza kwa kina dhana ya tamthilia, historia fupi ya tamthilia teule, dhana ya wahusika na uteuzi wa kiongozi wa kike katika tamthilia teule za lugha ya Kiswahili.

# SURA YA TATU

# NAFASI YA KIONGOZI WA KIKE KATIKA TEULE ZA KISWAHILI

## 3.1Utangulizi

Sura hii inahusu nafasi ya kiongoziwa kike katika tamthilia teule za Kiswahili. Katika uchunguzi wetu tumeweza kutafiti nafasi mbalimbali ya kiongozi mwanamke kama mhusika katika kazi teule za utafiti huu. Nafasi zenyewe zinajidhirisha wazi katika vitengo viwili vikuu: nafasi dhalilishi na nafasi chanya.

Katika sehemu ya kwanza, tutachunguza nafasi dhalilishi anayopewa mwanamke katika uongozi wake jamii ya tamthilia*;* kuna kuenea kwa taasubi ya kiume ambapo mila na desturi zinampendelea na kumpa kipaumbele mwanamume na kumtesa mwanamke na hivyo mwanamke kuonewa na kutosikilizwa katika hatamu zake za uongozi. Mitazamo hii ambayo ni mikatale ya utamaduni unaomsawiri mwanamke kama chombo cha mapenzi, chombo cha kuzaa na kulea, na kuitwa malaya akitangamana na wanaume akipigania haki za wafanyikazi katika shamba la Delamon, ugawaji wa kazi kumkandamiza mwanamke, kuonewa kwa sababu ya maumbile, uhusiano wa kudunisha mwanamke katika hali ya juu katika jumuiya ya fasihi, kudhulumiwa akipigania haki za wafanyikazi na kiumbe cha huduma.

Katika sehemu ya pili, tumeangazia nafasi chanya anayopewa mwanamke kiongozi. Mwandishi amemjenga mwanamke kihadhi kwa kumwinua katika jamii inayomdhalilisha na kumdunisha. Kupuuza mwanamke katika jamii inayozingatia haki na usawa wa kijinsia. Waandishi wamempa na kuchochea mwamko wa mwanamke. Mwanamke amesawiriwa kama jasiri, mwenye bidii, na anayestahili uhuru wa kimawazo.

## 3.2Nafasi Dhalilishi na Duni ya Kiongozi Mwanamke

Suala la usawa wa kijinsia limepewa kipaumbele katika tamthilia za Kiswahili. Waandishi wameangazia ukinzani wa kimtazamo ulivyo kuhusu nafasi ya mwanamke kama kiongozi katika jamii. Pana changamoto tele anazokumbana nazo na hili linatupa taswira jinsi mfumo huu umejikita na kujijenga katika mila na desturi baguzi za jamii ambazo zinamtukuza mwanamume na kumkandamiza mwanamke.

Millet (1969) anapinga malezi yanayomrutubisha na kudumisha ukinzani na ukandamizaji wa mwanamke. Millet anaeleza namna ambavyo mtotowa kiume

hulelewa kwa namna ya kumwandaa kuwa mwanamume ‘kamili’ mwenye udhibiti na anayetumia nguvu kujisimamia kiume. Mtoto wa kiume huonea fahari kiungo cha kiume na kuchukulia kama taashira ya ‘uwezo’ wa mwanamume. Mfano mahususi, katika tamthilia ya kiingereza *Betrayal In The City (1976),* mhusika Mulili anaonyesha mawazo kama hayo. Anamdadisi mwenzake Jere kuhusu haja ya kunyenyekea mbele ya wahusika Doga na Nina. Anamwambia Jere, *wakati mwingine, najiuliza ni kwa nini unamiliki kiungo hicho, katikati ya miguu yako* (pp. 13)

Nafasi ya mwanamke katika jamii imekuwa kadri jamii za ulimwengu zinavyochukua muundo tofauti.Katika jamii za enzi za kale kulikuwa hakuna matabaka. Lakini tunaposema matabaka tuna maana gani kwa mujibu wa Leon, T.

> *“Matabaka ya kijamii ni makundi makubwa ya watu wanaotofautiana kwa sababu ya nafasi walioishika katika mfumo wa kihistoria na kiuchumi.’’.*

Maana ya kauli hii ni kuwa, mwanamume aliwekwa kwa jamii au tabaka la juu ilhali mwanamke aliwekwa tabaka la chini. Tabaka la juu ndilo lililomiliki mali yote, mashamba na hata watu -wanawake- na watoto. Uongozi ulitunukiwa tabaka hili la juu na kuwaachia wanawake tabaka la chini la kutii amri kutoka kwa tabaka la juu.

Uzalishaji mali katika uhusiano huu wa kitabaka uliwekwa na kudumishwa kisheria. Njia za uzalishaji mali katika jamii husika ilikuwa jukumu la wafanyikazai. Kulikuwepo pia mkondo wa kupokea rasilmali za jamii ulikubalika. Mambo mawili katika maelezo haya ni kwamba watu wa tabaka moja huwa wameshika nafasi moja katika mfumo wa uzalishaji mali na njia za uzalishaji mali. Katika mfumo wa zamani wa kijamii uliokuweko, kila mtu alifanya kazi kwa manufaa ya jamii na njia za uzalishaji mali hazikumilikiwa na watu binafsi bali zilikuwa mali ya umma. Njia zilizokubalika zilitumiwa kwa manufaa ya umma huo. Lakini kadri jamii zilivyoendelea kukua, ndivyo uhusiano wa kikazi ulivyoanza kubadilika.

Hapo kale, akina mama walishughulikia mambo ya nyumbani wakati wanaume walikuwa wasasi. Kazi ya kina mama nyumbani ilikuwa ya kijamii, nyumba ilikuwa kiwanda cha kutayarishia wanaume vyakula lakini hali hii ilibadilika wanaume walipoanza kuwatawala wanawake manyumbani mwao. Jamii iliacha kujishughulisha na mambo ya kinyumbani, upishi, na kadhalika, ukawa huduma ya kibinafsi.

Mwanamke akaanza kuwa mtumishi nyumbani anayepaswa kumtii mumewe na kumhudumia kwa kila njia. Uhusiano huo umeendelea kusisitizwa na tamaduni nyingi barani Afrika na hali hii ya kudunishwa kwa hadhi ya mwanamke kumeandamana na kupandishwa kwa hadhi ya mwanamume.

Hali hiyo imemfanya mwanamume aliye na taasubi za kiume kujichukulia kama binadamu mwenye cheo, heshima na hadhi kubwa zaidi anapolinganishwa na mwanamke. Katika mfumo wa kipebari haja ya wafanyikazi kiwandani na kwingineko imewaandama wanawake wengi majumbani na kuwaingisha katika shughuli za uzalishaji wa mtaji. Lakini idadi ya wanawake wafanyao kazi ya mshahara viwandani na kwingineko ingali ndogo sana. Wengi wao wamebaki kuwategemea waume wao katika mahitaji yao ya kila siku. Hata wale wanaofanya kazi mashambani na viwandani wakizalisha mtaji, wanatarajiwa na jamii kuwahudumia waume wao kwa kila hali. Huduma zote za nyumbani zinatarajiwa kutolewa kwa njia ya kutosheleza. Hivyo ndivyo hali ilivyo kwa Lanina na wanawake wengine wa *Kilio cha Haki*. Lanina anajikuta akikinzana na Delamon (kaburu mwenye shamba) na Mwengo (mumewe).

### 3.2.1 Mwanamke Kuteswa Kwa Sababu ya Maumbile

Mwanamke ananyanyaswa, anadhulumiwa na kuonewa kwa sababu ya maumbile yake ya kike, anadhulumiwa katika mazingira ya kikazi, ananyimwa haki ya jasho lake na nguvu yake ilhali yeye ni mfanyikazi kama wanaume.

Dhuluma ni tele. Mwanzo Lanina anakamatwa na kupelekwa mahakamani kwa kisingizio cha kuchochea mgomo wa wafanyakazi wa shamba la Bwana Delamon. Habari hizi zinasomwa na Musa na Dewe katika gazeti moja lililotupwa jaani.

> ‘‘LANINA KUPELEKWA MAHAKAMANI’’,
> Lanina wa Muyaka, mwanamke aliyekuwa
> Mfanyakazikatika shambamaarufu
> la Bwana Delamon, ametiwa tena kizuizini.
> ...alichocheamgomomkubwa…(uk. 2)

Wafanyikazi kama Musa na Dewe wanajaribu kusoma zaidi kujua sababu za kiongozi wao kukamatwa na kuwekewa lawama za kuchochea mgomo na mauaji ya manokoa watatu wa shamba la Bwana Delamon. Kauli yao ni kuwa Lanina ameonewa na kufitiniwa na wasaliti. Ingawa Lanina hakuwepo alidhaniwa kauchochea mgomo na kukamatwa kwa visingizio tu. Mgomo huu na mauaji tunaona unawatorosha Musa

na Dewe hadi nchi geni. *Maishayatakuwa magumu hapa ugenini* (uk.1). Musa na mwenzake ni wa jinsia ya kiume ambao wana uwezo wa kutoroka na kula makombo yaliyotupwa mapipani angalau wayanusuru maisha yao, jambo gumu kwa mwanamke kufanya.

Lanina kama kiongozi wa kike anapojaribu kutetea haki zao kama wafanyikazi wa Delamon, anapigwa kofi huku akiulizwa aache upuzi wake kwa sababu anapigania haki, kitu ambacho yeye kama mwanamke hakielewi. Kwa mujibu wa askari ambaye ana ubabedume ni kwamba mwanamke hana haki mbele ya mwanamume.

LANINA: Lakini sisi tunajaribu kutetea haki zetu kama…

ASKARI 1: (*Anampiga Lanina kofi*)

Wacha upuuzi wake huo!
Haki! Haki! Unapigania...
hata ukipewa hujui……..
Mpumbavu wee! (uk. 14)

Dhuluma ipo pia katika mazingira ya kazi. Lanina ananyimwa haki ya nguvu na jasho lake kwa kuwa yeye ni mfanyikazi wa kike. Lanina anadhulumiwa na kuonewa kikazi kwa sababu hana nafasi katika ulimwengu unaotawaliwa na wanaume. Dhuluma hizi za kijinsia ndizo zinakuwa athari kwa ukombozi wa mwanamke kwa mazingira ya kikazi, ndiposa Lanina anapowaongoza wafanyikazi kugoma mwanamume anaona wivu na hata anatukanwa Malaya. Kosa lake kuu likiwa ni kutangamana na wanaume katika harakati za kupigania haki za wafanyikazi wa shamba la Delamon. Mwengo anaona udhia kuwahudumia watoto wake mkewe akiwa kifungo. Anakuwa kama mtu asiyejiweza, Mwengo anakubali kutiwa pingu na utamaduni katika uhusiano wake na mkewe.

MWENGO: Lanina! Lanina!
Wewe unajua… siku ngapi sasa
watoto wanakula chakula kibichi"
… Naona huna haja ya mume
wala watoto wewe. (uk. 29)

Halafu ,
"Angalia! Angalia namna gani
watoto wanavyotaabika;
Angali majonzi na shida zao!
Halafu unajiita mama yao" (uk. 30)

Hapa kunazuka athari za utamaduni ambao unamkandamiza mwanamke, badala ya Mwengo kumpa pole mkewe kwa dhiki alizopata gerezani anamgombeza kwa kumwaachia watoto kulea, naye Lanina anamjibu kwa busara, upole na kwa uzindushi wa hali ya juu kwamba hamna makosa yoyote mume kuihudumia familia yake, kuwapikia na kuwatazama watoto wake. Utamaduni uliopo ndio uliowafinyanga ndiposa hawapaswi kuwa wafungwa wa utamaduni wala kutawaliwa nao. Huu ni ushawishi na mwamko mpya wa mwanamke aliyejitolea kukosoa utamaduni ambao umepitwa na wakati na ambao unaegemea kuitukuza jinsia ya kiume.

LANINA*: (kwa upole zaidi)*
Na unaona ni makosa Mwengo?
Wewe kuwatunza watoto wako?
Wewe kupikia jamii yako.

LANINA: Utamaduni, utamaduni?
Utamaduni ni kitu gani Mwengo
Kwa nini…tuwe watumwa…….
Si sisi tulioufinyanga utamaduni
Si sisi tulioupa uhai utamaduni…
…kwa nini tuache utamaduni ututie
pingu na fahamu kuzitawala (uk. 32)

Wanaume wote wanaokuja kumposa Bikisiwa wanaonekana wakimletea vitu vya thamani ili kumshawishi awakubali. Jambo hili linatuonyesha wazi kwamba mwanamke anasawiriwa kwa nafasi duni ya kunaswa kwenye mapenzi kupitia vyombo vya dhahabu. SS anaposaidia jamii ya Bikisiwa kutokana na mavamizi ya wajukuu wa Kolumbus anahitaji malipo kwa kazi yake na hakuna malipo mwafaka bila kuozwa Bikisiwa, binti ya mfalme. Anapomrai ili amkubali anamwambia kuwa akimwoa ataishi kwao na kuwawekea ulinzi kisha anampa zawadi. Pete ya dhahabu, sakini za kupigania vita, magauni ya Hariri, vyombo vya mapambo vyenye vito vyema pamoja na farasi na watumishi ili ziwe kama dalili ya mapenzi yake kwa Bikisiwa. Lakini kupitia athari aliyonayo yeye kama kiongozi aliyezinduka kupigania haki za jamii yake, kutotekwa nyara na kuondoa mtazamo finyu kuwa wanawake ni watu wa kushawishika haraka kwa mapambo na vitu vizuri anamjibu SS kuwa ingekuwa bora wangelinda nchi yao wao wenyewe na wangefurahi sana ikiwa wangewafundisha mbinu zao za kulinda nchi na hivyo kuwaweka kina SS kama washauri wao. Na kuhusu zawadi zake za kumtaka amkubali Bikisiwa anamjibu kwa

ujasiri na werevu kwamba zawadi ni nzuri lakini haziyeyushi moyo wake na cha muhimu zaidi ni kwamba ndoa yao italeta natija gani kwake na kwa watu wa jamii yake. Kwa yakini nafasi na athari ya kiongozi wa kike imekumbwa na udunishi wa hali ya juu. Beauvior (1969) anafafanua hali ambapo wanawake wengi wamebakia katika ngome zao za nafsi kwamba wametekwa nyara na tamaa ya vitu vya thamani vinavyowafanya kuwa bora au kuonekana kama wanajiweza kwenye ushindani wa mapambo na mavazi kiasi kwamba hawajajikomboa kiakili.

Vishawishi hivi vya mapambo vinamwathiri sana Bikisiwa kwa kuwa kila anayekuja kumposa kuvitumia ili kumteka nyara kimawazo na kimwili. Bikisiwa amezinduka na harudi nyuma tena.

Wanawake katika jamii hii ya *Posa za Bisikiwa* wanadunishwa na vyombo vya dola kama vile askari. Askari hawawapi ulinzi raia wote hasa wanawake. Raia wanawapelekea malalamishi kwao ya kubakwa, hakuna hatua inayochukuliwa kama kuwatia mbaroni wanaowabaka. Sheria haina nguvu kwa vyovyote vile. Cecilia na Jane wanapokutana na Mpitanjia na Mtambaji, Mpitanjia anakuwa mwepesi kuwahukumu kwamba Cecilia na Jane ni malaya wanaokuja kujiuza jijini na wametimuliwa na polisi kwa kushindwa kulipa kodi za vyumba vyao vya laana huko wanakojiuza. Ukweli ni kuwa yanayowatorosha makwao si ubakaji. Cecilia amekimbia kwao ili kuhepa ndoa ya lazima na mtu wa kulazimishiwa naye Jane ametoroka kubakwa na mjombake. Ubabedume umewaathiri watu wa jamii kiasi kwamba hata watu wa familia yake si mamake, si babake wala si wapitanjia kwani kwao wanawake ndio wenye makosa. Mtambaji kwa maneno yake anaonyesha kwamba ni kweli jamii na vyombo vya dola kwa jumla haviaminiki vyote vimetawaliwa na umwamba wa kiume.

MTAMBAJI: ... Wakibakwawanataka wenyewe
na atakaye sheria haimkamati kwa sababu
wanawake wanataka wenyewe kubakwa.
Mwacheni bwana huyu kwani mpaka sasa
hajaelimika na masuala ya wanawake.
...Bado ana jeuri ya kijanadume(uk. 27)

Kweli sheria katika jamii hii haikutungiwa mwanamke jamii nzima hasa Mpitanjia hajaelimika na masuala ya wanawake na hata simulizi ya Mtambaji haijawaathiri kwa vyovyote vile kuuondoa ujeuri wa kijanadume. Sheria inaamini kuwa mwanamke

ndiye mwepesi wa kuingia kwenye laana ndiposa kwa kila jambo sheria inamhukumu mwanamke kama mwenye makosa.

Athari inayotokana na utamaduni uliopo kwenye jamii hii inaonekana kuinasa na kuathiri hata vyombo vya dola hasa Askari kubagua raia wake ndiposa hata mtambaji anakiri kwamba mambo haya yamekuwa sugu tena yameenea kila mahali na watu wanaiga mambo ya kinyama kwa vyovyote vile.

MTAMBAJI: Nimesadikisha kwambamambo
haya ni sugu tena yapo kila pahala.
Yameenea kote ….…….sishangai
watu wanaiga ya kinyumba (uk. 28)

Sheria ikijumuisha na ubabedume kwa wanaume kuongoza na kujifanya kuwa wao ndio wanaojua kila kitu na japo hawajui chochote, ndio chanzo cha kuanguka kwa wanawake na wanaowasukuma ni wanaume ambao ndio wanakamata hatamu na kuvuta ili kuwaangusha kabisa. Mvutano huu wa kuwaangusha wanawake ndio chanzo cha ufeministi. Sheria na vyombo vya dola kwa jumla kumwonea mwanamke na kumpendelea mwanamume.

### 3.2.2 Mwanamke kama Chombo cha Kumfurahisha Mwanamume

Millet (1969), katika harakati zake za kupinga nafasi chukivu ya mwanamke katika kazi za sanaa. Anadhihirisha namna mwanamume anavyolishughulikia tendo la ngono kama ishara ya uthibiti na uwezo juu ya mwanamke. Anaangazia kazi ya Jean Genet.*The Thiefs Journal*na anafafanua mtazamo wa mwandishi aliyeumba mhusika *Armand*. Mhusika *Armand* anajivunia na kuonea sarari ushindi wake kwa mwanamke ambaye ni kijakazi wake. *Armand* ananasibisha kitendo cha ngono na udhibiti, uwezo wake na ushindi.

Katika *Kilio cha Haki*, mwandishi anafaulu kutusawiria hali kama hiyo katika jamii hii aliyoitungia kazi yake. Amewaumba wanaume wawili Hatila na Kachero wanaojaribu kumvunjia heshima na kumnajisi Lanina. Haya yanadhihirisha kwamba mwanamke ni chombo cha kukidhi hisia za wanaume na vile vile chombo cha kumfurahisha mwanamume. Haya ni matokeo ya malezi kwa watoto wa kiume ambayo yamejaa taasubi ya kiume na kumpa mwanamume hadhi ya juu kuliko mwanamke.

MWENGO*: (Anakwenda alipokaa Lanina na kumkumbatia)*
...mimi mumeo na watoto wako**?**
Huoniya kwamba unatutupa kwa
sababu ya msimamo wako huo? (uk. 31)

Mwengo, mumewe Lanina anamsihi Lanina akae naye nyumbani na awache harakati za kupigania haki za wafanyakazi wa shamba la Delamon. Anataka mkewe akae amburudishe na awe mlezi. Harakati za kutafuta haki zinamfanya Lanina kujihusisha na wanaume, hali inayompa sifa ya kuwa malaya.

LANINA: Wewe pia unaamini kuwa mimi malaya Mwengo? (uk. 33)

ASKARI: Aaah! dada, usijifanye mtoto.
Unajua mimi na wewe tunaweza
kuona raha, na mimi nitakusaidia
Nitakuletea chakula kingi, sigara
….Unasemaje dada? (uk. 73)

Wanawake nao wanaonekana kuwa wamedanganyika kiasi cha kuamini kuwa wao ni vyombo kumridhisha mwanamume. Wanawake pia wametekwa nyara na mikatale ya utamaduni pale ambapo wamesawishika kwamba wao ni viumbe wa kuwahudumia wanaume. Mamake Lanina ni mfano mwema pale ambapo anampa nasaha Lanina kuwa utamaduni amemfunza kuwa mke daima awe chini ya mume. Lazima amtii na amhudumie mumewe. Kauli hii inaashiria kuwa badala ya mwanamke kujikomboa na mikatale ya utamaduni ametiwa pingu na kuukubali utamaduni unaomfanya chombo cha huduma na cha kukidhi hisia cha wanaume.

MAMA: Aaa! Aaa! Aaa! Usiseme hivyo mwanangu
Umefunzwa, mke daima awe chini ya mume?
Lazima amtii na amhudumie mumewe
Si umefunzwa hayo tangu utotoni…

MAMA: Mwanangu, fikra hizo za kihalifu…
Fikra hizo za kujifanya sawa na waume
Fikra hizo za kuharibu mila zetu
Fikra hizo umezitoa wapi?(uk. 41)

Kauli hizi zinadhihirisha wazi namna jamii inavyotawaliwa na taasubi ya kiume. Jamii yenyewe humlea mtoto wakiume kwa namna ya kumwandaa kutumia nguvu ili kudhihirisha uume wake. Mhusika Baba (babake Lanina) katika kauli yake

……..*Nitakupa mawaidha mazuri ya bakora*, kuonyesha kuwa kutumia nguvu kunaashiria uanaume.

Tamthilia ya *Posa Za Bikisiwa,*vilevile imeangazia jinsi mwanamke anavyosawiriwa kama chombo cha mapenzi kwenye sehemu ya utangulizi. Sauti ya mwanamke inasikika huku akisema kwamba nyinyi ni walewale mnaotaka kuudhibiti mwili wangu, mwili mnaweza kuuchukua kwa nguvu lakini hamwezi kuichukua roho yangu kwa nguvu. Hamwezi kuupata ukubalifu unaotoka moyoni mwangu.

MWANAMKE: Tuseme nanyi ni walewale
mnaotaka kuudhibiti mwili wangu?
Mwilimnaweza kuuchukuakwa nguvu
lakini hamwezi kuichukua roho yangu kwa nguvu.
Hamwezi kuupata ukubalifu unaotoka
moyoni mwangu.(uk. 2)

Waandishi hawa wawili, *Alamin Mazrui* na *Kimani Njogu* wamemsawiri Sudana kama ambaye ni mhusika wao mkuu kwenye tamthilia hii. Amerigo na Muzungu wanamchukulia Sudana kama chombo cha mapenzi na kutosheleza ashiki na haja za mwanaume. Sudana anajikuta katika njia panda na kutekwa nyara na taasubi ya kiume kiasi kwamba wanaume wamemdhibiti ili kutosheleza ashiki zao. Hata Sudzungu ambaye ni mwana wa Sudana ni mwana wa mimba haramu:

SUDANA: ...We!usizoeetenakuniita
‘‘Mwanamke’’!Mtovu wa adabu we!
Usisahau katu usisahau, kwamba mimi ni
mamayo,kwamba wewe ni mwanangu,
ingawa kwa mimba ya haramu. Hebu jaribu
kukumbuka hilo Sudzungu mtoto wangu! (uk. 22)

Kulingana uzungumzi huu mwanamke amechorwa kama chombo cha mapenzi na kuongeza kizazi. Licha ya Sudzungu kuwa mwanawe Sudana, anamshawishi mama yake kuitikia kuwa malaya wa Amerigo ili kupata pesa nyingi na ili kuimarisha uhusiano wao baina ya Wamerope na Wazanji.

SUDZUNGU: Haya pole mama sasa nasema ukubali tu!
Unajua Mwamerope ni Mwamerope atakupatia
marupurupu mengi na sisi wanao tunaweza
kunonea nunduni wasemaje mama?(uk. 23)

Jambo ili linamwathiri Sudana kiasi kwamba anajuta mbona hakuavya mimba iyo kuliko kuzaa mwana ambaye ni maradhi na asiye na heshima kwake. Sudana anasema kuwa alikosea kutowasikiliza wanawe wengine ambao walimrai kuiharibu mimba iyo kwa kupuuza ushauri wa wanawe, amezaa ibilisi ambaye anajifanya gagwadi wa mamaye na anazidi kumuuliza ni faida gani atakayoipata kwa kumgeuza mamaye malaya wa Wamerope. Hapa tunaona athari ya mwanamke inajitokeza kwamba ni kutokana kwa mwili wa mwanamke ndiko mwili wa mwana hukulia tangu kuwa mchanga hadi kiasi kwamba amefikia utu uzima. Pia ni kutokana na mwili wa Sudana ambapo Sudzungu na nduguze wengine wameweza kupata mahitaji yao yote. Mama mtu amekuwa mkate na mvinyo wa mwili wa Sudzungu na hilo latosha. Si lazima kumuuza mamake kwa Wamerope kama malaya lakini kwa kuungana kwa mama na watoto wake wanaweza kustawisha kizazi chenye nguvu na haiba.

Amerigo anapomshawishi Sudana kumkubali na kumtosheleza haja zake za ngono anakataa. Utamaduni umemfunza Amerigo kuwa yeye ni mwanaume na ana udhibiti juu ya mwanamke. Amerigo anaamua kumnajisi kwa nguvu na wanamfunga kwa silisili kitandani na kumwita Shume ambaye ni mwana wa Sudana kuja kushuhudia uovu huo. Shume anaathiriwa jinsi mamake anadhalilishwa na kufanywa chombo cha ngono kwa mwanaume mwenzake.

> SHUME: Kila nilalapo, ewe mama yangu,
> maumivu ya maonevu unayovumilia
> yanauchoma moyo wangu.lakini najua hayo
> yote yana mwisho wake. Ghera na heshima yako
> ni kama mtambo wa maisha yangu; manukato ya
> maziwa unayoninyonyesha hayatoki kinywani
> mwangu. Kwa hivyo usikate tamaa mama.
> Mwili wangu umejaa damu ya moyo wako(uk. 29)

Katika *Sudana,* waandishi *Alamin Mazrui* na *Kimani Njogu* wamefaulu pia kudhihirisha hali hii ya mwanamke kuwa miliki ya mwanaume kupitia kwa hali anazopitia Sudana. Mwanzo Sudana anapokataa kukubali matakwa ya Amerigo ya kuwa malaya, Amerigo anaamua kummiliki kwa nguvu ndiposa anaagiza wamerope wawili kumfunga kitandani kwa silisili na hatimaye ili kumfanya akubali kuwa miliki yake. Kisha anaagiza wamerope wamlete mwanaye Shume kukamatwa na kuchapwa viboko hamsini mgongoni na kunyimwa chakula kwa siku tatu. Amerigo anazidi kumwambia kwamba hali ingekuwa shwari ikiwa wangeafikiana tangu awali na

madhila haya yote hayangekuwa na ushenzi wowote. Sudana angerekebisha kwa njia ya malezi na mafunzo mema lakini kwa kuwa amekaidi kukubali awe kahaba na mali ya Amerigo. Kuna udhalili zaidi ya huu wa kufungwa silisili kitandani na kubakwa, kuona watoto wake wakipigwa wakihasiriwa vibaya sana, naye Sudana asiwe na uwezo wa kufanya lolote.

Amerigo anapotaka kuumiliki na kuudhibithi mwili wa Sudana kama chombo cha kukidhi haja zake za kingono Sudana anamkataa na kumjibu kuwa kumiliki mwili wake hawezi kwa kuwa mwili wake Sudana ni mwili wake tu. Naye Amerigo shauku yake kuizimia kwa mamake Shume na japo Amerigo anamwambia kuwa yeye ni tunda lake la peponi, Sudana ameathiriwa kiasi kwamba amechoshwa na ubabedume unaomfanya miliki ya mwanaume ndio maana Sudana anamjibu kuwa :

> SUDANA: Tunda? Kweli mimi ni tunda la peponi, lakini
> utaweza kulitunda? Ni tunda linalozingirwa na
> miba yenye sumu; waona litatundika? Na
> ukijasiri kulitunda utakuwa umeitunda roho
> yako; je u tayari kwa hilo? Hebu usighilibike kwa
> sura ukasahau sumu iliyomo ndani – Au
> umesahau ya Adamu?! (uk. 43)

**3.2.3 Kanuni za Utamaduni Kutomtambua Kiongozi wa Kike.**

Utamaduni umetoa kanuni za kufuatwa katika utangamano wa wanaume na wanawake na kwamba anayekiuka kanuni hizo anachukuliwa kama msaliti.

> BABA: Vijana wa siku hizi!..
> Na hasa vijana wa kike
> wanataka kuwa waume.
> ...Ole wao, wanaotupilia
> mbali mila zao! (uk.36)

Kulingana na kauli hii ya baba yake Lanina, Lanina anataka kuwa mzungu kwa kupigania haki za wafanyakazi. Baba anamkana Lanina asiitwe mwanaye na hata kumlaani. Anamkataa Lanina na hata kumtusi malaya. Harakati za Lanina kupigania usawa unampa mama yake mwamko mpya wa maisha. Anamtakia heri na fanaka katika mkondo wake mpya wa maisha wa kuongoza.

> MAMA: Lanina sasa ana kazi mjini,
> …Lanina ni kijana kidogo
> Jicho la hasidi lisimkumbe. (uk. 37)

Kanuni hizo ndizo zinazomfanya Seromanga kumpiga Lanina hata kabla hajamaliza habari za kizuizini.  Babake Lanina anamwaambia Lanina,

BABA: Na wewe binti wa shetani!
Mimi si wanaume wale wengine unaowachezea
Mimi si akina Mwengo
Mimi ni dume kweli kweli
Kaa nalo ulifunze adabu na heshima
Ulifunze maana ya uuke! (uk. 38)

Utamaduni umemfunza Seromanga kwamba mke hapaswi kuwa na tabia za ‘kiume’kama kupigania haki na usawa, umemfunza kwamba Mwengo hapaswi kupika, kufagia au kufua. Yeyote anayejaribu kubadilisha kaida hata kama ni mbavu ni ‘msaliti’.  Jamii imempa Seromanga uwezo wa kuwapiga mkewe na bintiye. Lanina anapigwa ili udume wake ukomeshwe ili afuate tabia za uuke.

Lanina anaitwa ‘Malaya’ kosa lake likiwa ni kuandamana na wanaume katika harakati za kupigania haki za wafanyikazi. Kachero wa kwanza anamwambia Lanina kuwa ni Malaya, anamwacha bwana yake na watoto nyumbani akizurura na wanaume wengine huku akijifanya anapigania haki.

KACHERO 1: Malaya huyu nitamwonyesha
Huyu mwanamke gani huyu
anamwacha mumewe na watoto nyumbani
Huku akizurura na wanaume wengine,
ati wanapigania haki zao na
Salamu zetu kututawalia.Utupige pande
na tabia yetu ya kuzingatia?
Kwa nini Mwengo!..
Tuendelee kufuata utamaduni
Hata uwapo makosani yamkini? (uk. 32)

### 3.2.4 Utamaduni na Ugavi wa Kazi Unaomkandamiza Mwanamke Kiongozi.

Beauviour(1969), anafafanua hali ambapo wanawake wengi wamebakia katika ngome zao za awali, kwamba hawa hawajajikomboa kiakili. Desturi za kike zinawajibika na kuwafanya watosheke kiuchumi na kijamii katika hali duni ya maisha. Jambo ambalo litamfanya mwanamume awe na taasubi za kiume kwa kujichukulia kama binadamu mwenye cheo, heshima na hadhi kubwa zaidi alinganishwapo na mwanamke.

Katika shamba la Delamon, Lanina tu ndiye mwanamke kiongozi anayejitolea kupigania haki na usawa wa wafanyikazi katika shamba la Delamon mwandishi *A.*

*Mazrui* hajawapa wanawake wengine hadhi hii ili kutupa taswira ya jinsi jamii hii imejaa taasubi ya kiume.

MAMA: Aaa! Aaa! Aaa! Usiseme hivyo mwanangu.
Si umefunzwa, mke daima awe chini ya mume?
Lazima amtii na amhudumie mumewe
Si umefunzwa hayo Lanina?
Si tumekufunza hayo tangu utotoni? (uk. 41)

Kama asemavyo Lanina hatupaswi kuwa watumwa wa utamaduni tuliofinyanga. Mwengo anapolalamika kuwa anawapikia watoto wake siku nyingine, kinyume na utamaduni anaambiwa:

LANINA: Kwa nini sisi tuwe watumwa wa utamaduni wetu!
Mwengo…
Si sisi tuliofinyanga utamaduni?
Si sisi tulioupa uhai utamaduni,uhai wa kutuongoa?
Basi kwa nini tuache utamaduni
ututie pingu na fahamu (uk. 32)

Mamake Lanina amekubali kufuata utamaduni japo uko na makosa yanayoonekana wazi. Hana sauti '*simba angurumapo'*. Hata katika umri wake mkubwa wa nyanya anapigwa na mumewe na kurudishwa kwa shangazi akafunzwe "kutii".

BABA:Na wewe, naona makungwi hawakufanya kazi yao vizuri.
Twende! Twende nikupeleke kwa shangazi yako
akufundishe tena kumtii bwanako (uk. 42)

Jambo hili la kuponzeka na utamaduni linamfunga hadi kwamba hawezi akaunga juhudi za binti yake katika harakati zake za kupigania haki na usawa katika jamii iliyojaa kasumba za taasubi ya kiume badala yake anamkanya binti yake na kumwambia kuwa utamaduni umetufunza daima kumtii mwanamume na kumhudumia.

Katika tamthilia ya *Posa za Bikisiwa,* wote waliomposa Bikisiwa, Biss, Sogoramaneno na Chachi, walitaka wamuoe kwa maslahi yao. Walitaka waudhibiti mwili wake. Azma kuu ya waliotaka kumuoa ni kuudhibiti mwili wake kama chombo cha mapenzi tu. *Mnataka, mnataka, mnataka kila kitu changu, lakini hamtaki kujali pande zote zinazohusika katika maisha yenu na yangu?*(uk.2)

BISS anataka kufunga ndoa mara moja ili aweze kummiliki Bikisiwa kabla wapinzani wengine hawajapata fursa ya kummiliki.

BISS: Kilichonileta ni pendo la moyoni.
Wewe ni tunda zuri li'lo mtini
Hamu imeningia mtimani
Nisipokupata wewe
Washindani wangu watakutia mikononi
Heri tuoane mara moja bila kisirani
Tuoane hivi sasa...(uk. 44)

BIKISIWA:Mbona maneno makali namna
hiyo? ...wewe umekuja kuposa au kunininua na
kunipora? Wewe ni mlowezi au mwindaji
haramu?.... (uk. 44)

Hali hii ya umiliki wa mwanamke pia inajitokeza katika *So long A Letter (1980: 10),* Ramatoulaye alikuwa na wanaume wengi waliotaka kumwoa tena baada ya bwanake kufariki. Tamaduni za jamii hii zinapeana ruhusa mwanamke kurithiwa na mwanamume mwengine pindi mume wake anapofariki. Ramatoulaye alikuwa ameanza ujenzi wa nyumba, naye mumewe akijiandikia kama miliki yake. Ramatoulaye anasononeka kwa namna mumewe, anamjengea mamake nyumba. Ramatoulaye mwenyewe anaamua kumwaga dukuduku lake kwa shogake, Aissatou. Anafanya hivi katika hatua ya 'kujitibu'.

Katika tamthilia hii ya *Posa za Bikisiwa,* mwanamke amesawiria kama kiumbe asiye na uwezo wa kujiamulia. Suala la ndoa ni swala ambalo linahitaji mtu binafsi kujiamulia wala si kulazimishwa au kuamuliwa na mtu mwingine. Mhusika mkuu Bikisiwa anajikuta katika njia panda kwa sababu posa zake zinakuwa nyingi. Mfalme ambaye ni babake hampi nafasi ya kujiamulia bali anataka kumfanyia uamuzi. Bikisiwa anamwambia babake kuwa kosa ni lake kwa kutotaka kushauriana na raia kuhusu posa zake. Yamkini mfalme hakutaka ushauri wowote kwa ndoa ya binti yake. Mfalme alijiona kuwa anaweza akafanya uamuzi kwa niaba ya binti yake jambo ambalo alisahau ni kwamba ndoa ni ya bintiye Bikisiwa bali si yake. Isitoshe, asasi za kitamaduni zilizoenziwa zilimpa mwanamume uwezo na hadhi kubwa akajitwika suala hili mwenyewe. Mfalme hawezi hata kushauriana na mkewe aliye malkia ili ampe mawaidha. Mfalme anaamua binafsi na kumchagulia Sogoramaneno - mwanamume ambaye Bikisiwa hakumpenda

BIKISIWA: Samahani baba, lakini kosa ni lako
hakipendi wala kukitaka na yeye tangu
mwanzo hakuridhia na moyo na nadharia
yake ilikuwa mbali na Sogoramaneno na alishuku

maana ya posa naye ilikuwa posa iliyosimama
kijuujuu tu. (uk.18)

Posa au uchumba lazima usimame ndani ya nafsi za wanaochumbiana. Nafasi ya Bikisiwa ilimwonya kwamba ndoa ila ingempoza kwa mwanamume aliyelazimishiwa.

Katika Posa ya Bikisiwa utamaduni haumpi mwanamke ruhusa ya kuamua juu ya ndoa na ni wajibu wa mwanaume kufanya uamuzi, ndio maana Mfalme hakutaka kumshauri mtu yeyote kuhusu ndoa ya Bikisiwa na alitaka afanye uamuzi pekee yake bila rai za watu wengine, ndio maana Sogoramaneno anapokuja kumposa Bikisiwa taasubi ya kiume inampata Mfalme na anaidhinisha posa hiyo bila kumshauri bintiye. Utamaduni umemfanya pia mwanamke kuwa miliki ya mwanaume kupitia sauti inayopenya dirishani chumbani mwa Bikisiwa:

SAUTI:Wewe Bikisiwa wewe ni mwanamke tu
sikiliza maneno yangu ili upulike, mwanamke
ni mwanamke uko chini yangu hata huwe
'Kisiwa', wewe ni wangu tu ukitaka usitake
wewe ni mali yangu upende usipende. (uk. 19)

### 3.2.5 Mwanamke kama Kizingiti cha Ukombozi wa Mwanamke Mwenzake

Wanjiku na Akinyi (1993), katika uchunguzi wao kuhusu hali ya mwanamke barani Afrika, wametoa mchango mkubwa. Walitambua kuwa jamii nyingi za kiafrika humnasibisha mwanamke na dosari ya kijamii. Kwamba nafasi za uongozi na kiuchumi hudhibitiwa na mwanamume. Mwanamke hashirikishwi kamwe kwa sababu ya kuhusishwa na dosari.

Mama yake Lanina, licha ya umri wake mkubwa - mama mzee, hawezi simama imara na kuunga juhudi za bintiye kujikomboa na mikatale ya utamaduni inayomkweza mwanamume na kutweza mwanamke. Yeye anadhihirisha wazi kuwa adui ya mwanamke ni mwanamke mwenzake. Anatekwa nyara na utamaduni unaomfanya asiweze kuona bintiye anapigania maslahi ya wote usawa kwa wanawake katika nafsi za uongozi na haki za wafanyikazi wote wake kwa wanaume. Tabia hii ya wanawake kujua utamaduni una makosa ya wazi na kutokuwa na sauti ya kuukashifu, ni baadhi ya mambo yanayolemeza juhudi za Lanina za ukombozi wa wanawake ambao wamekwama na utamaduni uliopitwa na wakati na enzi za mama mkongwe (mamake Lanina) kurudishwa kwa shangazi yake kufunzwa kutii, naye hapingi. Mila na desturi

kama hizi zimepitwa na majira ndiposa Lanina licha ya pingamizi zote kama mhusika mkuu anatoa wito wanawake wasidunishwe. Lanina awe kielelezo cha mwanamke anayejikomboa kifikra na ambaye yuko mbioni kupigania haki za waodhulumiwa. Aidha, mwandishi anasema ukandamishaji wa wanawake unarudisha nyuma ukombozi wa wale wote wanaodhulumiwa. Kwa hivyo wanaume kwa wanawake hawana budi kuungana dhidi ya Delamon anayewadhulumu wote kiuchumi.

Katika tamthilia ya *Pango*, mwandishi huyu pia amefaulu kumsawiri mwanamke katika nafasi dunishi ya kuwa msaliti wa jamii yake. Mwanamke badala ya kushirikiana na jamii yake kufanya maendeleo ambayo ni ya manufaa kwa jamii yao na kujikakamua ili ajiinue na kijijenga kihadhi anafanya mambo ya kuibomoa jamii hivyo kuisaliti jamii. Babake Katango anawasingizia binti zake kuwa ndio wanaocheza ‘pangoni’ na hasa ndio chanzo cha hali ya ‘pangoni’ kuharibika. *Nyukiwamegoma kuunda asali kwa kuwa wanacheza na kulisha mifugo karibu na pango*. Katango naye anashtakiwa kwa babake kuwa wamemgundua yeye ndiye hucheza pangoni kwa kujigeuza kizuu na bali si wao kama vile baba yao amekuwa akiwadhania. Katango ambaye ni mgombea wa nafasi ya ulinzi wa pango kuonekana kucheza pangoni ni usaliti wa wanajamii kuwa na imani naye kulinda pango ipasavyo.

Uyakinifu huu wa kumsawiri mwanamke kama msaliti ni uyakinifu ambao unatufichulia ukweli uliopo kwenye tamthilia ya *Pango*, kwamba uonevu alionao mwanamke katika harakati mbalimbali za maisha na kwamba jamii ziko mbioni kuacha hali dhaifu na dunishi dhidi ya dhuluma mbalimbali za kijamii. Mbinu mwafaka ni kukabili utu kikamilifu na kujitenga na mivutano ya utamaduni iliyopo kati ya wanaume na wanawake. Hali hii bila shaka inaonyesha upana na utatanishi wa maisha na jambo hili lisipoangaziwa kwa umakini linazua mgogoro wa kijinsia katika jamii. Tukimtazama Katango huenda tukafikiri ni mhusika wa kidhanifu. Kwa mujibu wa nadharia ya uyakinifu wa kijamii, Katango anawezekana. Katango ni kielelezo cha viongozi wanawake ambao wakipewa nafasi wanaweza wakaongoza vyema zaidi kuliko hata wanaume wanavyoongoza ulimwengu wa kisasa. Iwapo jamii itatupilia mbali mtazamo finyu kuwa wanawake ni wasaliti na kuwapa fursa ili kujiinua kitabia na kimawazo ili kiwe kigezo cha kila mmoja wetu ajipime kwacho na tukiona tumepungukiwa, tujifungate masombo tujaribu kumfikia.

Katango anaathiriwa na hii nafasi dunishi ya kutosikizwa na kupewa nafasi kuongoza kiasi kwamba si wanawake tu ambao hawajapewa fursa ya kuongoza bali vijana ambao Katango anawawakilisha hawajapewa fursa. Kuathiriwa huku kwa Katango kutoongoza na kuwa mlinzi wa pango kunadhihirisha kweli mabadiliko si rahisi kukubalika.

### 3.2.6 Mwanamke kama Kiumbe Asiyeweza Kuongoza

Kwenye tamthilia hii ya Sudana, waandishi wamemsawiri mwanamke kama kiumbe anayepitia madhila na mateso mbali mbali anapowapigania wanawe kwa kila hali. Ni kweli kuwa aijuaye dhiki na uchungu wa mwana ni mama. Sudana amepitia hali nyingi dunishi kwenye juhudi zake za kuwatetea na kuwaongoza wanawe. Sudana haya kwa kuonyesha taabu iliyo Afrika, bara ambalo bado halijajitawala. Limekolea ukoloni mamboleo:

> SUDANA: Wanangu, wana-Afrika,
> ... silaha mikononi
> ... hamu yenu ya uhuru
> hamu isiyofifia. (uk. 3)

> SUDANA: ...dunia inayowazunguka ikipasua
> kicheko na kucheka tambo lenu huzidi
> kuinamika kwa mzigo wa mchana
> mlioutweka mabegani mwenu mzigo
> dhahiri wa madhila yenu….(uk. 4)

Hali hii inadhihirisha wazi madhila aliyonayo Sudana kwa kuona watoto wake wakiteseka matekani waliko. Wakiwafanyia wamerope kazi inamuuma sana. Dhiki wanazopitia wanawe zinamsononesha kiasi kwamba kwa vyovyote vile amejitolea kupigania haki za wanawe hadi kifo chake licha ya kuwa na udhaifu wa mamlaka aliyonayo. Sudana hana uwezo wa kuwatetea watoto wake vilivyo.Mwanawe Sizwe anapokaidi amri ya wamerope ya kuibomoa meli ya wazanji na kutoa mbao anafikishwa mbele ya Amerigo na kushtakiwa. Sudana anashtuka na kujazwa na kilio asijue la kufanya naye Amerigo anamwambia maisha ya Sizwe yamo mikononi mwake.

> AMERIGO: ... Sudana, maisha yake yamo mikononi
> mwako. **'The decision is yours'**(uk. 37)

Ni kupitia kwa madhila haya ndipo Sudana anamwambia Sizwe kwamba licha ya kifo chake hatakufa, bali atakuwa chanzo cha uzindushi na uzalendo utakaoibua hisia na kuwachochea wazanji kuungana pamoja kupigania haki zao kutokana na dhuluma za wamerope. Kifo cha Sizwe kingeleta mwamko mpya wa kupigania haki zao na kuleta uongozi thabiti wa Sudana. Hata hiyo Sudana anayakini kuwa kamwe Sizwe hafi bali kuleta usawa na utekelezaji wa haki za kimsingi kwa kila binadamu.

SUDANA: Ni kweli Sizwe! Maadamu mimi ni hai
nawe katu hutakufa Sizwe, ndiyo katika
kifo chako katu hutakufa Sizwe,
kwani katika kifo chako mna mbegu
zisizo idadi ya kizazi chako,
basi katu hutakufa Sizwe.(uk. 40)

Katango na Ngwese ndio wanaogombea kiti cha mlinda 'pango'. Ngwese anaamini yeye ndiye kiongozi bora tu. Jamii nyingi ikiwemo jamii ya 'pango' zinashikilia tamaduni zinazomwinua kihadhi mwanaume na kumfanya kiongozi bora kiasi kwamba hata wakati ni wafisadi na wezi wanaofuja mali ya umma watazidi na wanaendelea kuwa katika nyadhifa za uongozi. Mwanamke hawezi kuwa kiongozi, hizi ni jamii zilizosheheni ubabedume.

NGWESE: ...Kuna nani mwingine wa kuchaguliwa
isipokuwa mimi? Nani niambie isipokuwa mimi
ambaye ninapumua pumzi ya ukuu?
Nani isipokuwa mimi ambaye nimekulia
katika nyumba ya utawala? Utaona tu!
(*Kwa majivuno*). (uk. 11)

Katika tamthilia ya *Pango*, kiongozi wa kike Katango anajikuta katika kinyang`anyiro hiki kushindana katika uongozi wa kulinda 'pango'. Ni ushindani ambao si wa uongozi tu, bali ni ushindani wa kijinsia na pia kati ya vijana na wazee kupigania mabadiliko katika uongozi. Ngwese hafurahi kuwa na mwanamke ndiye mgombea mwenza, ndiposa anamwambia Katango kuwa hajapata kusikia mwanamke akiwania uongozi wa kulilinda pango, mawazo yake ni kuwa Katango ni mtovu wa nidhamu anafaa kuolewa na kutiwa adabu na mumewe.

NGWESE: (Akicheka) Umesikia wapi

Katango maji ya mto kuupanda
Mlima; niambie umesikia wapi?
Mwanamke kuongoza pango...(uk. 11)

Katango pia anaonekana kutoelewana na baba yake kuhusu suala hili la uongozi. Badala ya baba mzazi kumuunga bintiye mkono, lake ni kumsuta na kumtukana. Hata wakati Katango anapoikuta uta na mishale na kuiokota babake anamkashifu kwa kuvunja utamaduni na kwamba atailetea jamii yake laana. Kisa na maana ni kuwa sheria na kaida za utamaduni wao haziruhusu mwanamke kushika ala za vita, ni mwiko na laana kwa familia na jamii kwa ujumla. Madai ya babake hayana mashiko yoyote, ni kasumba na unafiki tu. Ukweli ni kwamba babake hakupendelea kumwona bintiye akiwania uongozi wa kulilinda 'pango' kwa sababu yeye ni miongoni mwa watu ambao wanashikiriana na Ngwese kulichafua na kuliharibu 'pango' kiasi kwamba, hata nyuki kutengeneza asali imekuwa vigumu na bado wanasingizia binti zake kuwa ndio wanaocheza 'pangoni' na kuwafukuza nyuki.

Ngwese hana imani kwamba Katango anaweza kulinda 'pango', ni upumbavu na ndoto tu alizonazo na kwamba ukoo wake ni wa viongozi. Babu yake alikuwa kiongozi na familia ya Katango imekuwa ikiwaonea wivu tangu enzi hizo. Mtazamo huu unaonekana kuwa sawa na hali anayojikuta mhusika mkuu 'Natala' katika tamthilia ya *Natala*, mwandishi Kithaka wa Mberia, mwanamke ananasibishwa na hali duni ya upumbavu kwa hivyo, chochote au yeyote anayedhihirisha upumbavu ananasibishwa na mwanamke. Natala anapohoji maneno yenyewe anakumbushwa kuwa mwanamke aliumbwa kutokana na kifupa kidogo cha mwanaume kwa hivyo si sawa na mwanaune, kwamba nafasi yake ni chini ya mwanamume 'kimaumbile'. Ndiyo maana mwanaume hutafuta sababu za kumweka mwanamke katika nafasi ya chini na kwamba kulingana na Bibilia imekuwa hivyo tangu mwanzo wa ulimwengu.

Wanjiku na Akinyi (1993), katika uchunguzi wao kuhusu hali ya mwanamke barani Afrika na mchango wa kundi la wanawake. Walitambua kwamba jamii nyingi zimemtenga mwanamke na nafasi muhimu katika jamii, walibaini kuwa jamii nyingi humnasibisha mwanamke na ugomvi katika jamii, na kwamba nafasi za uongozi haziwaafiki wanawake kwa kuwa ni wagomvi na badala yake nafasi hizo za uongozi

zinastahili kuwa ni za wanaume na hudhibithiwa vilivyo na jinsia ya kiume huku mwanamke hashirikishwi kwa sababu ya dosari ’ugomvi’.

Katika *tamthilia ya Pango,* mwandishi naye amesawiri nafasi hiyo kwa kumhusisha mhusika wake mkuu Katango na uovu kama vile ugomvi, umbeya na usaliti.Kwanza kabisa mwanamke anasawiriwa kama mtu mgomvi na mtu asiye shukrani hata atendewe fadhila za kiwango gani. Huishia kudharau na kukosa shukrani. Katango anaambiwa na Ngwese kwamba, kugombana na mwanamke asubuhi na mapema ni ishara ya siku mbaya kwa mujibu wa Ngwese. Ugomvi wa mwanamke asubuhi ni ishara mbaya ya kuanza siku, huenda siku nzima ikawa siku ya mikosi. Ngwese anamwambia Katango yeye ni mwanamke na hapaswi kujibizana na mwanaume na nia yake ya kuwania nafasi ya kulinda pango ni ugomvi tu.

Kwa kujaribu kujua mbona Ngwese anawakataza wadogo wake –Susa na Sota- kupita njia kwenda kuteka maji anaonekana kuwa mgomvi na mwenye dharau kwani njia hiyo ambayo Ngwese anawakataza wasipitie ni njia iliyoko kwenye shamba lake. Kwake kuulizwa maswali na Katango ni kugombana naye na ni madharau. Ngwese ana haki ya kuwaambia wasipite kwa shamba lake wakienda kuteka maji na watafute njia mbadala ya kuwafikisha kuteka maji.

Lukacs (1963), kwenye kazi yake ’ *The meaning of contemporary Realism’*kwenye utafiti wake anasisitiza kwamba wanawake wananyanyaswa mara dufu kwa kutopewa nafasi ya kuwasilisha hoja zao kuhusiana na mtazamo wa maisha. Lukacs anasema kwamba, wanawake tangu enzi za kale wamekuwa hawana sauti mbele ya wanaume. Haya ni baadhi ya maudhui ambayo yamehimiliwa na dhamira kuu ya mwandishi wa *Pango*.

Kwa mujibu wa Lukacs, dhamira katika fasihi lengo, kusudi na madhumuni ndiyo yanayomwongoza mwanafasihi kuyaangazia maswala yote yanayoiathiri jamii. Kwa hivyo kuyashughulikia ili kuhamasisha na kuzindua wanajamii, kuhusu makosa wayafanyayo ya kuhidhalilisha jinsia moja na kuinua jinsia nyingine kwa wakati mmoja. Kwake yeye viumbe wote wana sauti na iweje mwanamke ambaye ni binadamu kamili kutokuwa na sauti ya kusikizwa, wivu na taasubi za kiume miongoni mwa wanaume ndio chanzo cha daima kumnyamazisha mwanamke asije akaongoza jamii iliyokuzwa kwa mikatale na miiko ya mwanamke kuongoza.

Beauvior (1969), anafafanua hali ambapo wanawake wengi wamefungwa katika tamaduni ambazo zimekuwa ngome za nafsi za kuwanyamazisha. Wanawake kujikomboa kimawazo na kiakili, kupaza sauti kujikomboa na maonevu ya jamii imekuwa vigumu. Katika jamii ya pango mhusika mkuu, Katango ameumbwa kama mwanamke anayejikuta katika njia panda ya kuathiriwa na utamaduni ulioko, unaompa mwanamume sauti mbele ya watu na mwanamke hana licha ya kuwa na nia nzuri yenye manufaa kwa jamii nzima. Anapopaza sauti inakuwa ni kelele za chura ambazo hazimzui tembo kunywa maji. Babake Katango haamini kwamba bintiye anaweza kuwa kiongozi wa kuitetea na kulinda 'pango', kwake Katango anapoteza muda wake, babake hamuungi mkono. Anayemunga mkono ni babu yake tu, ndiye alimtia moyo na kumwambia asikate tamaa mabadiliko yatafanyika siku moja.

> SEKI*:* *(Kwa sauti ya juu)* Unajua kichwa cha nyoka
> hakistahimili kilemba wewe? Ndiyo huo usasa
> wenu umekupa kiburi cha kuinua kichwa
> na kukigotesha jabalini chini kama
> mjusi?...Hujasikia lakini kuwa kuna majabali
> yasiyokwewa na mijusi wewe? (uk. 20)

Ngwese naye anasema kwamba hajapata kusikia kwamba mwanamke ni mlinzi wa 'pango' na kwa vyovyote vile uongozi utasalia kwa nyumba yao, babu yake alikuwa mlinzi na familia ya kina Katango wakamwonea wivu lakini sasa Ngwese hataruhusu tena mwanamke kuongoza. Katango anapoteza muda wake bure yapaswa aolewe, apate mume wa kumtia adabu. Kauli hii inamsawiri mwanamke kama miliki ya mwanaume na kumfanya mwanamke kuwa chini ya mumewe kuadhibiwa atakapoonekana kupaza sauti ama kunung`unika.

> NGWESE: ...Nitakupapata makofi wewe.
> Naona... Unatakiwa kuolewa,
> utiwe adabu na mumeo! (uk. 14)

Fikra hizi za kibinafsi walizonazo wanaume zimechangia sana katika kuendeleza uonevu kwa wanawake kama viumbe wasio na sauti katika jambo lolote kwa kuweka maslahi yao mbele. Ubinafsi wa wanaume ya kujali maslahi yao bali si ya jinsia zote huondoa ushikamano wa watu, ndiposa kampeni za Katango kuambulia patupu. Katango anaathiriwa kiasi kwamba hapewi nafasi ya kuongoza na nia yake nzuri haifui dafu. Anayepewa jukumu la kulinda 'pango' ni kinaya kwa sababu ni mwizi mkuu – Ngwese. Kupagazwa mlinzi wa 'pango' huku akiliibia 'pango' la wanajamii

kwa manufaa yake na ya wachache wanafiki kama yeye. Ndio maana Lukacs (1963:24) anatoa rai kwamba wanawake wasidunishwe bali wapewe nafasi sawa na wanaume katika nyadhifa na kazi mbali mbali kwa kuwa wanaweza.

### 3.3 Nafasi Chanya Anayopewa Kiongozi Mwanamke

Mwandishi anaangazia uwezo na mchango muhimu wa kiongozi mwanamke katika ujenzi wa jamii mpya. Zaidi ya kuonyesha taswira chanya anadhihirisha uwezo na nguvu ambazo zikiimarishwa zitakuwa msingi muhimu katika jamii yenyewe, kwamba zitahakikisha usawa na haki kwa jinsia zote mbili. Hili ni jambo linaloangaziwa vyema.Kama njia mojawapo ya kusisitiza haja ya kumkomboa mwanamke katika jamii, amemwumba mwanamke jasiri, huru na mlezi mwema . Akamfanya mhusika mkuu. Huyu ni Lanina anayetumika kama kielelezo cha harakati za ukombozi wa mwanamke katika jamii inayotawaliwa na mfumo wa kiume. Anafanya hivyo kwa nia ya kuitafakarisha jamii razini na hasa wanawake kuhusu haja na namna ya kujinyakulia ukombozi wao.

Wafeministi watukuka wanatoa pendekezo kuhusu suala la kijinsia, kwamba wanawake kwa wanaume wanastahili kujitahidi kwa ushirikiano katika kupiga vita ubabe dume katika jamii. Wanaeleza kwamba maumbile hayawezi kubadilishwa lakini mfumo unaweza kubadilishwa kwa sababu ni tokeo la jamii, mazoea na desturi. Kwao jamii inaweza kubadili mfumo ulioanzishwa na wanajamii wenyewe.

Kwa maoni yao, kile kilichoanzishwa na jamii kinaweza kubadilishwa na jamii iyo hiyo. Mwandishi Mazrui ametumia mwanamke kama mhusika mkuu kumwinua kihadhi na kuizindua jamii kuhusu haja ya kutambua mchango muhimu wa mwanmke. Nafasi anayompa Lanina tamthiliani inalenga kudhihirisha kuwa jamii itafaulu kubadili mkondo wa mambo endapo wanawake na wanyonge watajasiria na kupinga mazoea na desturi zinazowakandamiza.

#### 3.3.1 Mwanamke kama Kiongozi Jasiri

Ni bayanakama mlango wa kanisa kwamba, tamthilia hii ya *Kilio cha Haki* imemsawiri mwanamke kama kiongozi ambaye ni jasiri anayestahimili changamoto zote za jamii ambazo hazimthamini mwanamke kama kiongozi. Katika jamii hii utamaduni umewafunza wakazi wake kuwa mkia hauwezi ukaongoza kichwa ndiposa wanaume hawathamini uongozi wa wanawake kamwe. Ni katika changamoto hizi ndipo A. Mazrui anamuinua hadhi mhusika wake mkuu Lanina na kumsawiri kama

kiongozi jasiri asiyeshawishika rahisi na nia yake ni kupigania haki za wafanyikazi jambo ambalo wanaume wanashindwa kulitekeleza. Dewe na Musa wametoroka nyumbani kwa kuwa hawana ujasiri wa kukabiliana na hali iliyo nyumbani. Wao ndio waliokuwepo siku ile ya mgomo na wana hakika kwamba Lanina hakuwepo siku iyo ya mgomo lakini wametoroka nyumbani hawapo kusimama kidete kumtetea Lanina. Kwa upande mwingine Lanina anatiwa mbaroni na kupelekwa mahakamani kwa kisingizio cha kuchochea mgomo uliosababisha mauaji ya manokoa watatu wa shamba la Delamon. Ni kupitia ujasiri huu wa Lanina kusimama kidete kupigania haki za wafanyikazi na hasa kupitia uzindushi waliopata kutokana na mzee mkongwe aliyepita walipokuwa wanapiga gumzo katika shairi lake:

MZEE: Kwa nini ewe bara la afrika
Ewe tamaa ya mtu mweusi
Ewe mashiko ya maisha yetu
Aliyeeneza mbegu za rangi huko duniani
Zikizaana katika uzao wa ulaini
Nijibu…
Kwa nini ungali ukinichoma moyoni
Kwa mahaba ya kifani?
Kwa nini ungali mpenzi wangu
Katika saa hii ya huzuni?
Kwa nini? (uk. 5)

Kauli hii inamzindua Dewe anayeona thamani ya Afrika ndiposa wanagundua kwamba walikosea kutoroka.Wanaona Lanina ana juhudi muhimu katika kupigania haki za wafanyikazi.

DEWE: Tumefanya makosa kutoroka nyumbani
Ni lazima turudi
Kichini chini ni lazima tuanze
kuwaamsha wafanyikazi wenzetu
Kichini chini ni lazima tuiendeleze kazi ya Lanina
Turudi Musa! Turudi nyumbani.

MUSA: Sasa umesema ndugu!
Huu ndio mwanzo wa mwanzo
Huku ndiko kuzaliwa kupya
Twende ndugu! twende…(uk. 6)

Ni kupitia kwa uongozi wa Lanina ndiposa Dewe na Musa wanaona kuwa wazi ujasiri wa kiongozi wao katika kupigania haki za wafanyikazi wote. Lanina anasimama tisti na kuzikabili hali mbalimbali kwa ukakamavu bila kukata tamaa. Lanina anapoletwa

mbele ya Kaburu wa shamba Bwana Delamon anazabwa makofi na askari hata hivyo hiyo haizimi azma yake ya kuwa jasiri. Anageuka polepole na kumtazama Delamon na kumkabili na maswali mawili mazito.

LANINA: Hili ndilo ulilotuitia Bwana Delamon?
kutaka kujua malalamiko yetu? (uk. 14)

Tunamwona Lanina kama kiongozi shupavu hatetereki katika hali zozote ngumu zinazomkabili. Beauvoir (1949: 737) anafichua pingamizi zinazokwamiza ufanisi kwa kumkomboa mwanamke. Mojawapo ni mwanamke mwenye kuangalia nyuma kimaisha, kwamba wanawake watazame mbele na kujikaza vilivyo. Lanina anaonekana kufanya hivyo kwani anasabilia kuvunja "desturi na mazoea" katika jamii inayotawaliwa naubabe dume. Anajitokeza kuwa kielelezo cha vita dhidi ya uhafidhina na mazoea.

Kwa mfano Lanina na Tereki wanapokuwa na miadi na Delamon yeye ndiye mwanamke pekee kati ya wanaume wawakilishi, na licha ya utamaduni kumfanya mwanamke asiwe na sauti mbele ya wanaume. Lanina anamsemeakwa ujasiri mwingi na taswira tunayoipata hapa ni kuwa Lanina kama mwanamke wa kisasa aliyejikomboa kiakili si mwanamke mwoga tena. Anamsihi Tereki asitilie maanani uongo wa kina Delamon wa unafiki, kuwaambia wamejitolea kuja kusaidia maendeleo ya nchi na kuwanufaisha waafrika kwa kuwapa kazi. Na kwa ujasiri anamwambia Delamon kuwa hawakuja kwa maendeleo ya nchi yao bali wamekuja kwa maslahi yao.

LANINA: Wacha kuutilia nguvu uongo wao huo.
Nyinyi hamkuja hapa kwa manufaa yetu
Hamkuja hapa kwa maendeleo ya nchi yetu
Mmekuja kutudhulumu tu.
Kutumia nguvu zetu.
Kutunyang'anya ardhi yetu.
Kuinyonya nchi yetu
Kwa gharama ndogo isiyokuwa na thamani. (uk. 13)

Tamthilia hii ya *Sudana* imemsawiri mwanamke kama kiongozi ambaye ni jasiri anayezikabili changamoto mbali mbali katikajamii ambazo hazimthamini mwanamke kama kiongozi kwenye jamii hii utamaduni umewafunza wakazi wake kuwa mkia hauwezi ukaongoza kichwa ndiposa wanaume hawathamini uongozi wa wanawake kamwe. Ni katika changamoto hizi ndipo waandishi hawa wanamuinua hadhi

mhusika wao mkuu sudana na kumsawiri kama kiongozi jasiri asiyeshawishika rahisi na nia yake ni kupigania haki za wanawe jambo ambalo wanaume wanashindwa kulitekeleza.

> SUDANA: (Kwa hasira) Usiniguse! ... Hayawani we!
> Usijaribu wewe kuniguse mie! (uk. 37)

Sudana anadhihirisha ujasiri kwa kiwango cha hali ya juu hapa. Amerigo anapojaribu kumkaribia ili kuyatimiza mahitaji yake ya kimwili, tunamwona akimwonya kwa ukali bila woga wowote. Ingawa yeye ni mateka wa huyu nahodha, haogopi kamwe. Waandishi wamemchora hivi kwa sababu ya utamaduni kuchora mtu wa jinsia ya kike aliyekosa ujasiri. Katika juhudi zake za kukosoa madhila ya Amerigo kubomoa meli yao na kutumia mbao zao kuzibia meli yao, Sudana anawapa wanawe matumaini kwa kutongoa shairi lifuatalo:

SUDANA: ...

> Na yote haya
> Ngarawa hii uionayo
> Imeshakumbana nayo
> Bila kufa moyo!(uk. 26)

> SUDANA: Nimejifunza kutokubali maafikiano mepesi
> yanayozidisha udhalili wangu, yanayobadilisha
> ushenzi wetu wa kibinadamu kwa ushenzi wenu
> wa kinyama! (uk. 42)

Kama kiongozi jasiri hakubali kamwe mateso wanayopitia wanawe, hasa Shume anapofungwa kamba na kuchapwa hadi kufa. Ukatili wao ni sawa na wanyama wa msiuni. Wanamuua mwanawe akiangalia. Haya yanatekelezwa na askari wa Amerigo ili Sudana akubali kuwa kahaba.

Waandishi wamemsawiri Sudana kama kiongozi jasiri anapomenyana na Amerigo pindi tu Amerigo anapomrukia ili ambake. *Anauchomoa upanga na kumkabili Amerigo* (uk.27). makabiliano haya yalitokea kwa sababu ya kujitahidi kuwatetea wanawe dhidi ya kazi nyingi na mateso kutoka kwa Amerigo na Muzungu walio manahodha wamerope, ilhali aila ya Sudana ni ya wazanji.

Katika tamthilia ya *Posa za Bikisiwa*, mhusika wa kiume Sogoramaneno anajaribu kumsifu Bikisiwa kwa lugha na maneno matamu, kweli hayawezi kumtoa nyoka pangoni. Licha ya kumtongolea misemo ya sifa, Bikisiwa haridhiki na maneno haya

na badala yake. Anamkataza kwa ukali, *Hongera za nini? Sema unataka nini*? (uk. 55). Bila shaka Bikisiwa anajua nia kuu ni kumuoa atekeleze mambo kitamaduni. Bikisiwa sasa ni mpya aliyejaa ujasiri na anayekataa mbinu za kuolewa za kuposwa.

> MTAMBAJI: Hapana sasa Bikisiwa ndiye aliye mbele yenu.
> Ndiye anayeongoza. (uk. 67)

Waandishi wamemchora Bikisiwa kuwa mpya aliye na mbinu ya utandawazi akilini. Anayajua yaliyo muhimu kwa maisha yake na hana budi kuyapigania. Wote kama Mpitanjia na Mtambaji wanajua yeye ndiye atakayewaongoza ili wapate usawa na haki. Jane na Cecilia wanajua wataepuka madhila ya ubakaji kwa kufuata wosia wa Bikisiwa.

Katika tamthilia ya *Pango*, jamii nyingi za kiafrika pana pingamizi tele zinazokwamiza ukombozi wa mwanamke. Mojawapo ni mwanamke mwenyewe kuangalia ‘nyuma’kimaisha. Ni vyema iwapo wanawake watatazama mbele na kujikaza vilivyo. Katango anaonekana kufanya hivyo kwani anasabilia kuvunja desturi na mazoea yaliyo kwenye jamii yake. Anajitokeza kuwa kielelezo cha kupiga vita uhafidhina na mazoea. Katango anasimama tisti na kuzikabili hali mbalimbali kwa ukakamavu bila kukata tamaa.

Katango anadhihirisha kiwango kikubwa cha ujasiri kwani anajitolea kwa vyovyote vile kumpinga Ngwese mwanaume kwenye kinyang`anyiro cha kumchagua mlinzi wa ‘pango’, Katango anakabili vitu vingi kwa ujasiri ili kupata nguvu za kuendelea kuwania nafasi ya ulinzi wa pango.

> KATANGO*: (Mshangao)* Utamaduni? Utamaduni gani huo?

> SEKI: Utamaduni gani huo? Umesikia wapi wewe
> mwanamke ameshika mata na mishale katika jamii hii.
> ...hiyo elimu ya kizungu ndiyo iliyokupa ujasiri
> wa kuipuuza mila? (uk. 18)

Tunamwona Katango akiookota uta na mishale kinyume na mila na desturi za jamii ya pango. Ni kosa na miiko kwani mwanamke hapaswi kushika ala za vita ni jambo ambalo halifanywi na wanawake na kitendo kama hicho kwa mujibu wa baba yake na ni jambo linaloweza kuleta nuksi kwa jamii yao. Kwa mujibu wa Ngwese ambaye pia ni mgombea mwenza katika nafasi ya kulilinda ‘pango’ anadai kwamba Katango ni

mwanamke ambaye anapaswa kuolewa na kutiwa adabu na mumewe kwa kuwa anaonekana hana adabu.

Kwa Katango haya ni madharau na matusi kwani kuokota uta na mishale hakuna ubaya wowote ndio maana anamjibu babake kwa ujasiri kwamba hakuna nuhusi yoyote ambayo yaweza kutokea kwa kuokota uta na mishale ni mbinu tu walizonazo wanaume ambazo wamezifungamanisha kwa utamaduni ili kuwazuia wanawake kutokuwa walinzi wa 'pango'.

> MBABEKAZI: Ndiyo lakini...jamii inawadharau wanawake.
>
> KATANGO: Hamna neno mradi wenyewe hatujidharau...wakati unapita. (uk. 27)

Katango anazidi kudhihirisha ujasiri anapokumbana na pingamizi anapofika mkahawani wanaume wanamsengenya kwamba hafai kuwa mlinda 'pango'. Lake ni wosia wa busara, wanawake wasijidharau bali wawe na ujasiri uongozi wataupata.

> KIKUBI*: (Akidakiza)* Ehh, Katango jiwe la mango amchezeaye huvunjwa maungo! (uk. 39)

Mwandishi amemsawiri kiongozi huyu kama aliye na nguvu na staha ya kuliongoza pango. Kampeni za kuwania uongozi zinamsifu Katango kama shupavu na chaguo la kizazi cha sasa. Wanaohudhuria siasa zake ni wa umri wote hata mzee Ngoi ana ndoto ya Katango kuzua uongozi mpya na bali sio ule wa jadi uliojaa maovu.

Katango ni kiongozi wa jamii ambaye amezinduliwa na elimu. Lengo lake kuu kutaka kuliongoza pango ni pawe na usawa wa haki na kijinsia. Jamii yake inaenzi mila na desturi sana. Utamaduni umewafunza kuwa uongozi ni wa wanaume. Hata vijana wenzake hawana imani kuwa jamii itakubali alilinde pango – awe kiongozi. Tashwishi hii ndiyo inapelekea rafiki yake kumdadisi kwa maswali:

> MBABEKAZI: Watu wataukubali uongozi wa vijana ... na tena awe mwanamke?(uk. 27)
>
> KATANGO: *(Kwa mshangao*) Mwanamke ana nini, anaweza kuongoza? Mwanamke nguzo...(uk. 27)

Kama kiongozi mkakamavu na mwenye kulenga, Katango ana imani ya ujenzi wa jamii mpya. Anamkumbusha rafikiye kuwa, mwanamke kama binadamu yeyote yule anaweza kuwa kiongozi. Kama nyumba yoyote ile, uongozi wa wanawake ni kama

‘nguzo’ zilizo muhimu ili nyumba iwe imekamilika thabiti. Wanawake wamekuwa viongozi wa nchi nyingi ulimenguni kutoka marais, waziri wakuu, maaziri na hata mabalozi. Vijana wamezinduka kuwa viongozi kwa kupigania haki hii. Kwa mujibu wa Kibwana na wenzake walio vijana wakati umebadilika sasa:

KIBWANA: Upepo umebadili majira, haya ni mengine majira
kale iliyokuwako imechwewa na jua
jua la kufahamu limetuchea, vijana!!
Hatutishwi na kupigwa kabari ii! (uk. 36)

Utamaduni umekuwepo tangu jadi. Hata leo unaenziwa ingawa kwa viwango lengwa. Nchi nyingi zimeendelea kiuchumi, kisaikolojia, kielimu na kidini. Sekta kama siasa zimebadilika pakubwa. Haki na usawa limekuwa azimio ya mataifa mengi kwa raia wake wote. Tunawaona vijana wakikubaliana na Katango kuwa muda umefika wa kubadili uongozi. Hata vijana wanaweza kuongoza. Mbali na maovu na madhila pana nia ya ujenzi wa jamii mpya itakayoongozwa na Katango.

KATANGO: ...*(Mtuo)*
Sasa macho tumeyafungua
Sasa upofu tumeupofua
Sasa vinywa tumevifungua
Maovu nayo umeyafukua. (uk. 87)

Kufikia mwisho wa tamthilia, mwandishi ameonyesha ufanisi wa vita dhidi ya ukosefu wa haki na jinsia. Wananchi wa jamii ya pango wanatambua ukweli. Ngwese anagunduliwa na sifa za uongo, ufisadi na uongozi mbaya. Askari wanaingia na kundi la vijana na kumkamata Ngwese.

### 3.3.2 Mwanamke kama Mlezi Mwema.

Mwandishi amesawiri mwanamke kama mlezi mwema. Lanina anapokuwa kizuizini, Mwengo anapata changamoto kuwalea watoto peke yake. Anakuwa kama mtu asiyejiweza.

MWENGO: Lanina! Lanina!
Wewe wajua siku ngapi sasa umeniweka bila ya usingizi
Unajua siku ngapi sasa watoto wanakula chakula kibichi
…

MWENGO: Angalia! Angalia namna gani watoto wanataabika.
Angalia majonzi na shida zao!
Halafu ati unajiita mama yao! (uk. 30)

Kupitia kwa maneno haya, Mwengo anaungama kuwa kazi ya kuwalea wanawe si kazi yake. Utamaduni umemfunza kwamba kazi ya kuwalea, kuwapikia, kuwaosha watoto ni kazi ya wanawake. Mwengo amemchukulia Lanina kama chombo chake kabisa cha kumhudumia daima.

Mwanamke pia ametwikwa jukumu la kuwafunza watoto maadili mema. Babake Lanina anamwambia mke wake kuwa binti yake amekuja amfunze adabu na aukomeshe ubabe dume wake. Yeye kama baba anaona wajibu wa kumfunza maadili mema binti yao Lanina ni wa mamake Lanina.

BABA: Haya jitoto lako limefika sasa.
Kaa nalo ulifunze adabu na heshima
Ulifunze maana ya uuke.!
Uukomeshe huo udume wake.
Umesikia hivyo.(uk. 38)

### 3.3.3 Mwanamke kama Mtu Mwerevu na Mwenye Akili Tambuzi

Mwanamke ni mtu mwerevu mwenye akili tambuzi kutokana na yale anayosema na anayofanya. Lanina anadhihirisha wazi utambuzi wa haki na usawa.

Lanina anafaulu kujikomboa na kuwaamsha wenzake. Mapambano ya kuubomoa ukoloni yanaanza kwa sababu ya uongozi wake thabiti. Wafuasi wake wengi ni wafanyakazi. Yeye ni kiongozi wa wana-mapinduzi. Maisha yake yanatawaliwa na hali halisi ya maisha na fikra yake inafuata mantiki, ilibidi atambue ukweli wa hali inayomzunguka na kuona haja ya mabadiliko. Lanina anaonyesha kuendelea kupevuka kwa akili na mawazo kadiri mazingira yanavyoendelea kumfinyanga na kumlea.

LANINA: Ndiyo! Kweli siasa ni mchezo mchafu.
Na ndiyo lazima sasa tuusafishe…
Ikiwa ulimi umeweza kuwa kisu cha kuulia,
hauwezi kuwa sabuni ya kusafishia? (uk. 40)

Harakati za ukombozi huwa na gharama kuu. Lanina amepigania haki na usawa wa wafanyakazi ili kuijenga jamii mpya. Bila shaka huenda mafanikio yaliwafika wote kwa sababu ya akili na werevu wa Lanina. Migomo, maandamano, matusi na

dhuluma hazikuwa juhudi za kupoteza muda bali mbinu mbali mbali zilizofaa kulilia haki kutendeka.

Katika tamthilia ya Posa zaBikisiwa, waandishi wamebainisha nafasi chanya ya kiongozi mwanamke katika jamii na athari za kiongozi huyu kwao mwanamke ni mtu mwerevu na mwenye akili tambuzi. Kutokana na yale anayoyasema na anayoyafanya mwanamke anaonyeshwa kwamba wametekwa nyara na tamaa ya vitu vya thamani vinavyowafanya kuwa bora au kuonekana kama wanaiweza kwenye ushindani na mapambo na mavazi kiasi kwamba hawajajikomboa kiakili. Desturi za kike zinawagubika na kuwafanya wasitosheke kiuchumi katika maisha yao. Hili tunaliona likishughulikiwa na waandishi hawa;

> BIKISIWA: Wewe mama u kama mimi. Sisi ni wanawake.
> Wanaume wanadhani sisi hatuna maana. Hatuna akili.
> Sisi wajinga. Ni watu wa chini tu. ...posa yetu na
> Sogoramaneno haiwezi kuendelea. Hii ni posa ambayo
> tokea mwanzo haikuwa ya halali. Ya halali haikuwa.
> Ni ndoto ambayo daima haitatimia. Ni uhusiano
> uliojaa mizaha na tuhuma. Inayopuliziwa
> na wasiotutakia mema. Siko tayari kuingia ndani naye.
> (uk. 21)

Umaizi wa haki na vita kupata usawa unamweka Bikisiwa katika orodha ya wanaharakati wakuu wa ufeministi. Usawa na haki haiji ila kwa ncha ya upanga. Bikisiwa anamsimulia mama yake, Malkia yaliyo rohoni mwake. Hii ni picha mahsusi ya mwanamapinduzi anayepigania haki zake kama kiongozi. Vishawishi hivi vya mapambo, dhahabu na hata pesa havimwathiri kwa vyovyote Bikisiwa.

> BIKISIWA MPYA: Upepo unaovuma
> Lete habari za mbali...
> Upepo!
> Ushindi gani?
> Ushindi wa nini?...
> Umetoka ... kuniambia upuuzi huu?
> (uk. 54-55)

Waandishi wamemchora kama mtu anayewaza na mtambuzi wa mambo. Amewakilisha nafsi za wanawake wengi wanaolazimishiwa waume kwa kuposwa. Amekataa katakata na kufaulu kutowaruhusu waingie moyoni mwake. Bikisiwa yu huru kujichagulia mume anayemtaka... Bila woga wowote anamshambulia

Sogoramaneno kwa maswali ambayo yanamwacha kinywa wazi. Nia kuu ya Sogoramaneno ni kumdhibiti na kumwoa, jambo ambalo Bikisiwa analikataa kamwe.

> SOGORAMANENO: Kwa nini lakini Bikisiwa unanidharau? Tena
> unanidharau vibaya kuniona kama ushuzi.
> Kitu kinachopita tena kwa kunuka. (uk. 57)

Bikisiwa amemchora na kumfanya Sogoramaneno kutambua kuwa utamaduni wa kitambo hauna mashiko karne hii. Ndoa ya kuozwa na wazazi zimepitwa na wakati na zinakiuka haki za anayehusika.

> BIKISIWA MPYA: ...Usisahau kwamba umesema
> utanipiga mwereka na kuniiba kunipeleka
> nyumbani kwako pindi nikikataa –
> tuko katika karne gani Bwana
> Sogoramaneno? (uk. 58)

Sogoramaneno anadhani kuwa mbinu ambazo angezitumia kujipatia mkea hazijulikani. Kwa mshangao mkuu Bikisiwa anamdokezea jambo ambalo linamwatua roho na kufanya mipango yake kufeli zaidi, kumuoa kwa nguvu.

Kiongozi wa kike katika tamthilia hii ya Sudana ameweza kuchorwa na kusawiriwa kama mtu mwenye msimamo imara katika uamuzi wake. Sudana amesawiriwa kama mwanamke ambaye ana msimamo imara na ambaye kwa vyovyote vile habadili msimamo wake

Sudana licha ya kuwa na mimba haramu na licha ya kushauriwa na watoto wake kuavya ile mimba, anamua kumlea Sudzungu ambaye baadaye anamletea mikosi kwa maisha yake. Sudzungu anageuka kuwa gawadi wa mamake na kutaka kuwa fuska wa Amerigo ili kupata hela. Anamtumia mamake kama kitega uchumi kwa kumuuza kwa Amerigo. Sudana anasononeka, Sudzungu ambaye ni mwanaye anamwambia *awache ujinga na akubalimatakwa ya Amerigo* (uk. 22). Lakini Sudana anajidhihirisha kuwa na msimamo thabiti licha ya kutoneshwa kidonda na Sudzungu ambaye ni mwana wa haramu anazidi kumkubali kama mwanawe.

> SUDANA: we! usizoee tena kuniita ‘mwanamke’ mtovu
> wa nidhamu we! Usisahau katu kwamba
> mimi ni mamako, kwamba mimi ni mamayo;
> kwamba wewe ni mwanangu ingawa
> kwa mimba ya haramu hebu jaribu

kumbuka Sudzungu mtoto wangu! (uk. 23)

Sudana anazidi kujidhihirisha kama mwenye msimamo thabiti anapomwambia Sudzungu kuwa, amemruzuku hadi akawa shababi kwa maziwa yake na hayo ni marupurupu tosha. *kutokana na mwili wangu huu mwili wako umejengeka na kutokana na mwili wangu huuumepata mahitaji yako yote ya utu uzima* na hauwezi kuiuza nafsi yake kumbembejea mwanaume kwa sababu ya pesa. Sudana anataka kuwalea watoto wake kwa upendo na amani. Amerigo pia anakiri kuwa Sudana ana msimamo thabiti kwa kuwa anaungama kuwa Sudana amekataa kuafikiana naye:

AMERIGO: Unaona kipenzi changu, kama tungeafikiana
tangu awali haya yote hayangekuwa,
ushenzi wa wanao ningeweza kuurekebisha
kwa njia sahali zaidi, njia za mafunzo
na malezi nia yangu ni nzuri nyie ndio
hamnifahamu. Ni maafikiano tu. (uk. 42)

Sudana anazidi kuwa na msimamo thabiti kiasi kwamba amekataa katakata kuwa kahaba wa Amerigo, hata baada ya Sizwe mwanaye kuuwawa. Amerigo hatimaye anamzaba kofi Sudana na kumwangusha naye Sudana hampi ruhusa ya kumvua nguo na kumbusu anampiga teke na kumrukia kujaribu kumtia makucha (uk. 38)

Katika tamthilia ya *Pango,* Katango amesoma na kuhitimu kuwa mwalimu. Katika jamii nyingi za kiafrika, mwalimu huwa anaheshimiwa na kuenziwa na wote kwa kazi yake. Mawaidha na maelekezo ya mwalimu hudhaminiwa sana.

NGWESE:...labda babako anaistahi elimu yako
lakini kwangu awe na elimu au la
mwanamke ni mwanamke tu! (uk. 10)

Kwa mujibu wa Ngwese, elimu ya mwanamke haithamini. Mwandishi amemchora Ngwese kama mkatili na asiyewaheshimu wanawake. Wanawake kwake ni jinsia duni awe na kisomo au asiye na kisomo.

Jamii ya ‘pango’ haithamini elimu ya mwana wa kike. Iwapo amesoma huwa ni kama laana. Mwanamke yeyote aliyesoma hudhaniwa kaasi tamaduni za jamii husika. Jamii inafaa kumtenga naye kwa sababu ameathirika na usasa, kasumba ya ukoloni. Katango, aliye mwalimu haheshimiwi na wanajamii wake hata wazazi wake. Kauli zake za mtu aliyezinduka kielimu zinapingwa na wote. Usasa humfanya mtu

kusahau hata mila na desturi za jamii yake. Tunamwona mzee Ngwese akimkemea na kusema haya anapomkataza Katango kuwa kamwe hatakuwa kiongozi.

NGWESE: ...Hiyo elimu ya jamii naona imekuzuzua
mpaka historia ya jamii... (uk. 11)

Ngwese anawatuma wahuni kumchapa Katango. Hii ni mbinu inayotumika katika nchi nyingi za kiafrika kuwanyamazisha wapinzani wa kisiasa. tunamwaona Katango akishambuliwa na kuumizwa na watu wawili –Mtu I na Mtu II.

MTU II:..Ni nini kikupacho kiburi sasa eeh!
au ni hiyo elimu yako? ...Mwanamke,
... Unadhani tumewaona wangapi? (uk. 32)

Mwandishi amewachora wanaume katika jamii hii kama wakandamizaji na wahuni. Wanatumiwa na wanasiasa kama Ngwese kudhihirisha ukosefu wa haki na usawa wa jinsia katika jamii ya 'pango'.

### 3.3.4 Mwanamke Msanii wa Lugha

Kipawa cha usanii kimedhihirika wazi katika tamthilia ya *Posa za Bikisiwa*. Bikisiwa ni msanii mtukuka aliyebobea katika lugha jinsi alivyochorwa na waandishi hawa.

*BIKISIWA: ...Tangu lini wingu lisilo na mvua likanyesha? (uk. 21)*

Hapa usanii unatumika kuelezea uhusiano uliopo ambao hauna upendo. Mfalme amemposa bintiye Sogoramaneno, asiyempenda. Methali hii ni mbinu mojawapo ya usanii inayotumika sana na huwa na maana fiche.

BIKISIWA: ...Hujui kuwa nyumba nzuri si mlango? (uk. 38)

Waandishi wamempa mhusika mkuu mbinu hii ya usanii kwa mujibu wa suala nzito la ndoa. Mwanamume SS naye anataka kumuoa Bikisiwa. SS anakuja kumwomba Bikisiwa amkubali amuoe. SS ndiye anawasaidia kuwafukuza adui wanapovamia himaya ya mfalme, baba yake Bikisiwa. Hata hivyo, penzi halioti rohoni mwa Bikisiwa kwa SS. Juhudi za SS kumtongoza zinaambulia patupu. Ndiposa methali hii ikafaa hapa.

katika tamthilia ya *Pango,*

KATANGO: Pwagu hupata wa kumpwagua! (uk. 11)

‘Pwagu’ hapa ni Ngwese. Ametumia methali hii ili kumtatiza Ngwese kisaikolojia. Ngwese hathamini uongozi wa Katango. Katango anamjuza kwa ujasiri kuwa, kipindi hiki amepata wa kumpwagua. Lazima pango lilindwe na kwa ukweli na heshima. Muda wa kubadili uongozi umewadia. Hili linamjaza Ngwese uhasama sana. Katngo wanapokuwa kwenye kampeni za kisiasa, kila mgombeaji anapewa muda wa kuwahutubia wananchi. Katango anatumia mafumbo yafuatayo:

> KATANGO: ...Ametanguliza mwenzangu
> Jua la mti linapoipita adhuhuri ya maisha
> Mzee hashiki mata kwenda vitani
> Anarudi zake nyumbani... (uk. 41)

Ngwese ni mkubwa kwa umri. Kipindi cha uongozi wake kimefika mwisho. Zamu sasa kwa mujibu wa mwandishi, ni ya vijana. Ngwese hawezi kuwinda jioni. Wakati umewadia wa kurejea kwake na kuona jinsi vijana wataongoza. Katango anatongoa hadithi inayosimulia maovu ya Ngwese kwa wanajamii anaofaa kuwaongoza kwa utangamano.

> KATANGO: Hapo zamani za kale wanyama
> waliishi pamoja kwa utaangamano, amani na
> udugu mkubwa. Hali hii ilikuwa shwari kabisa.
> Basi siku moja ukame ukaingia... (uk. 42)

Hali nzuri waliyoishi wanyama ni hali ya kale sana, amani na udugu. Lakini, chini ya uongozi wa Ngwese – ukame – kisima cha kuwasaidia wanakijiji maji, Ngwese anawakataza kina Susa na Sota wasipitie shambani mwake. Ngwese anamtusi na kumkandamiza Katango kwa sababu anampinga kisiasa.

### 3.4 Hitimisho

Katika sura hii tumeangazia kwa kina nafasi mbili alizopewa kiongozi wa kike. Nafasi dhalilishi na nafasi chanya katika tamthilia teule za utafiti huu. Katika sehemu ya kwanza, waandishi wamemsawiri kiongozi wa kike kwa namna ambayo amedhalilishwa na kudunishwa kwa kupewa nafasi chukivu.

Katika sehemu ya pili, waandishi wamemsawiri kiongozi wa kike kwa kulenga nafasi chanya anayopewa katika jamii yake. Wamefaulu kumjenga kihadhi na kuonyesha mwamko wa ujenzi wa jamii mpya iliyo na utetezi wa jinsia ya kike.

# SURA YA NNE

# ATHARI INAYOMKABILI KIONGOZI WA KIKE KATIKA TAMTHILIA TEULE ZA KISWAHILI

## 4.1 Utangulizi

Katika sura hii, tumetathmini athari inayomkabili kiongozi wa kike katika harakati za kujenga usawa wa jinsia katika jamii. Kwa muda sasa, kiongozi wa kike amejihusisha na harakati za kujiendeleza kisiasa na kiuchumi. Harakati zenyewe zimeendelezwa na wataalamu wa ufeministi na hususan wanawake. Hata hivyo, kama inavyodhihirika katika *Kilio cha Haki* (Mazrui:1981), *Pango* (Wamitila:2003), *Posa za Bikisiwa* (King'ei na Mohamed:2008) *na Sudana* (Mazrui na Njogu:2006), bado kuna changamoto kadhaa zinazomwathiri kiongozi wa kike. Tumezibainisha changamoto zenyewe kwa kuzigawa katika makundi mawili: asasi za kitamaduni; ndoa, mila na desturi na masuala ya kiuchumi yanayofafanua harakati za ukombozi.

## 4.2 Asasi za Kitamaduni

Kila jamii hapa barani Afrika ina utamaduni unaowaelekeza na kuwaongoza wanajamii na maisha yao. Asasi za kitamaduni zimeonekana na kujengeka kwa namna inayompendelea mwanamume na kumdunisha mwanamke. Wataalamu wa masuala ya ufeministi wanadadisi mtazamo hasi unaobainika wazi dhidi ya mwanamke. Wanahoji kwamba, utamaduni humkweza mwanamume na kumtweza mwanamke. Nao Pilcher na Imelda (2004), wanasema kuwa kuna ithibati tosha kuonyesha ugavi wa majukumu kulingana na jinsia ya mwanajamii. Tamaduni nyingi za kiafika zimegawia wanajamii majukumu kwa kufuata utaratibu maalumu. Kazi za mwamamume zinajulikana nazo za mwanamke zimebainika. Utamaduni umeonekana kukwamiza na kukinzana na harakati za usawa baina ya wanajamii. Asasi ya ndoa,mila na itikadi ndizo zimechorwa kutomshirikisha mwanamke katika maamuzi hasa uongozi.

### 4.2.1 Asasi ya Ndoa

Asasi ya ndoa ni mojawapo ya kitamaduni inayoendeleza ukandamizwaji wa wanawake. Asasi yenyewe imejengwa kwenye imani ya uwezo mkubwa alio nao mwanamume na kuishia kumwangalia mwanamke kama chombo tu. Dini inatilia mkazo itikadi ya kiume inayopatikana katika jamii nyingi. Inaipa nguvu tamaduni dhalilishi dhidi ya mwanamke kwa kuziwekea mihimili ya matamko ya kidini.

Kila mwanajamii hutamani kuheshimiwa, kusikilizwa na kupewa haki yake. Sawa na mume katika ndoa, mke huhitaji staha na heshima. Tofauti na maagizo ya dini, tamaduni nyingi za Kiafrika humtarajia mwanamke kumheshimu mume na kunyenyekea. Nafasi yake ni ya pili, chini ya mume wake. Ndoa au harusi inamtosa mwanamke katika hali chukivu. Kulingana na *(Greer*:1970), harusi hutamausha na kumfanya mwanamke kuwa mtumishi nyumbani anayemtegemea mwanamume.

Tuckwell na Moore (1975), wanasema kuwa wake katika ndoa hulazimika kunyenyekea mbele ya waume zao. Wanasema kuwa wake huwa na masuala yanayowahusu na huhitaji kushughulikiwa. Hata hivyo, wanawake wenyewe hulazimika kunyamaza. Hii ni kwa sababu ya kuogopa matokeo ya mjadala kama huo. Wanaeleza chanzo cha hali hii ni malezi. Mume huandaliwa kimalezi kuwa mdhibiti katika familia. Mke naye huandaliwa awe na unyenyekevu kwa mumewe. Utamaduni humfanya mwanamke kuogopa kuchukuliwa kuwa anayeasi na kupinga utaratibu wa jamii yao.

Hali hii inajidhihirisha wazi katika *Kilio cha Haki* (Mazrui:1981). Lanina ni mkewe Mwengo. Ni mwanaharakati wa kimapinduzi katika tamthilia hii. Mbali na kumhudumia mumewe bado tunamwona mume wake akilalamika. Mazrui anamchora mwanamke jasiri asiyevia kutekeleza lengo lake. Usawiri wa Lanina kama mhusika wa kimaono na mwenye msimamo mkali unamwezesha mwandishi kutuonyesha kiongozi mwanamke anayeweza kukabiliana na maudhi ya jamii yake.

Bali na kuwa mwanamke aliyeolewa, ni mwenye maono na aliyemakinika. Lanina yumo mbioni kujikomboa kutokana na mikatale ya kijamii na kiuchumi. Utamaduni huu umeshindiliwa hata akilini mwa wafanyakazi wanaotumainiwa kufahamu zaidi. Lanina anapokutana na wafanyakzi wenzake kwa mzee Ingeli, analalamika kuhusu wivu wa Mwengo. Anasema:

> Lanina: ... Mume wangu ... Mwengo ana wivu sana.
> Musa: Simlaumu! Hata mimi ningekuwa na wivu.
> Lanina: (*Acheka*) Hii ndiyo taabu ya wanaume. Maisha mnayafanya yawe machungu kwa wivu wenu wa kipumbavu. (*Dewe na Musa wanacheka kidogo*). (uk.59)

Tukiyachunguza maongezi ya wahusika hawa, tunaona ya kuwa maoni na imani za Lanina ni kadhia zilizobobea katika mkabala unaomwongoza kupinga nguvu zozote

zinazokinza utetezi wake wa utubora. Musa haoni wivu kuwa ni upungufu fulani wa hulka unaopaswa kufutiliwa mbali kutoka kwa mioyo ya wapiganiaji haki. Ni wazi kwamba Dewe na Musa hawana fununu yoyote kuhusu wadhifa wa uongozi alio nao Lanina. Mwengo naye ana wivu, hulka iliyo ndani mwa mume yeyote kwa mkewe. Asasi hii ya ndoa inatilia maanani itikadi ya mke kuwa miliki ya mume.

Katika tamthilia ya *Pango* (Wamitila:2003), Katango ni mwanamke kijana ambaye ni mwalimu. Ni kipaza sauti cha usasa katika jamii iliyojaa mila na itikadi kali. Jamii ya mhusika huyu inatilia mkazo jinsia ya kiume, jambo ambalo Katango analipinga kiharakati. Katango anazua mgogoro wa kiutamaduni baina ya ukale na usasa. Mhusika Ngwese anamkaripia Katango. Anasema:

> Ngwese: (Anajaribu kumsogea kwa hasira) Nitakupapata makofi wewe. Naona unanikosea adabu! Unatakiwa kuolewa, utiwe adabu na mumeo! ... Basi nitakunyamazisha mimi! ... (uk.14)

Tunatathmini kuwa, ndoa ndiyo asasi inayomdhibiti mwanamke hasa katika jamii nyingi za Kiafrika. Katango, aliye kijana na bado hajaolewa anakaripiwa na Ngwese aliye mwanamume mzee. Vijana wanataka kiongozi mpya. Mbali na kuwa Katango hajaolewa, hilo halifanyi wao kutomchagua kama kiongozi. Vijana hawataki kukandamizwa na kunyamazishwa. Baadaye Katango anaumizwa na majambazi. Tendo hilo la ukatili halizimi ndoto yake ya ujenzi wa jamii mpya. Katango anachaguliwa kuwa kiongozi na wakatili wanakamatwa na kushtakiwa kwa ufisadi wao. Tunamwona Katango akimjibu Ngwese akisema:

> Katango: ... Sauti ya kizazi kipya inaita
> Sauti ya wanawake waliokuwa mashujaa
> ... Sote tulikubaliana ... tulibebe gogo ...
> ... tulipagaza mabegani kwa kujitoea ...
> (uk.14)

Mwandishi amemsawiri hapa, kuwa mwanamke aliye jasiri na mkakamavu. Hafi moyo hata kama anatukanwa na kukandamizwa na itikadi kali. Lazima jamii mpya ijengwe. Naye kiongozi ambaye wamekubaliana lazima ajitoe mhanga. Wamekubali, jamii nzima vijana kwa wazee wenye maono wamemwona Katango kuwa kiongozi bora. Mbali na mwandishi kuzua mgogoro wa kiitikadi lugha teule ya jazanda. ‘gogo’ linamaanisha uongozi mpya, ni mzigo wa kujitwika na hawana budi kuubeba.

Katika tamthilia ya *Sudana* (Mazrui & Njogu: 2006), waandishi hawa wamemsawiri mhusika aliye kiongozi kama aliyelaaniwa na itikadi. Yumo mbioni kuwanusuru wanawe kutoka najisi. Kijazanda, Sudana ameonyesha jinsi bara la Afrika linavyonyofolewa kiuchumi na kunajisiwa na nchi za Magharibi na Mashariki.

Mahusiano kati ya Amerigo (Bara Marekani), Merope (Bara Uropa) na Sudana (Afrika) yanazua asasi ya ndoa haramu. Sudana ananajisiwa na Amerigo. Anasema:

> Amerigo: ... Aaah! Nimechoshwa na huo mdomo wako!
> (*Kichwa cha Sudana kinajigonga na kitanda. ... Anageuka kumtazama Sudana ambaye bado hana fahamu. ... Anaendelea kuvua nguo huku akimsogelea Sudana. ...* ) (uk. 44)

Ndoa haramu ya kulazimisha inazua zao ambalo ni kuzaliwa kwa mwanawe Sudana aitwaye Sudzungu. Sudzungu anatumika na waandishi kutuonyesha utamaduni mseto wa waafrika na wazungu. Ni mwanaharamu asiye na baba wa kiafrika. Ndoa iliyomzaa bila shaka haina heshima maana Sudana ananajisiwa wakati hana hata fahamu. Unyama ulioje na hili lina onyesha jinsi utamaduni unavyokandamiza jinsia ya kike.

Katika *Posa za Bikisiwa* (King'ei na Mohamed:2008), wamemhusisha kiongozi wa kike Bikisiwa. Bikisiwa ni mwana wa mfalme na Malkia. Bikisiwa amefikia umri wa kuolewa. Wanaomposa wana hulka mbalimbali. Wanafika kina Sogoramaneno wenye maneno ya kumsuta na kumuongoa, wengine walio na mali tele na hata zawadi na vitu vya thamani. Baadhi ya wanaotaka wamuoe wanafika katika kasri lao Bikisiwa.

> SS: Muhibu... mimi natamani nikuoe. Tujenge himaya yetu madhubuti.(uk.38)

SS anafika ili amrai Bikisiwa amuoe. Bikisiwa anakataa kauli zake. Kwa maneno ya kumuongoa, *Aaa, Bikisiwa wewe ni bingwa wa lugha. ...sifa zako nzuri zimepaa hadi kwetu jangwani. Huijui thamani yako. Janibu nyingi za huko ng'ambo zinajua thamani yako. Umejaa jamala la mvuto wa ajabu. Ndipo mimi nikaamua nilete posa.* (uk.38)

> CHACHI: ... wewe hutaolewa na mtu yeyote pia. Utaolewa na mimi mwenye uluwa. Mimi niliye karibu na ufalme... (uk.48)

Chachi naye anakuja kumposa Bikisiwa kwa kumuahidi mambo makuu makuu na ufalme. *Hatutakuwa na tatizo kukunyenyekea.* Mposaji huyu amevalia kifalme na ushawishi wake ni waungane ili waendeleze uchumi wa milki zao pamoja.

> SOGORAMANENO: Nataka tuungane mimi na wewe tuwe kitu kimoja,
> mume na mke kama chanda na pete. (uk.58)

Sogoramaneno naye anawasili kumposa Bikisiwa kwa maneno matamu. Wahusika hawa wana nia moja, ndoa. Lao ni wampate jiko wampose. Athari hii katika uhalisia ni bara la Afrika. Rodney (1972), anasema kuwa, nchi nyingi zinasutwa na mataifa ya magharibi na sasa hata mashariki kama Uchina. Thamani yetu ya malighafi na soko la bidhaa linatunyofoa na kutuuacha tukiwa maskini. Hata hivyo pana umaizi na ugunduzi wa kunyanganywa raslimali yetu. Waandishi wamefaulu kusawiri mwamko huu na Bikisiwa Mpya. Anasema:

> BIKISIWA MPYA: ...Atawezaje kugundua udhati na ukweli
> wa maneno anyoambiwa? Vipi kijana
> wa kiume kama wewe unaweza kuthibitisha
> uhitaji na usafi wa nia yako? Vipi anaweza
> kujua kwamba anayemkabili ni mtu au
> mnyama? Walii au shetani? Jambazi
> au msalihina? Usisahau kwamba
> umesema utanipiga mwereka na kuniiba
> na kunipeleka nyumbani kwako pindi
> nikikataa – tuko katika karne gani
> Bwana Sogoramaneno? (uk.58)

### 4.2.2 Mila na Itikadi

Utamaduni katika jamii aghalabu huongoza maisha ya wanajamii, matarajio yao na hata utendakazi wao kijamii. Mila na itikadi ndizo hujenga dini ya jamii husika. Ni mambo yanayoshiliwa ili kuendeleza msimamo wa kale. Ni hali inayozua uhafidhina, kupenda uasilia wa mambo kwa gharama yoyote ile. Wanajamii wanashikilia desturi za kikale na kutokubali mabadiliko na mambo mapya ya kisasa.

Maamuzi ya masuala ya kijamii katika jamii nyingi za Kiafrika aghalabu hutekelezwa na mwanamume. Mwanamume hupewa usukani na udhibiti wa maamuzi ya familia, jamii na maisha kwa ujumla. Mwanamke hashirikishwi. Wataalamu was Ufeministi wa tapo la Kiafrika wanahoji kimya cha kulazimishwa katika jamii. Wanasema kuwa mwanamke hata awe kiongozi, hulazimika kuitikia maamuzi ya mwanamume hata pale ambapo mashauriano yangefaa zaidi.

Kulingana na Pilcher na Imelda (2004), wafeministi hawa wanashuku kuwa itikadi ni pingamizi katika uletaji wa usawa wa kijinsia katika jamii. Wanalaumu hali ya kutamani wajibu tofauti kulingana na jinsia katika jamii. Kwa mujibu wao, wanaume na wanawake wanafaa kuwa na mipaka bayana ya kiwajibu kulingana na jinsia. Kwa kuzingatia mtazamo huu, nafasi ya mwanamke huchukuliwa kuwa jikoni na ulezi wa watoto.

Aghalabu jamii nyingi za Kiafrika humtarajia mwanamke kuwajibikia kazi za nyumbani na malezi ya watoto. Naye mwanamume hutarajiwa kushughulikia masuala ya ulinzi, uongozi na maamuzi. Mawazo haya ni ya kiitikadi na kuyakiuka kunaleta mabadiliko. Waandishi wamedhihirisha hali hizi katika tamthilia teule za utafiti huu.

Katika tamthilia ya *Kilio cha Haki* (Mazrui:1981), Mwengo, babake Lanina anamwambia Lanina:

> MWENGO: "Na wewe binti ya shetani!
> Mimi si wanaume wale wengine
> Unaowachezeachezea
> Mimi si kina Mwengo.
> Mimi ni dume kweli kweli.
> ..................................................
> Kaa nalo ulifunze adabu na heshima!
> Ulifunze maana ya *uuke!* (uk. 38)

Utamaduni umemfunza Seromanga kwamba mke hapaswi kuwa na tabia za 'kiume' kama kupigania haki na usawa. Umemfunza kwamba Mwengo hapaswi kupika , kufagia na kufua. Yeyote anayejaribu kubadilisha kaawaida hata kama ni mbovu ni "msaliti". Jamii imempa Seromanga uwezo wa kuwapiga mkewe na bintiye ili awe mtii. Lanina anapigwa ili udume wake ukomeshwe, ili afuate tabia za kike.

Katika kioski cha mzee Ingeli, wafanyakazi fulani wanafikiri Lanina ni chambo cha kuvutia wanunuzi. Wengine wanamtaka mapenzi japo anawaambia ni mke wa mtu. Wakati akiwa kizuizini Hatila na Kachero Ben wanajaribu kumvunjia heshima na kumnajisi. Saikolojia yao inayotokana na mfumo wa kiuchumi na kitamaduni inawapa dhana kuwa mwanamke daima yuko ili amhudumie mwanamume. Imani hizo zinakashifiwa katika *Kilio cha Haki.*

Mila na itikadi kali hazipaswi kufuatwa ikiwa zinamdunisha mwanamke. Tamaduni nyingi za Kiafrika zimelazimika kubadilika ili kuleta usawa wa kijinsia. Kama asemavyo Lanina, hatupaswi kuwa watumwa wa utamaduni tuliofinyanga. Utamaduni ni zao la jamii lakini haufai kumweka mhusika mateka na 'mfungwa'. Lanina anapinga itikadi kali zinazokandamiza. Ni mwenye moyo thabiti na msimamo imara. Suala la utabaka linaweza kuzuka lakini kimsingi ni usawa wa kijinsia ambalo ndilo suala nyeti hapa. Mwengo anapolalamika kuwa anawapikia wanawe siku nyingi anaambiwa:

Lanina:Kwa nini sisi tuwe watumwa wa utamaduni wetu!
Mwengo....
Si sisi tuliofinyanga utamaduni?
Si sisi tulioupa uhai utamaduni...
uhai wa kutuongoa?
Basi kwa nini tuuache utamaduni
Ututie pingu na fahamu zetu kututawalia
Utupige pande na tabia yetu ya kuzingatia?
nini Mwengo!...
Tuendelee kuufuata utamaduni
Hata uwapo makosani yakini? (uk. 32)

Mwandishi Wamitila (2003), amedhihirisha hali ya itikadi kali katika tamthilia ya *Pango*. Katango anakabiliwa na pingamizi chungu nzima. Seki aliye baba yake anamshutumu kwa kukiuka tamaduni kwa kutaka kuingilia siasa. Anamwambia:

Seki: Hudhani? Hudhani? Kwani kuna cha kudhani hapa?
(*Akimwangalia Katango*) Huyu utamwamini? Mwone
Anavyokwenda kinyume na utamaduni kabisa!
Utamaduni gani huo? Umesikia wapi wewe
Mwanamke ameshika mata na mishale katika jamii
Hii? (*Kwa nguvu zaidi*) Ehh niambie, hiyo elimu ya
Kizungu kilikupa ujasiri wa kuipuuza mila? (uk. 18)

Jamii yake Katango inashikilia mila za mwanamke kutoshika ala za vita. Ni uasi kwa mujibu wa Seki. *Utawezaje kufanya jambo ambalo hawafanyi wanawake? Kitendo kama hicho kinaweza hata kutuletea nuhusi...* Seki ni mtamaduni na ana imani kuu kwa mila na itikadi zao. Bado anaongezea kuwa, itikadi ni *Imani zetu; roho ya kuwepo kwetu; uboho wa mifupa ya jamii.* Seki anaendelea kumkashifu mwanawe Katango kuwa aliyeasi mila anaposema, *Wewe tangu ugomee kupashwa*...(uk.19).

Tunapochunguza maongezi ya baba na mwanawe tunaona kuwa hata kupashwa tohara ni mila aliyoikaidi Katango.

Waandishi Mazrui na Njogu (2006), katika tamthilia yao ya *Sudana*, tunapata ya kuwa wahusika wa kiume Amerigo na Muzungu wanamnajisi Sudana. Baada ya najisi hii ni vyema kumtakasa mama yao ili wasipatwe na nuhusi. Shume anawaambia ndugu zake:

> Shume:Kwa hivyo kwanza ni lazima tumtoharishe mamaetu, tumtakase na najisi iliyompata. Bila ya hivyo, idadi ya ndugu wanaonajisika itaongezeka kati yetu, ndugu ambao, kwa athari ya najisi hiyo, huendelea kutusaliti kwa kila njia. Bila hivyo, kizazi chetu kitahasirika kwa miaka yote. Wakati huo huo ni lazima tujitoe mhanga ... (uk. 45)

Waandishi King'ei na Mohamed (2008), katika tamthilia ya *Posa za Bikisiwa* wanamsawiri kiongozi wa kike Bikisiwa aliyemakinika na aliyejinasua kutoka mikatale ya mila na itikadi. Usasa na mambo ya maendeleo kama utandawazi una athari kuu katika kiongozi huyu. Hata mfalme, aliye babake Bikisiwa anaafiki haya anaposema:

> Hiki ni kizazi kipya. Hii ni enzi ya uhuru na ushindani. Vijana wanadai uhuru wao. Uhuru wa mawazo na kufukiri na kufanya wanavyopenda. Uhuru wa kusaili na kutafiti mila, sheria, kanuni na desturi. Uhuru kujiamulia na kujichagulia. (uk.61)

Ni bayana kuwa waandishi hawa wamedhihirisha nafasi dhalilishi aliyoko kingozi wa kike. Uhafidhina huu unaonekana kukwamiza harakati za kumkomboa mwanamke. Kwa hivyo udumishaji wa uhafidhina utadumisha ubabedume. Hii itamaanisha kuwa mwanamke azidi kuitikia hali dhalilishi na mwanamume kudumisha hadhi ya yake ya juu.

### 4.3 Masuala ya Kiuchumi Yanayofafanua Harakati za Ukombozi

Ufanisi wa harakati za kujenga usawa wa kijinsia una changamoto tele. Kikwazo kikuu hasa ni uwezo duni wa mwanamke kiuchumi. Mwanamke yeyote, hasa walio viongozi wana uwezo wa kudai haki yao ya kujitegemea kiuchumi. Hata hivyo hawana uwezo wa kudhibiti nyenzo za uzalishaji mali. Tujuavyo ni kuwa mhitaji hana chaguo isipokuwa kuitikia matakwa ya mfadhili wake. Wanawake

wamelazimika kuwa wategemezi wa wanaume kiuchumi. Wanawake, hata awe kiongozi wamelazimika kunyenyekea mbele ya waume zao wanapoolewa. Kwa mujibu huu wanaume wameelewa udhaifu huu wa wanawake, wanajihifadhia hadhi kwa kuwapa wanawake masharti fulani.

Lanina, aliyeongoza wafanyakazi wengine kazini katika *Kilio cha Haki*, amepevuka na ana msimamo wake thabiti kuhusu masuala ya wafanyakazi wote waume kwa wake. Jamii ya kiafrika anamosawiriwa inamtambua mwanamume kuwa mmiliki wa mali na nyenzo za uzalishaji mali hayo. Lanina anafaulu kuwaunganisha wafanyakazi wenzake wapiganie haki zao. Ni kiongozi anayeelewa nadharia ya kimapinduzi. Anaamini katika nguvu za wafanyakazi na jukumu lao la kihistoria la kuubadilisha mfumo wa kibepari ili wafanyakazi wapate stahiki yao. Lanina haogopi kumvunja Delamon kwa sababu anajua kwa yakini kuwa Delamon ni adui yake. Hata anaapomkaribisha chai (uk.12) anakataa kwa uthabiti. Anafahamu kusudi la delamon ni kufanya urafiki wa kinafiki awateke Lanina na Tereki kisaikolijia wawasaliti wafanyakazi na waanze kushirikiana naye. Lanina anapinga mfumo huu wa kiuchumi na propaganda zinazoambatana kwa sababu ya upevu wake wa kisiasa na uelewaji wake wa nadharia ya ukoloni.

Taylor (1985), katika makala yake *Women: A World Report* anagusia suala hili. Anaeleza namna mtoro msichana huwasaidia wazazi wake, punde anapoolewa, anamsaidia mumewe kuchuma mali. Anaeleza hata hivyo kuwa mchango huu wote unakosa kutambuliwa na jamii. Mwanamke hukosa kupiga hatua kiuchumi kwa sababu ya kutomiliki nyenzo kuu za kiuchumi. Anaangazia bara la Afrika, ambapo umbapo umaskiminini suala nyeti. Anaona chanzo cha hali yenyewe kuwa ni kasumba za kikoloni, utamaduni, mifumo ya kisiasa na sera zisizofaa *What Do African Women Want? 1995:137).*

Mfumo wa kiuchumi humpa mwanamume umiliki wa nyenzo za kuzalisha na kudhibiti mali. Jamii nayo inamwona mwanamke kama msaidizi wa mwanamume lakini hamiliki chochote. Badala yake, anahesabiwa kuwa sehemu ya mali ya mwanamume. Mke, watoto, shamba na mifugo ni mali ya mwanamume. Akifafanua suala hili, Newland (1979) anasema kuwa jamii nyingi zinaonekana kuendeleza ubaguzi wa kijinsia dhidi ya wanawake. Anasema katiba za kisasa zinaonekana

kumpendelea mwanamume. Anatoa mfano wa kanuni za Kirumi zilizosanifishwa na Napoleon Bonaparte ambazo zinamkweza mwanamume na kumtweza mwanamke. Kanuni zenyewe zinamchukulia mwanamke kuwa mali ya mwanamume. Mwananmke yuko chini ya mwanamume kulingana na kanuni zenyewe.

Katango, kiongozi wa kike katika tamthilia ya *Pango*, aliye mwalimu haruhusiwi na wanajamii wake kuendeleza ndoto yake ya kuliongoza pango. Anapingwa na hata kudhulumiwa kwa kuwa na maono kama haya. Jamii nyingi katika bara la Afrika, hazimpendelei kiongozi wa kike. Ushauri potovu wanaompa baba yake na hata mama yake ni kwanza, aolewe ili atiwe adhabu na mumewe. Mgogoro unazuliwa ambapo hata tunamwona mama yake Katango hajui ampe mwanawe ushauri upi kuhusu uongozi. Tunamwona akitongoa ubeti wa ushairi akisema:

Mama: Ndiyo njia panda hii tuliyo,
... mume huku, mwana huku
... mwanamke na mwanamume
yupi ni yupi??? (uk.23)

Tuligundua kuwa, wanaume katika jamii nyingi barani Afrika ndio humiliki pesa na hata wana ushawishi mkuu wa kifedha. Pesa huwa chanzo cha uongozi mbaya. Wao hutumia pesa ili wabaki mamlakani miaka nenda miaka rudi. Tunamwona mhusika Jitu katika tamthilia ya *Pango* ana ushawishi mkuu wa kifedha. *Pesa...Pesa...Pesa bwana! Hiyo ndiyo dawa yake! ... Nina uzoefu mkubwa katika utumishi... . . . Anayenipinga ninamlainisha kwa pesa tu* (uk.83). Taswira halisi imejitokeza hapa kuwa wanaume ndio walio na mfumo huria wa kiuchumi. Wanaume wanatumia pesa kubaki uongozini.

Bikisiwa, mhusika aliye kiongozi wa kike katika tamthilia ya *Posa za Bikisiwa* hamiliki nyenzo za uzalilishaji mali. Wanaokuja kumposa wanakuja na zawadi tele za kumshawishi ili akubali wamuoe. Anakataa katakata lakini hawachoki kumletea zawadi tele. Yote haya yanasaidia kuelezea mfumo wa kiuchumi unavyosaidia kufafanua harakati za ukombozi

Hassan ni mwanamume anayemsihi kwa vitu kochokocho, *...hatimaye anamkabidhi Bikisiwa magauni ya hariri, herini za dhahabu, kidani cha dhahabu chenye vito vya thamani, manukato...* (uk.33). SS pia ni mwanamume anayemletea Bikisiwa zawadi

tele ili ampose. *...Pete za dhahabu. Sakini za kupigania vita. Magauni ya hariri. Vyombo vya mapambo vyenye vito vyema. Farasi na watumishi wote hawa* (uk. 39)

Sudana ndiye kiongozi wa kike katika tamthilia ya *Sudana,* hana uwezo wowote wa kifedha. Haya yanalemaza shughuli zao hasa urekebishaji wa wa mashua yao. Tunamwona Amerigo akiwaambia akina Sudana kuwa, *Msijali, hapa mtapata msaada muutakao mpaka mashua yenu iwe imetengenezeka* (uk.13).

**4.3 Hitimisho**

Katika sura hii, tumezifafanua baadhi ya athari na changamoto zinazoonekana kukwamiza ufanisi katika kujenga usawa wa kijinsia katika *Kilio cha Haki*, *Pango, Posa za Bikisiwa na Sudana.*Kwanza tumeangazia asasi za kitamaduni zinazoonekana kudidimiza mwanamke katika jamii. Mwanamke amepewa nafasi duni katika jamii yake. Mwanamume naye amepewa udhibiti wa mila na desturi zinazomkandamiza mwanamke.

Pili, tumeangazia mfumo wa kiuchumi unavyofafanua harakati za ukombozi wa wanawake. Mwanamume ana udhibiti wa kiuchumi. Mfumo wa kiuchumi humpendelea na kuzidi kumwinua mwanamume. Haya yanaonekana kurutubishwa na utamaduni, kasumba za kikoloni na mfumo wa kijamii kwa ujumla.

## SURA YA TANO
## MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.1 Utangulizi

Utafiti huu ulilenga kuchunguza nafasi na athari ya kiongozi wa kike katika tamthila za *Pango* (Wamitila:2003), *Sudana* (Mazrui na Njogu:2006), *Posa Za Bikisiwa* (Mohamedna King'ei: 2008) na *Kilio cha Haki* (Mazrui:1981).Kwa kuongozwa na nadharia ya Ufeministi, tulijikita katika eneo la Afrika. Hii ni kwa sababu tamthilia zenyewe zimetungwa katika mandhari ya Kiafrika. Kwa sababu hiyo tumeteua tapo hili kimuktadha. Sura hii itashughulikia muhtasari, matokeo, mahitimisho na mapendekezo kuhusu tafiti za baadaye.

### 5.2 Muhtasari wa Utafiti

Uchanganuzi huu ulikuwa na madhumuni ya kubaini nafasi na athari ya kiongozi wa kike katika tamthilia teule za Kiswahili. Kwa minajili ya kufikia lengo kuu la utafiti wetu tuligawanya tasnifu hii katika sura tano.

Sura ya kwanza ilishughulikia mambo ya kimsingi ya utafiti ambapo tuliangalia usuli wa utafiti, mada ya utafiti, nadharia tete, mipaka na upeo wa utafiti, sababu za kuchagua mada, umuhimu wa utafiti, msingi wa kinadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada na hatimaye mbinu za utafiti. Sura hii ilikuwa ya umuhimu sana katika utafiti wetu mzima kwa sababu ndiyo iliweka msingi wa ufafanuzi wa malengo.

Katika sura ya pili tulichanganua dhana za tamthilia na uhusika. Maelezo ya kina yalitolewa kuhusu uteuzi wa wahusika wa kike walio vongozi katika tamthilia teule. Katika sura ya tatu tilipambanua nafasi ya kiongozi wa kike katika tamthilia teule za Kiswahili. Nafasi mbili zilichunguzwa kwa kina ambazo ni dhalilishi na chanya. Katika sura ya nne ya utafiti huu tulishughulikiaathari ya kiongozi wa kike katika jamii husika katika tamthilia teule za Kiswahili. Nayo sura ya tano tulishughulikia muhtasari wa matokeo, hitimisho na mapendekezo ya utafiti wetu.

### 5.3 Matokeo ya Utafiti

Katika utafiti wenyewe tulikuwa na madhumuni mawili, kwanza tulilenga kuchunguza nafasi anayopewa kiongozi wa kike katika jamii. Pili tulilenga kuchunguza athari za kiongozi wa kike katika jamii husika. Jamii nyingi za kiafrika zilishikilia mfumo wa kiutamaduni ambapo ulimdhalilisha na kumnyanyasa mwanaume kwa kumfanya awe ni mali na milki ya mwanaume na kwa kumfanya

mwanamke awe udhibiti na milki ya mwanaume ni hali ambayo *Greer (1970)* anapinga asasi za kiutamaduni ambazo kwa muda mrefu zimetumiwa kumdhalilisha mwanamke katika jamii na kumchukua mwanamke kama miliki na mtegemezi wa mwanaume kwa kila jambo.

Mwanamke alijulikana kama mtu asiyeweza kuzalisha au kumiliki chochote bali ni mzigo kwa mwanaume, na kutokana na mtazamo huu wanaume hujiona kama wanadamu vielelezo, wenye vyeo, heshima na hadhi kubwa kuliko wanawake. *Greer* anaangazia hali inayowakabili wanawake hasa wanaoishi vijijini. Wanawake kama hawa aghalabu huwa hawana miungano, kwa hivyo huishia kuwa miliki na wategemezi kwa wanaume wao katika kila hali ya kimaisha.

Asasi ya utamaduni ilimsawiri mhusika mkuu Lanina kushughulikia kazi za nyumbani. Mwengo, mumewe Lanina anamwambia kwamba utamaduni wao haumruhusu mume kuwapikia na kuwaosha watoto. Hiyo ni kazi ya mwanamke. Mwanamke hapaswi kuchelewa nyumbani na anapaswa kufika mapema kuihudumia jamii yake anaonekana kuathirika na kauli hii ya Mwengo. Utamaduni huu unaompendelea mwanamume ndio ambao unamzindua Lanina na kumwathiri kiasi kwamba sasa amejazwa na hamu ya kutafuta ukweli ulikofichika. Lanina hapumziki hadi ameridhika na usawa wa jinsia zote. Mamake Lanina naye ameathirika na utamaduni unaomdunisha.

Kwa wanawake kukomboa nafsi zao zilizolemaa na daima kumpembeja mwanamume na hata kama viongozi wanakumbwa na changamoto kuzichukua hatamu za uongozi katika jamii iliyotawaliwa na taasubi ya kiume.Ndiposa malezi ya mtoto wa kiume, anavyoeleza Millet (1969) humfanya na kuunasibisha uume na matumizi ya nguvu, utundu na umilikaji wa kila kitu. Anasema kuwa malezi haya humfanya mwanamume kutumia kiungo cha uume kuwanyanyasa wanawake.

Utamaduni huu una athari yake kwa kiongozi wa kike kwa sababu unamponza mwanamke na kumfanya mwanamke awe ni adui ya mwanamke pindi tu mwanamke kama vile Lanina anasimama dhabiti kuukosoa utamaduni uliojaa kasumba tele, kuna wanawake wengine waliotekwa nyara na kuabudu utamaduni ndiposa kwa kauli yangu kupitia kazi hii ya A. Mazrui anatoa rai yake kwamba utamaduni haupaswi kufuatwa ikiwa unamdunisha.

Kisiasa, mwanamke huchukuliwa kama mtu asiye na hekima na busara ya kuongoza. Ilikuwa ni kasumba kwamba mkia hauwezi ukaongoza kichwa kwa vyovyote vile. Mwanamke halisi hayawezi masuala ya uongozi. Kwa mujibu wa Greer (1969), kichwa -mwanaume - ndiye aliyepewa kipaumbele cha kuongoza na utamaduni ambao waasisi wake hatujawatambua. Utamaduni huu umepitwa na wakati. Kipindi kipya kimewadia kwa yeyote yule aliye na tajriba na uwezo kupewa nafasi ili kuwepo mabadiliko katika sera mbalimbali. Akizidi kuwaangazia wanawake anasema kuwa, aghalabu mara nyingi huwa hawana miungamo kwa hivyo huishia kunyamaa na kutoonekana wakitaka kuwania uongozi. Maana yake ni kazi ya kiume kama utamaduni unavyoviweka vigezo vyake.

Mfumo wa ubabedume ulimchukulia mwanaume kama mdhibiti na kiongozi bora huku mwanamke akichukuliwa kama mkia kuongozwa na mwanaume na kuwa msaidizi katika mambo ya nyumbani tu. Beauvior (1949), anatoa fasili ya uongozi huu wa ubabedume, anaeleza kuwa namna ambavyo mwanamke huchukuliwa kama mtu asiyeweza kuongoza, bali ni mtu ambaye anapaswa kuongozwa huu ni uongozi wa kiutamaduni ambao umepitwa na wakati. Beauvoir anapinga kaida hizi zinazomkosea heshima na kukiuka haki za mwanamke.

Ubabedume huu ulimwathiri Katango kiasi kwamba siku ya uamuzi na siku ya kumteua kiongozi atakayelilinda ‘pango’, Ngwese kwa msaada wa baba yake Katango na wazee wengine walitumia vishawishi kuwarai wanajamii kumchagua Ngwese ambaye ni mnafiki badala ya kulinda pango la jamii alichaguliwa kuliiba na kulichafua ‘pango’. Juhudi za Katango kwenye kampeni zake ziliambulia patupu licha ya kisomo chake na ndoto yake ya kulikomboa ‘pango’. Japo hawakumpa kura vitendo vya Ngwese hatimaye vilibainika wazi na kweli Ngwese hakuingia uongozini kilinda ‘pango’, bali kuivunja ‘pango’ na kosa la wanajamii kutomchagua Katango kama mlinzi wa pango linawaathiri na wanajuta laiti wangalimchagua mwanamke labda angelinda ‘pango’ kwa manufaa ya wanajamii wote.

Pana uwezo na mchango muhimu kwa kiongozi wa kike katika ujenzi wa jamii mpya, nguvu za mwanamke ambazo zikiimarishwa zitakuwa msingi muhimu katika jamii yenyewe na zitahakikisha usawa na haki kwa jinsia zote mbili. Japo kuna uonevu na kudhalilishwa kwa wanawake, sasa wanawake wamezinduka kujikomboa na mikatale ya utamaduni inayowadunisha huku ikimwinua kihadhi mwanaume.

Kwa njia mojawapo ya kusisitiza haja ya kumkomboa mwanamke, mwandishi wa tamthilia ya *Pango*,alimuumba mwanamke jasiri, kiongozi bora, mwenye akili tambuzi na akamfanya mwanamke mhusika mkuu katika tamthilia. Mhusika huyu mkuu ni Katango ambaye ni kielelezo cha kuendeleza harakati za ukombozi wa mwanamke katika jamii iliyotawaliwa na mfumo wa kiume. Mwandishi anafanya hivyo kwa nia ya kuitafakarisha jamii razini hasa wanawake kuhusu haja na namna ya kujinyakulia ukombozi wao.

Suala la usawa katika jamii ni la kimsingi, kisa na maana ni kwamba wake na waume wanastahili kujitahidi kwa ushirikiano katika kupiga vita ubabedume. Maumbile hayawezi kubadilishwa lakini mfumo mbaya unaweza badilishwa kwa sababu ni tokea la jamii yenyewe. Jamii inaweza badili mfumo ulioanzishwa na wanajamii wenyewe. Kilichoanzishwa na jamii kinaweza kubadilishwa na jamii husika.

Msanii ametumia sanaa yake kumuinua mwanamke katika tamthilia ya *Pango* kihadhi na kuzindua jamii kuhusu haja ya kutambua mchango muhimu wa mwanamke katika jamii kwa jumla. Nafasi anayompa Katango ililenga kudhihirisha kuwa jamii itafaulu kubadili mkondo wa mambo endapo wanawake na wanyonge watajasiria na kupinga mazoea ya mila na desturi zinazowakandamiza.

*Posa za Bikisiwa (*2008), tamthilia ya Said A. Mohamed na Kitula King'ei. Katika tamthilia waandishi walifaulu kubainaisha nafasi na athari ya kiongozi wa kike. Tuliainisha nafasi dhalilishi na dunishi anamowekwa mwanamke yaani - nafasi ya pili - baada ya mwanamume na nafasi chanya kama walivyobainisha waandishi kwa namna ya kumwinua na kumjenga mwanamke kihadhi.

Tuchanganua na kupambanua nafasi na athari ya kiongozi wa kike katika thamtilia *Sudana* (2006). Katika uchunguzi wetu tumeweza kutafiti nafasi mbali mbali na athari zinazotokana na uongozi wake. Nafasi zenyewe zinajidhirisha wazi katika vitengo viwili vikuu: nafasi dhalilishi na nafasi chanya.

Katika uchunguzi wetu tulipata kuwa nafasi dhalilishi anayopewa mwanamke katika uongozi wake katika jamii ya *Sudana* kuna kuenea sana kwa taasubi ya kiume ambapo mila na desturi zinampendelea na kumpa kipaumbele mwanamume na kumtesa mwanamke. Mitazamo hii ambayo ni mikatale ya utamaduni inamsawiri mwanamke kama chombo cha mapenzi, chombo cha kuzaa na kulea, kuonewa kwa

sababu ya maumbile, uhusiano wa kudunisha mwanamke katika hali ya juu katika jumuiya ya *Sudana*.Katika sehemu ya pili, tuliangazia nafasi chanya anayopewa mwanamke. Waandishi walijenga mwanamke kihadhi na kumwinua katika jamii inayomdhalilisha na kudunisha.

Suala la usawa wa kijinsia lilipewa kipaumbele katika tamthilia ya *Sudana*. Waandishi wameangazia ukinzani wa kimtazamo ulivyo kuhusu nafasi ya mwanamke kama kiongozi katika jamii na athari anazokumbana nazo na hili linatupa taswira jinsi mfumo huu umejikita na kujijenga katika mila na desturi baguzi za jamii husika.

Nafasi ya mwanamke katika jamii imekuwa kadri jamii za ulimwengu zinavyochukua muundo. Mfumo wa kibepari umekita mizizi kwenye jamii ya *Sudana* kwani mwanamke hana hadhi yoyote mbele ya wanaume. Taasubi za kiume zimekolea mno na hali hii ndiyo *Alamin Mazrui* na mwenzake *Kimani Njogu* wanavyomsawiri mhusika wao mkuu Sudana na jinsi anakumbwa na udhalilishaji huu kwenye jamii yake anapowania ukombozi na uhuru wa watoto wake. Nafasi dhalilishi na dunishi tutakazozingatia ni kama vile: mwanamke kama chombo cha mapenzi, mwanamke kama milki ya mwanaume na kadhalika.

Kama njia mojawapo ya kusisitiza haja ya kumkomboa mwanamke katika jamii, waandishi walimuumba mwanamke jasiri, huru na mlezi mwema. Wakamfanya mhusika mkuu. Huyu ni Sudana, anayetumika kama kielelezo cha harakati za ukombozi wa mwanamke katika jamii inayotawaliwa na mfumo wa kiume. Anafanya hivyo kwa nia ya jamii razini na hasa wanawake kuhusu haja na namna ya kujinyakulia ukombozi wao.

Wanjiku na Akinyi (1993), wanatoa pendekezo kuhusu suala la kijinsia kwamba wanawake kwa wanaume wanastahili kujitahidi kwa ushirikiano katika kupigania vita ubabe dume katika jamii. Wanaeleza kwamba maumbile hayawezi kubadilishwa lakini mfumo unaweza kubadilishwa kwa sababu ni tokeo la jamii, mazoea na desturi. Kwao jamii inaweza kubadili mfumo ulioanzishwa na wanajamii wenzao.

Kwa maoni yao, kile kilichoanzishwa na jamii kinaweza kubadilishwa na jamii iyo hiyo. Waandishi hawa wametumia mwanamke kama mhusika mkuu kumwinua kihadhi na kuizindua jamii kuhusu haja ya kutambua mchango muhimu wa mwanamke. Nafasi wanayompa Sudana inalenga kudhihirisha kuwa jamii itafaulu

kubadili mkondo wa mamboendapo wanawake na wanyonge watajasiria na kupinga mazoea na desturi zinazowakandamiza.

Wafeministi wanapinga malezi yanayorutubisha na kuzua ukinzani na ukandamizaji wa wanawake. Kwa mujibu wa Millet (1969) mtoto wa kiume hulelewa kwa njia ya kumwandaa kuwa mwanaume na kiongozi, mwenye uwezo wa kudhibiti na kutumia nguvu kujikidhia haja zake za kiume. Anazidi kueleza kuwa namna ambavyo mtoto wa kiume anapoionea fahari kiungo cha uume katika jamii iliyojaa taasubi za kiume na kuchukulia kama silaha ya kuwanyanyasa wengine kiungo hiki huchukuliwa kama uwezo wa mwanaume.

Asasi za jamii kama utamaduni huongoza maisha ya wanajamii, matarajio yao na hata utendakazi wao. Kulingana na Pilcher na Imelda (2004), wafeministi hawa wanashuku kuwa uhafidhina ni pingamizi katika uteteaji wa usawa wa kijinsia katika jamii. Aghalabu, wanawake kwa wanaume wangependa kuwa na mipaka bayana kulingana na jinsia. Kwa kuzingatia mtazamo huu, mwanaume amepewa jukumu la kushughulikia maswala ya ulinzi, uongozi na maaamuzi. Maamuzi ya masuala ya kijamii katika jamii nyingi za Kiafrika aghalabu hutekelezwa na mwanaume. Jamii zenyewe humpa usukani na udhibiti mwanaume.

Kwa hivyo, maamuzi ya familia, jamii na maisha kwa jumla ni shughuli ya mwanamume. Ingawa mwanamke huwa na mchango muhimu katika maamuzi ya masuala ya kijamii, aghalabu hashirikishwi. Kwa kuzingatia hali hizi, waandishi walionekana kuelewa udhalilishaji, udunishaji na nafasi chukivu wanayopewa wanawake katika jamii. Kwa maoni yetu, waandishi hawa wamefaulu kubainisha nafasi dhalilishi anayopewa kiongozi mwanamke.

Kwa upande mwingine waandishi hawa pia waliweza kumjenga na kumwinua kihadhi kiongozi mwanamke, waandishi wa tamthilia hizi nne: K.W Wamitila *(Pango*), Alamin Mazrui (*Kilio cha Haki*). Kimani Njogu (*Sudana*) na Said A Mohammed na Kitula King'ei (*Posa za Bikisiwa*). Waliweza kuzindua jamii ili iweze kutambua umuhimu wa kiongozi wa kike na kuutilia maanani umuhimu huu katika jamii. Waandishi hawa walitumia wahusika wao wakuu: K.W Wamitila (*Pango*) alimhusisha Katango, Alamin Mazrui (*Kilio cha Haki*) alimhusisha Lanina, Kimani Njogu na Alamin Mazrui (*Sudana*) walimhusisha Sudana na Said A Mohammed na Kitula King'ei (*Posa za Bikisiwa*) walimhusisha Bikisiwa. Wote hawa kwa kutumia

sifa chanya walimsawiri mwanamke kama mwenye bidii, kiongozi bora, mlezi mwema wa watoto na mwenye akili tambuzi ili kufanikisha shughuli zao za kumsawiri mwanamke kama kiongozi ambaye anafaa kuenziwa na kupewa fursa kuongoza.

Utafiti wetu tulichunguza jinsi mwanamke anavyoathiriwa na changamoto mbali mbali na vikwazo vinavyokwaza mwanamke katika uongozi wake. Tulibaini wazi kuwa asasi za ndoa, utamaduni na ubabedume unavyoathiri viongozi wanawake. Katika kuzichunguza athari hizi tuliongozwa na nadharia ya ufeministi wa kiafrika unaotambua utamaduni kuwa suala kuu. Nafasi chukivu anayopewa mwanamke katika jamii inarutubishwa na utamaduni unaodhibitiwa na mfumo wa kiume. Ndiposa kwenye kazi hizi, waandishi hawa wamedhihirisha mchango wao muhimu katika harakati za kumkomboa mwanamke katika ujenzi wa jamii mpya.

**5.3 Mahitimisho**

Waandishi walifaulu kupambanua nafasi dhalilishi na chanya anamowekwa mwanamke na jamii inayomwenzi na kumkweza mwanamume. Jamii ya aina hii ina mfumo unaompendelea mwanamume na kumtweza mwanamke kutokana na anavyosawiriwa katika tamthilia. Kulingana na Wafula na Njogu (2007), mwanamke amewekwa katika kitengo maalum katika jamii kwa sababu ya jinsia yake ya uke.

Katika tamthilia hizi viongozi wameonyesha nguvu za wanawake kupitia Katango *(Pango*), Lanina (*Kilio cha Haki*), Bikisiwa (*Posa zaBikisiwa*) na Sudana (*Sudana).* Kutokana na juhudi zao wanawake wenyewe wamedhihirika kuwa viongozi wanaofaa licha ya athari na changamoto zilizoko kwenye jamii.

Waandishi hawa walimsawiri kiongozi wa kike kama mhusika mkuu katika kuleta nafasi ya kiutawala. Mwanamke ana nafasi ya kuchangia katika asasi mbalimbali za kijamii na hivyo, anastahili aachwe ili awajibikie nafasi hiyo vilivyo. Licha yachangamoto tele mhusika huyu ana athari za kimapinduzi ili kujenga jamii mpya.

**5.4 Mapendekezo**

Utafiti huu ulilenga kuchunguza nafasi na athari ya kiongozi wa kike katika tamthilia nne teule za lugha ya Kiswahili. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Ufeministi wa kiafrika. Watafiti wa baadaye wanaweza kutafiti mada hii kwa kuongozwa na nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa. Utafiti mwingine unaweza kufanywa kuhusu mada hii katika riwaya teule za lugha ya Kiswahili.

Watafiti wengine pia wanaweza kuchunguza dhima ya utamaduni na athari yake, katika masuala ya usawa wa kijinsia katika tanzu zingine za fasihi kama vile hadithi fupi, riwaya na hata ushairi. Nadharia ya Umarksi na Ujamaa zinaweza wafaa. Tafiti zilizo pendekezwa zitanufaisha sio tu wasomi wa fasihi na hata wasomi wa sosholojia.

## MAREJELEO


Beauvoir, S. (1969: 690). '*Second Sex'*. London: Routledge.

Beckson, K & Ganz, A. (1960). *Literary Terms:* A Dictionary: New York:Farran.

Briskin, L. & McPhail, M. (1998). Study Of Women and Education: Feminist, Philosophical Reflections on Reproductive Rights in Canada. Toronto: University of Toronto Press.

Burhani, Z. (2003). Usawiri wa Wahusika Wanawake Waislamu. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (isiyochapishwa)

Chioma, F.S. (1981). *Black Woman and Survival. A Maroon Case*. London: Wellsley

Devries, J. (1999). *Contemporary Literature*. Newyork. Ether Pub. Ltd.

Felder, K. (1996). *Empowering the woman*. New York: Bighton Publishers Ltd.

Holman, C. H (1960). *A Handbook to Literature*. New York: The Odyssey Press Inc.

Jackson, P. (1999). *Understanding West Literal works*. Dublin. Ireland Pub. Ltd.

Katola, E. (2006). Dhuluma dhidi ya wahusika wa kike katika tamthilia za Kiswahili. Tasnifu ya uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (isiyochapishwa).

Katwina, R. (2012). Uchanganuzi wa Mwanamke kama Mhusika. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Kimani, N. (1997). Uhakiki wa Riwaya za Visiwani Zanzibar. Nairobi University Press, Nairobi, Kenya.

Kimani, N. na Wafula, R. (2007). Nadharia za Uhakiki wa Fasihi. Nairobi. Sai Industries Limited.

Kimani, N. na Chimerah, R. (1999). Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu. Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi.

King'ora, M.N. (2014). Utendaji katika tamthilia za Sudana na Kimya Kimya. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Kinoti, T.M. (2008). Fasihi Simulizi na Utamaduni. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Kombo, D. & Tromp D.L.A. (2006). *Proposal and Thesis Writing: An Introduction*. Nairobi: Paulines Publications Africa.

Kruger, G(1998). *The Illusion of Superiority among Humans*. Journal Paper.

Trotsky, L. (1924). *Literature and Revolution*. New York: Russell & Russell Press.

Lugano, N. (1989). Usawiri wa mhusika wa kike katika riwaya tatu za Kezilahabi. Chuo Kikuu cha Kenyatta. Tasnifu ya Uzamili. (isiyochapishwa)

Lukacs, G. (1963). *Realism in the Balance*. Budapest: Heines Press.

Maingi, J. (2005). *Uhakiki wa Fani katika Ngano teule za Kiswahili*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mayore, M. (2007). Taswira ya Mwanamke katika tamthilia za Kiswahili. Chuo Kikuu cha Nairobi. Tasnifu ya Uzamili. (isiyochapishwa)

Mavisi, R. (2011). Usawiri wa wahusika wa kike katika kazi za Zainabu Burhani.Chuo Kikuu cha Kenyatta. Tasnifu ya Uzamili. (isiyochapishwa)

Mazrui, A. (1981). *Kilio cha Haki*. Nairobi. Longhorn Publishers.

Mazrui, A. Na Njogu K. (2006). *Sudana*, Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.

Mbatiah, M (2001).*Kamusi ya Fasihi,* Nairobi: Standard Textbooks and Graphics and Publishing Ltd.

Millet, K. (1969:20), *Sexual Politics*. New York: Doubleday &Co.

Mirikau, S. A. (2011). *Taswira ya Mwanamke katika Tamthilia za Wamitila*. Chuo Kikuu cha Nairobi. Tasnifu ya Uzamili. (isiyochapishwa)

Mohamed, S. Na King'ei K. (2008) *Posa za Bikisiwa*. Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.

Moi, T. (1985). *Textual Politics: Feminist Approach of Literal Theory*. London: Routledge.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*, Nairobi: East African Educational Publishers Ltd. M. Press.

Muchiri, P. M. (2011). *Lugha ya Wanawake Wakikuyukatika maongezi ya kawaida.* Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (isiyochapishwa)

Mugenda, O. & Mugenda, A. (1999) *Research Me*thods. Nairobi: Acts

Mugambi, P. (1982). *Ecumenical Initiatives in Eastern Africa*. Nairobi: AMECEA

Muindi, A. (2012). *Usawiri wa Wahusika Makahaba katika riwaya za Said Ahmed Mohammed.* Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (isiyochapishwa)

Mukobwa, J. (1987). *Influence of Kenyan Educators on Curriculum: A Case Study*. Toronto: University of Toronto Press.

Mulila, J. (2009). *Usawiri Chanya wa Wahusika Wanawake*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mwanakombo, S. (2008). *Changamoto zinazokumba jinsia ya* kike. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (isiyochapishwa)

Mwanje, I. J. (2001). *Qualitative Research Process: Social Science Research Methodology Series, Module 2*. Addis Ababa: OSSREA

Mwenderani, R. (2012). *Taswira ya Mwanamke katika Tamthilia mbili za Kiswahili*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (isiyochapishwa)

Mwihaki, C. N. (1998). *The Image of the Woman in African Oral Literature: The case of Swahili and Gikuyu Proverbs*. Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Ndungo, C. (1985). *Wanawake na Mabadiliko ya Kihistoria katika Fasihi ya Kiswahili*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Ramatoulaye. M. (1980:10). *So Long a Letter*. Heinamann: Hardback &Paperback.

Rodney, W. (1972). *How Europe Underdeveloped Africa*. London: Bogle L'Ouverture

Senkoro, F.E.M.K (1982). *Fasihi*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.
-----------(1987). *Fasihi na Jamii.* Dar es Salaaam: Press and Publicity Centre.

Syambo, K. na Mazrui A. (1992). *Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Thirkettle, G. L (1980). *Business Statistics and Interpretation*. London: Stalin Publishing Ltd.

Thiong'o, N. et al (2001). *Masuala ya uana katika jamii za kiafrika*. Chuo Kikuu cha Nairobi. Makala ya Kongamano.

Truex, M. (1969). *Language Policy and Research of Language Issues*. London: Oxford University Press.

Wafula, R. M. (1987). *Uhakiki wa Tamthilia: Historia na Maendeleo yake.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wafula, R. N. & Njogu, K. (2007:92). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: JKF.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi : Jomo Kenyatta Foundation.

______________*(2003). Pango,* Nairobi. Focus Publishers Limited.

______________(2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Publishers.

_______________(2003). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi.* Nairobi: Focus Publications Limited.

_______________ (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uhakiki na Uchanganuzi wa Fasihi.* Nairobi: Vide-Muwa Publishers Ltd.

Wanjiku, M. na Akinyi, R. (1993:13). *Elimination of All Forms of Discrimination Against Women*. Nairobi: EAEP.

Wollstonecraft, M. (1792). *A Vindication of the Rights of a Woman with Strictures on Political and Moral Subjects*. New York: W.W. Norton Company.

## KIAMBATISHO A

## MASWALI YA KULENGA ILI KUPATA DATA YA UTAFITI HUU

**(a) Masuala ya kimsingi ya utafiti huu**

(i) Ni ipi misingi ya utafiti huu?

..................................................................................................................................

(ii) Ni pengo lipi litazibwa katika fasihi ya Kiswahili na utafiti huu

..................................................................................................................................

(iii) Madhumuni yepi yataongoza utafiti huu na umuhimu wake ni upi?

..................................................................................................................................

(iv) Ni mipaka ipi ya kudhibiti uchangannuzi wa data iliyokusanywa?

..................................................................................................................................

(v) Ni kundi lipi la kulengwa katika utafiti huu?

..................................................................................................................................

(vi) Ni kutoka matini ipi data itadondolewa na itachanganuliwa vipi?

..................................................................................................................................

**(b) Muhtasari wa Tamthilia Teule za Kiswahili**

(i) Utungo wa tamthilia ni upi kama utanzu wa fasihi andishi?

..................................................................................................................................

(ii) Ni ipi historia fupi ya tamthilia teule ili kazi hii ya sanaa iweze kufaidi utafiti huu?

..................................................................................................................................

(iii) Dhana ya uhusika itachambuliwa vipi ili kutosheleza mada ya utafiti?

..................................................................................................................................

(iv) Wahusika wa kike walio viongozi waliteuliwa vipi ili kutosheleza wajibu wao?

.......................................................................................................................................

**(c) Nafasi ya Kiongozi wa Kike Katika Tamthilia Teule za Kiswahili**

(i) Ni nafasi gani aliyopewa kiongozi wa kike katika tamthilia teule?

.......................................................................................................................................

(ii) Mhusika wa jinsia ya kike aliye kiongozi amedunishwa vipi katika tamthilia teule?

.......................................................................................................................................

(iii) Nafasi chanya inadhihirika vipi katika kiongozi wa kike aliye mhusika katika tamthilia teule?

.......................................................................................................................................

**(d)Athari Inayomkabili Kiongozi wa Kike Katika Tamthilia Teule za Kiswahili**

(i) Ni asasi zipi za kitamaduni zinazomwathiri kiongozi wa kike katika tamthilia teule?

.......................................................................................................................................

(ii) Asasi ya ndoa inamkabili vipi kiongozi wa kike katika tamthilia teule?

.......................................................................................................................................

(iii) Mila na itikadi zinamkabili vipi mhusika huyu wa kike aliye kiongozi katika tamthilia teule za Kiswahili?

.......................................................................................................................................

(iv) Ni masuala yepi ya kiuchumi yanayofafanua harakati za ukombozi kama kioo cha jamii nyingi barani Afrika?

.......................................................................................................................................

## KIAMBATISHO B

**NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE, TECHNOLOGY AND INNOVATION**

Telephone: +254-20-2213471, 2241349, 310571, 2219420
Fax: +254-20-318245, 318249
Email: secretary@nacosti.go.ke
Website: www.nacosti.go.ke
When replying please quote

9th Floor, Utalii House
Uhuru Highway
P.O. Box 30623-00100
NAIROBI-KENYA

Ref: No.

**NACOSTI/P/15/7023/4348**

Date:
**18th March, 2015**

Martha Nyangweso Syekei
Maasai Mara University
P.O.Box 861-20500
**NAROK.**

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION**

Following your application for authority to carry out research on ***"Nafasi na athari ya kiongozi wa kike katika tamthilia teule za Kiswahili,"*** I am pleased to inform you that you have been authorized to undertake research in **Kisii County** for a period ending **31st August, 2015.**

You are advised to report to **the County Commissioner and the County Director of Education, Kisii County** before embarking on the research project.

On completion of the research, you are required to submit **two hard copies and one soft copy in pdf** of the research report/thesis to our office.

**DR. S. K. LANGAT, OGW**
**FOR: DIRECTOR GENERAL/CEO**

Copy to:

The County Commissioner
Kisii County.

The County Director of Education
Kisii County.

APPROVED

COUNTY COMMISSIONER
KISII COUNTY

COUNTY DIRECTOR OF EDUCATION
KISII COUNTY
P. O. Box 4499 - 40200, KISII
Date

*National Commission for Science, Technology and Innovation is ISO 9001: 2008 Certified*

# KIAMBATISHO C

**CONDITIONS**

1. You must report to the County Commissioner and the County Education Officer of the area before embarking on your research. Failure to do that may lead to the cancellation of your permit
2. Government Officers will not be interviewed without prior appointment.
3. No questionnaire will be used unless it has been approved.
4. Excavation, filming and collection of biological specimens are subject to further permission from the relevant Government Ministries.
5. You are required to submit at least two(2) hard copies and one(1) soft copy of your final report.
6. The Government of Kenya reserves the right to modify the conditions of this permit including its cancellation without notice

**REPUBLIC OF KENYA**

NACOSTI

**National Commission for Science, Technology and Innovation**

**RESEARCH CLEARANCE PERMIT**

Serial No. A 4494

CONDITIONS: see back page

THIS IS TO CERTIFY THAT:
*MS. MARTHA NYANGWESO SYEKEI*
of MAASAI MARA UNIVERSITY, 4139-40200 KISII, has been permitted to conduct research in *Kisii County*

on the topic: *NAFASI NA ATHARI YA KIONGOZI WA KIKE KATIKA TAMTHILIA TEULE ZZA KISWAHILI*

for the period ending:
*31st August,2015*

Permit No : NACOSTI/P/15/7023/4348
Date Of Issue : 18th March,2015
Fee Recieved : Ksh 1,000



*Applicant's Signature*

*Director General*
*National Commission for Science, Technology & Innovation*